# Kweli Muhimu Sana

*Mtazamo Halisi, wa Biblia kuhusu Maisha ya Kikristo*

J. Cliff Canipe

Kweli Muhimu Sana
Mtazamo Halisi, wa Biblia kuhusu Maisha ya Kikristo
© 2020 na Cliff Canipe & Equippers International. Haki zote zimehifadhiwa.
Vifungu vya maandiko vimenukuliwa kutoka kwa Biblia ya Swahili Union Version (SUV) ©2014 (SUV) na nyingine zilizotajwa.
Herufi za italiki zilizotumiwa kwa dondoo za Maandiko zimeongezwa na mwandishi.

Kimechapishwa na Equippers International
P.O. Box 126002
Benbrook, TX 76126

ISBN: 978-0-578-71280-2
eISBN: 978-0-578-71684-8
LCCN: 2020911178

Haki zote zimehifadhiwa. Isipokuwa dondoo fupi zinazotumiwa kwa makusudi ya kufafanua, sehemu yoyote ya kitabu hiki isinakiliwe au kutumiwa kwa jinsi yoyote kwa njia ya elektroniki au ya mitambo, kurekodi, au kutoa nakala, kuhifadhi na kutoa habari bila idhini kutoka kwa mchapishaji.

Kimechapishwa Marekani
Toleo la Kwanza 2020

*Kwa Stephanie, Camille, Natalie, na Wesley, kwa uvumilivu mwingi na upendo wenu kwangu kama mume na baba. Safari yetu pamoja imekuwa ya kushangaza!*

# Shukrani

Mojawapo ya furaha kuu maishani hupatikana unaposhiriki na wengine furaha hiyo. Mimi hushangazwa na jinsi Mungu huwaleta watu wanaofaa maishani mwetu kwa wakati ufaao. Watu wengi sana wamechangia pakubwa katika safari yangu binafsi. Asante sana Ken, John, Mike, na Gene, waliokuweko katika miaka yangu ya mwanzo kama muumini. Nawashukuru wale wote waliochangia pakubwa kuniwezesha kugundua maisha ya kushirikiana na Roho kwa kina wakati ambao nafsi yangu ilitamani kuwa ndani ya Roho zaidi. Nawashukuru maprofesa wote walionipa hekima na maarifa wakati wa masomo yangu ya kitaaluma.

Shukrani kwa Vern Fromke, ambaye kitabu chake—"No Other Foundation"—kilitokea katika nchi ambayo haikutarajiwa kabisa na kikanitingiza kwa kwa hali ya ajabu. Kwa wengine, wakiwemo E. Earle Ellis, T. Austin Sparks, Watchman Nee, Dan Stone & David Gregory, na James Fowler, nawashukuru nyote kwa kujitolea kwenu kumjua Bwana na kushiriki na wengine Yule mliyempata. Watu hawa wote wameathiri safari yangu kwa kiwango kikubwa, wamesaidia kukuza imani yangu, na kunipa maneno kwa wakati ufaao kuhusu kile ambacho roho yangu ilikuwa ikiona. Nimekutana na wengine wenu binafsi. Kwa wale ambao hatujakutana, siku moja tutakutana nao mbinguni, na nina hakika ushirika huo utakuwa mzuri sana.

Asanteni sana Rene Brown na Jack Horn, wazee wanyenyekevu sana walio katika safari hii ya Kikristo na ambao wamenionyesha mfano wa maana ya kumpenda Yesu kwa moyo wangu wote na kuwa na njaa ya kupata kweli inayopatikana tu kwa kutumia muda mwingi katika maombi, mazungumzo, majadiliano, na kunywa vikombe vingi vya chai pamoja. Mmenifunza kwamba hata wazee hujifunza!

Nashukuru jamii yangu ambayo kila mara imenisaidia kumfuata Bwana kwa gharama yoyote ile, na wakati mwingine wamehitajika kufanya kile ambacho huenda hawakuwa tayari au radhi kukifanya wenyewe. Kujitolea kwenu ni manukato mazuri mbele za Bwana.

Mwisho, Ningependa kumshukuru mtu mmoja katika maisha yangu ambaye ni himizo langu kubwa zaidi. Asante, Stephanie—mke wangu wa ajabu—kwa msaada wako usiokoma na kwa kunihimiza nimfuate Yesu zaidi. Asante kwa mazungumzo (na mijadala) isiyoisha ambayo tumefanya kwa miaka mingi iliyopita, na kuwa radhi kushiriki nami kwa undani zaidi mambo ya imani na mambo unayosadiki. Asante kwa stadi zako za uhariri wenye thamani na za uhakiki. Naiheshimu sana safari yako na Yesu na ufahamu wako wa Maandiko. Wewe ni Barnaba wangu katika kila hali-mhimizaji wangu na taji yangu.

# Pendekezo

Kitabu hiki cha Kweli Muhimu Sana ni mojawapo ya madhihirisho wazi ya kila kitu ambacho Mungu ametupatia ndani ya Kristo ambacho nimewahi kusoma—Mimi mwenyewe nimeandika kuhusu kweli hii kwa miaka 25. Cliff Canipe anatoa mafundisho murwa ya biblia, na vilevile anafumia ndani mifano mizuri ya namna ya kuenenda kwa imani katika Kristo aliye ndani yetu. Kwa yeyote anayejiuliza iwapo kuna mengine zaidi ndani ya maisha ya Kikristo kuliko kujaribu sana kwa nguvu zako mwenyewe bila mafanikio, hili ni jibu kwako! Nilibarikiwa sana na kitabu hiki, na ninakipendekeza sana.

David Gregory
Mwandishi wa kitabu kilichouzwa zaidi cha
*The New York Times' Dinner with a Perfect Stranger* na
*The Rest of the Gospel: When the Partial Gospel Has Worn You Out*

Nimemjua Cliff kama mfafanuzi wa injili aliye na shauku ya kweli, na vilevile rafiki mpendwa na mwaminifu. Kila kitu anachokifunza ni kweli aliyoidhihirisha maishani mwake. Nashukuru kwamba amefikia kiwango ambacho ameweza kushiriki na wengine kwa njia hii, ufunuo na mambo aliyoyapitia ya Agano Jipya. Kitabu hiki kinashughulikia baadhi ya kweli muhimu sana ya msingi ya maisha ya Kikristo. Kila mada imeshughulikiwa kwa njia inayofikika yenye kina na yenye kuweka huru. Hiki si kitabu unachoweza kusoma bila kutilia maanani, bali ni kitabu kinachokufanya uwe na hamu ya kushiriki na wengine.

Philip Du Toit, PhD
Mhadhiri Mkuu wa Agano Jipya
North-West University, South Africa

Nimemjua Cliff tangu mwaka wa 1993, na amekuwa mmoja wa rafiki zangu wa karibu sana maishani. Tumecheka pamoja, tumelia pamoja, tumeomba pamoja, tumesafiri pamoja, na tumehudumu pamoja. Yeye hachoki katika safari ya kumfuata Kristo, kufuata kweli ya injili, ufafanuzi wa Agano Jipya la Ufalme wa Mungu, na kweli ya neno la Mungu. Kitabu hiki ni cha kutia moyo, cha msingi, cha kuelimisha,ch enye ufafanuzi, kamili, sahihi, kilichojaa ufunuo—cha kiroho na halisi—chenye changamoto, na hata cha kukabiliana na mambo kwa njia bora zaidi iwezekanavyo. Ninampendekeza kabisa pamoja na kitabu chake!

Rick Montgomery
Mkurugenzi, ZEB'S Foundation
Texas, United States

Kwa wale walio na hamu kuu ndani ya roho zao kupata kitu kinachozidi kile wakionacho kanisani

jinsi wanavyokifahamu au walivyofunzwa, kitabu cha Dkt. Canipe kitafungua taswira mpya kabisa. Kila sura ya kitabu hiki inafunua mada iliyo muhimu kwa safari yetu ndani ya Bwana Yesu Kristo. Kutokana na chembe hizi muhimu za kweli, wengi watatiwa moyo kuzama zaidi katika imani wanapokuj kumjua Bwana wao kwa njia mpya za ajabu.

Rene P. Brown
Foundation Ministries International
Texas, United States

Sisi ni kizazi chenye uwezo mkubwa wa kufikia habari, makala, mahubiri, vitabu, ujumbe, na mafunzo ya Kikristo ambacho kimewahi kuishi katika historia ya mwanadamu. Hata hivyo, kutokana na uhalisi wa kutokomaa kweingi na ukosefu wa majibu halisi kutoka kwa Kanisa hadi kwa matatizo ya jamii ya kihisia, kimwili, na kiroho, naweza kusema kwamba kizazi chetu kinahitaji kumtegemea Kristo zaidi ya nyakati zote. Tunahitaji Kweli Muhimu Sana ili kupata mgeuzo tunaokamia sana ufanyike. Zaidi ya yote, tunahitaji kurudi kwa misingi ya Biblia inayosababisha mtazamo halisi wa kubadilika kwa mtu binafsi na kuathiri vizuri sehemu zote za maisha yetu na jamii zetu kwa jumla. Kila sura ya kitabu hiki ni mwaliko wa kuishi maisha halisi ya imani na ukomavu ndani ya Kristo. Ni kitabu kinachoondoa mzigo wa udini, kinachoeleza misingi ya Kikristo kwa njia rahisi bila upendeleo. Mbali na kukipendekeza kitabu hiki, ninapendekeza hasa maisha, jamii na huduma ya Cliff, kwani ninajua upendo na shauku aliyo nayo kwa injili. Ni heshima kubwa kwangu kusoma na kuipendekeza kazi ya rafiki yangu ya imani na utiifu.

Hiago Angelucci
Mkurugenzi wa Mafunzo, University of the Nations
Curitiba, Brazil

Kuna watu wengi wanaoandika vitabu siku hizi. Hauhitaji kuwa mtu mwenye hulka nzuri au hata mfuasi Yesu mwenye shauku ili uweze kuandika kitabu cha "Kikristo", ingawa hilo husaidia. Cliff anatosha kabisa. Anampenda Yesu, jamii yake, na jirani zake. Pia Cliff ni mwandishi mwenye akili nyingi na pia ana kipawa. Clliff ametumia maisha yake yote kukiishi kitabu hiki. Kinunue. Kisome. Kitumie katika maisha yako. Utahimizwa kumpenda Yesu na jirani zako pia.

Richard Henderson
Mwanzilishi, Fellowship of the Sword
Texas, United States

# Dibaji

Mbona niandike kitabu kuhusu maisha ya Kikristo? Bila shaka kuna vitabu vingi vilivyoandikwa kuhusu mada hii. “Mbona?” ni swali ambalo nimejiuliza mara nyingi kwa miaka mingi. Nadhani ni swali ambalo kila mwandishi hujiuliza kabla ya kuandika kitabu. Kitu nisichotaka kufanya ni kurudia yale ambayo wengine tayari wamesema. Lakini hili haliwezi kuepukika. Mwandishi wa kitabu cha Mhubiri alitwambia kwamba hakuna jambo jipya chini ya jua (Mhu. 1:9). Sitaki kuwa mwenye kiburi kwa kudhani kwamba nina jambo jipya la kusema ambalo halijawahi kusemwa hapo awali.

Kwa miaka mingi nimepewa changamoto na kuchangamshwa na watu mbalimbali kupitia vitabu vyao na safari yao ya kuenenda na Bwana. Nilitaja baadhi ya watu hao katika sehemu ya shukrani hapo juu. Lakini lazima kuwe na sababu ya uwezo wa kujitegemea katika uandishi wa kitabu kuliko kutoa muhtasari tu na kuwasilisha mawazo ya wengine. Nafikiri hatimaye nimeipata sababu hiyo.

Nimehimizwa kueleza yale niliyoyapitia na vile yameathiri maisha yangu binafsi na safari yangu na Bwana kwa miaka thelathini na nne iliyopita. Sitasema kwamba kila kitu kilicho ndani ya kitabu hiki ni kweli iliyo kamili, lakini nina hakika kwamba kina kweli nyingi. Nikiwa na imani hiyo, natoa mawazo yangu kuhusu maisha ya Kikristo.

Kuna hali moja ya kipekee kwa mtazamo ninaokusudia kutumia ambao ni kichocheo kwa yote nitakayoshiriki katika kurasa hizi. Nina hamu kuu ya kutoa mtazamo halisi kabisa na vilevile mtazamo wa biblia kwa maisha ya Kikristo. Kuna sababu kadhaa zinazofanya mtazamo huu kuwa muhimu sana kwangu.

Kwanza, nimekuja kufahamu kwamba maisha ya Kikristo ni jitihada halisi linalotuwezesha kupata uhalisi wa Yesu aliye hai ndani ya maisha yetu kila siku. Kusema kweli, Ukristo ni Kristo na maisha ya Kikristo yanahusu kumjua Yeye. Kwa sababu hii, kila kitu ninachoshiriki kinatoka kwa shauku kuu ya kuhimiza watu na kuwasilisha hali halisi ya kukutana na Yesu na kuwa na maisha yaliyobadilishwa. Tunahitaji kumjua Bwana kwa kweli na kisha tutumie imani yetu kushiriki naye kwa njia ya kuabudu na kuwa na uhusiano wa karibu. Ni matumaini yangu kwamba unaposoma na kuingiliana na kweli iliyo ndani ya kitabu hiki itakuwa ni kana kwamba “tunadhihirisha utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi” (2 Kor. 3:18).

Pili, nataka kuwasilisha mtazamo wa bibilia kwa kila kitu ninachoshiriki. Tangu nilipokutana na Yesu mwaka wa 1986, kila mara nimekuwa na shauku kuu ya kuyajua Maandiko. Hii ilinielekeza kusoma na hatimaye kusomea shahada ya uzamivu au PhD katika Uinjilisti na Agano Jipya mwaka wa 1997. Wengi wa wasomi wenzangu waliamua kufuata vyeo vya kitaaluma kama wahadhiri, watafiti, na wasimamizi, huku Bwana akiniongoza katika uwanja wa misioni. Baada ya miaka mingi ya kufanya huduma katika mazingira mbalimbali, ikijumlisha shule za mafunzo ya misioni, makanisa, na kongamano za uongozi vijijini mwa nchi zote za Afrika Mashariki na Kusini pamoja na nchi zilizo Ulaya, Asia, na Marekani Kusini, nimekuja kuamini kwamba kuna hitaji kubwa katika mwili wote wa Kristo la waumini kukita mizizi ndani ya kweli iliyo ndani ya maandiko.

Kila mmoja wetu ana safari yake binafsi na Bwana. Muda unapoendelea, Yeye huyaelekeza na kuyaongoza maisha yetu katika njia ya mtu binafsi. Hii haimfanyi mtu awe bora au mbaya kuliko mwingine. Ni kweli kwamba sote tuko tofauti. Nakubali kwamba safari yangu na Bwana iliniongoza kwanza kupitia kipindi cha masomo magumu ya kitaaluma. Nilibahatika kupitia miaka hiyo nikiwa bado nina imani yangu na vilevile shauku ya kujua zaidi kuhusu Yesu. Kutokana na mambo niliyopitia, ninawapa kioo cha pekee cha kutumia kuyatazama maisha ya Kikristo. Ni kioo kinachochanganya vitu hivi viwili; mtu kukutana binafsi na Yesu na kuyafahamu maandiko kwa kina.Natumai mtazamo huu utakuhimiza na kukuwezesha kuyaona mambo kwa jinsi mpya na pia ya kukupa uhai.

Kitabu hiki kina maandiko mengi! Kila mara mimi hukumbushwa kile ambacho Yesu aliwaambia Mafarisayo kuhusu Maandiko:

> "Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima" (Yohana 5:39-40).

Katika juhudi zetu za kuyaelewa maandiko na kujifunza zaidi kuhusu Mungu kupitia neno Lake, tunatakiwa kuwa waangalifu tusiwe kama Mafarisayo. Tunapaswa kukumbuka kila mara kwamba ni Yesu ambaye hatimaye hutupa ufunuo kupitia kwa Roho Wake ili tuweze kumjua Yeye vyema zaidi. Jambo muhimu zaidi ni kumwendea Yeye. Tunapofanya hivyo, Maandiko yatafanya kile ambacho yanatakiwa kufanya-kufichua mengi zaidi kuhusu Yesu.

Ningependa kukusaidia kuona jinsi Maandiko yanashuhudia wazi kweli ya maisha ya Yesu yaliyo ndani yako kama muumini. Kusoma na kuyachunguza Maandiko sio mwisho wa mambo. Tunapofichua kweli iliyo ndani ya Maandiko, yatatusukuma mbele zaidi kukutana na Yeye.

Nitasema pia kutoka mwanzo kwamba haya si maelezo kamili ya kila kitu ninachoamini kuhusu maisha yetu kama waumini. Kushiriki kuhusu sehemu zote za maisha ya Kristo hakuwezi kutoshelezwa na kazi ya kitabu kimoja. Kuna mambo mengi ambayo sitayajadili katika kurasa hizi. Haya yanajumlisha mambo kama kukuza hisia njema, nidhamu za kiroho (kama maombi, kuyatafakari Maandiko, na kunuia), na utenda kazi wa kila mshirika aliye katika mwili wa Kristo, nikitaja machache tu. Mada hizi na nyingine muhimu zitangoja majadiliano yatakayofanyika baadaye Bwana atakavyoongoza.

Maandiko yote katika kitabu hiki yako hapa ili kuunga mkono kila ninachoshiriki kwa kutumia Biblia. Maandiko hayo pia ni kwa manufaa yako. Nikuhimiza uchukue muda wa kuyasoma Maandiko hayo unapopitia kila sura ya kitabu hiki.

Kitabu hiki, hakitakuwa kama vitabu vingine, kuendelea kama hadithi au kukuza maudhui maalum. Kitabu hiki ni, uwasilishaji wa kweli kama inavyohusiana na baadhi ya mambo mengi muhimu ya kitambulisho chetu cha kiroho.Siwasilishi mambo haya kwa kupendekeza taratibu ya kuanza na mambo yaliyo muhimu.Hapo mwanzo mambo hayo yataonekana kama hayahusiani au yameachana. Lakini mambo haya yanahusiana kwa njia yenye kutatanisha kabisa, na yote yanatumika kama matofali ya kujenga kitambulisho chetu kama wana wa Mungu.

Yafuatayo ni baadhi ya maswali nitakayoshughulikia. Haya ni maswali ninayosikia mara tena na tena ninapokaa na Wakristo katika sehemu nyingi za ulimwengu.

- Je, Mungu ana kusudi na maisha yangu?
- Ni nini maana ya kuishi kwa imani?
- Nitapokea vipi neema ya Mungu katika maisha yangu?
- Wajibu wa Roho Mtakatifu katika maisha yangu ni nini?
- Ni nini maana ya kuwa mwenye haki?

- Ni dhambi ngapi zangu zilizosamehewa, na ni vipi ambavyo naweza kupata msamaha wa Mungu?
- Je, nahitaji kutubu dhambi zangu kwa Mungu ili aweze kunisamehe?
- Ninawezaje kuishi bila dhambi?
- Mbona bado nasumbuliwa na dhambi katika maisha yangu baada ya kuwa Mkristo?
- Mbona maisha ni magumu sana, hata baada ya kuwa Mkristo?
- Je, kuna njia ya kupata amani na pumziko la kweli katika maisha yangu?

Iwapo kuna kitu ninachotaka kutimiza kupitia kitabu hiki, ningependa kukusongeza karibu na Yesu Kristo. Kwani Yeye ndiye msingi wa maisha (1 Kor. 3:11) na kweli yote inatoka kwake na inapitia kwake (Yohana 14:6), inafaa kila kitu kielekezwe kwake. Naamini kwamba unaposoma kila sura ya kitabu hiki utahisi Mungu akijenga kitu fulani kilicho imara ndani ya maisha yako.

Kama nilivyosema, ningependa kukuunganisha na Neno la Mungu na Roho Mtakatifu atakayewaongoza katika kweli yote(Yohana 16:13). Sitaki kitabu hiki kijitokeze kama somo la kitaalam, au kitabu cha kufanya ibada tu. Ningependa kisaidie kukuonyesha njia ya wewe kukutana na nguvu za kweli ya Neno linalowekwa moyoni mwako kwa kazi ya Roho Mtakatifu na maisha ya Kristo yaliyo ndani yako!

Kila sura itamalizika kwa kipindi cha ibada fupi. Sehemu ya Kuifanya Upya Nia Yako itakusaidia kutumia kweli muhimu kutoka kwa sura hiyo na vilevile kukupa tamko la imani unaloweza kutumia kuimarisha kweli hiyo katika maisha yako. Sehemu ya Kuenenda Katika Kweli itakupa hatua za namna ya kuenenda katika kweli ya kila sura, kila siku.

Ombi langu ni kwamba utahimizwa na kutiwa nguvu, na kwamba utajikuta unampenda Yesu zaidi na kushangazwa na utajiri wake usiopimika (Efe. 3:8). Asante kwa kuchukua muda wa kusoma kitabu hiki. Naamini kitakuwa cha manufaa kwako.

# Utangulizi

Yesu akamwambia, "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima" (Yohana 14:6); na "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote" (Yohana 16:13); na "tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru" (John 8:32). Kuwa na ufahamu wa kweli kumhusu Yesu humpa mtu wingi wa neema ipatikanayo kwa kuwa na hakika kamili ya ufahamu kwa sababu hazina yote ya hekima na ufahamu vimefichwa ndani Yake (Kol. 2:2)!

Nakumbuka vizuri sana tukio langu la kufanyika Mkristo na kuanza uhusiano wangu binafsi na Mungu. Ilikuwa Juni 1986 nilipoomba na ninakubali kwamba nilimhitaji Yesu. Wakati huo, miaka thelatini na nne iliyopita, nilikuwa na ufahamu mchache sana au hata ufunuo kuhusu maana ya kuwa Mkristo. Sawa na watu wengi, nilidhani kwamba kuwa Mkristo kulimaanisha maisha yangu yangeundwa ili mambo yaniendee vizuri katika siku za baadaye. Na wakati huo nilihitaji hilo sana maishani mwangu! Kuongeza kwa maisha yangu kutatuliwa, pia ningepata kuishi na Mungu milele, ambayo mara nyingi huitwa "tikiti ya kwenda mbinguni." Wazo hilo lilikuwa na maana kabisa wakati huo, na itikio langu la kumpa Bwana maisha yangu lilikuwa muhimu na la kweli.

Nikaanza safari ya kuishi maisha yangu mapya na Bwana. Nilijifunza upesi kutoka kwa watu wenye nia nzuri mambo waliyoamini kuwa ni shughuli za lazima na nidhamu kwa kila Mkristo. IMambo hayo yalijumlisha kusoma Biblia yangu kila siku, kuomba kila siku, kutoa muda wangu na pesa zangu kwa njia halisi (pamoja na fungu la kumi), kuwa mshirika mwaminifu wa kanisa, kuwaeleza watu imani yangu kila mara, na orodha hiyo ilikuwa ndefu.. Kwa hivyo, nilijishughulisha kufanya mambo hayo yote. Ni kana kwamba nilikuwa na kazi mpya na baada ya muda fulani nilifanya mambo hayo vizuri sana.

Haikunichukua muda mrefu kutambua kwamba kuyafanya mambo yote mazuri hakukuniunganisha kwa uzima wa Yesu na kweli Yake. Muda ulipoendelea, nilianza kugundua kwamba mawazo mengi niliyokuwa nayo kuhusu Mungu na maisha ya Kikristo yalikuwa pungufu, na mengine yalikuwa yenye makosa kabisa. Miaka thelatini na nne iliyopita imekuwa safari ya kuendelea kujifunza, kukua, kubadilika, na zaidi ya yote, kumjua Yesu zaidi.

Katika miaka hiyo yote, nimekuja kuyaona mambo kwa dhahiri kabisa. Nimekutana na kweli ambayo imeniweka huru. Pia nimejifunza kwamba huku kweli yote ikiwa ndani ya Yesu, kweli hiyo ina kweli nyingine nyingi ya kina na ya maana sana inayotakiwa kuunda imani yetu na ufahamu wetu kuhusu Mungu na pia kujua sisi ni nani kama waumini. Kweli hiyo isipoimarishwa ndani ya maisha yetu, tutang'ang'ana sana ili kuishi maisha kama alivyokusudia Mungu tuishi.

Kuna mada nyingi zinazohusiana na maisha ya Kikristo. Nyingi ni muhimu na za manufaa, ingawa zote si muhimu sana. Sidhanii kwamba mada zote nitakazojadili hapa ni orodha iliyo kamili au zina kweli yote. Hii ni kweli ambayo nimeiona kuwa muhimu sana wakati nimetafuta kumjua Mungu zaidi na kupata kipawa cha uzima alichonipa ndani ya Yesu Kristo. Ni Kweli Muhimu Sana.

Kusema jambo ni muhimu sana kuna maana kwamba jambo hilo ni la lazima kabisa au lina umuhimu

mkuu. Kusema jambo ni muhimu sana pia kuna maana kwamba mambo mengine si munimu sana. Nitawezaje kubainisha tofauti hiyo? Nitasema kwamba chochote kilicho ndani ya uhusiano wetu na Mungu tunachoweza kufanya kwa juhudi zetu wenyewe si muhimu sana. Hii ina maana kwamba mada zilizo ndani ya kitabu hiki ni mambo ambayo Mungu ametimiza kwa matendo Yake mwenyewe kwa manufaa yetu. Ni kweli inayotoka kwa uzima wa Yesu na kazi aliyokamilisha kwa niaba ya wanadamu wote. Kusema ni muhimu sana kuna maana kwamba ni ya lazima maishani mwetu kwa ajili ya kufurahia uzima ambao Mungu alitukusudia mwanzoni. Hili huenda likawa ndilo jambo muhimu zaidi kuhifadhi katika nia yako unaposoma kitabu hiki.

Kweli muhimu sana ni ya lazima kwetu ili tuishi maisha ya Kikristo kwa njia inayoleta mgeuzo na maana ya kina. Si orodha ya mambo unayoyafanya, bali ni kweli unayopata, unayoamini, na unayoruhusu iyaunde maisha yako.

Katika kile tunachokiita Mahubiri ya Mlimani, Yesu alitangaza kwamba nyumba ya mtu huwa imara sawa na msingi uliojengewa nyumba hiyo (Mat. 7:24-27). Mtume Paulo alisema, "…Hakuna mtu awezaye kuweka msingi mwingine badala ya ule uliokwisha wekwa, yaani Yesu Kristo" (1 Kor. 3:11). Nataka kukaa karibu na msingi huu kadri iwezekanavyo ili nijenge kwa dhahabu, fedha, na mawe ya thamani ili kazi yangu idumu (1 Kor. 3:14).

Hiki si kitabu cha "namna ya kufanya" mambo yanayohusu maisha ya Kikristo. Sitaki kukuacha ukifikiri au ukiwa na mzigo huu kwamba kuna mengi zaidi unayotakiwa kufanya ili uwe Mkristo bora zaidi. Badala yake, ningependa kushiriki nawe kweli yenye nguvu na ya kukupa uzima kwamba, ukiamini, maisha yako yanaweza kugeuzwa yafanane na mfano Wake (Rum. 8:29), na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa kwa ajili yetu (Ebr. 12:1).

Yesu pia alitwambia kwamba tutaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itatuweka huru (John 8:32). Neno "fahamu" linajitokeza wazi ninaposoma kifungu hiki. Nimekuja kuelewa kwamba tukiifahamu kweli ndipo kweli hiyo hutuweka huru. Shauku yangu ni kukusaidia kuipata kweli hiyo. Wajibu wako ni kufahamu na kuamini kweli ili iweze kukuweka huru.

Safari yangu ya kiroho imenipa uhusiano wa maana sana na wangu binafsi na Yesu Kristo. Pia nimepata mgeuzo wa kudumu na wa kuyabadilisha maisha kwa kuutazama utukufu wake (2 Kor. 3:18). Mgeuzo huu umetegemea ufunuo mwingi wa kweli ninayojua kuwa ni ya kudumu na yenye kugeuza kwa sababu kweli hiyo haitegemei mambo niyafanyayo au nisiyoyafanya. Inahusiana na kile alicho Yesu na kile ambacho amefanya.

Huu ndio niuitao utaratibu wa "Kuundwa kiroho." Kuundwa kiroho lazima kufanyike iwapo utawahi kuupata uzima ndani ya Kristo anavyokusudia Mungu na kukua "hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo" (Efe. 4:13). Kuundwa kiroho hakufanyiki kwa shughuli za kidini kama vile: kwenda kanisani, kusoma Biblia, na kuishi maisha mazuri. Kuundwa kiroho hufanyika tu tunapomjia Bwana kwa imani kamili na kushirikiana na Yesu aliye hai, kila siku.

Utayarishe moyo wako kwa ajili ya kweli unayoenda kuipata. Huenda ikawa mpya, tofauti, au yenye changamoto ikilinganishwa na kile ambacho umesikia katika safari yako ya Kikristo. Iwapo utaifunua nia yako na kumuuliza Roho akufunze unapoendelea kusoma kitabu hiki, Naamini itakuwa baraka kuu kwako. Hebu tuanze safari hii pamoja na tuone itatuelekeza wapi.

# 1

# KUSUDI

*Tunapogundua nini maana ya kuishi katika mandhari yake ya milele, na kutazama sehemu mbalimbali zinavyohusiana na hali nzima, tutaona jinsi ilivyo muhimu kuwa na mwanzo unaofaa.*

*~ DeVern Fromke*

*Kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu. Katika yeye tunao ujasiri na uwezo wa kukaribia katika tumaini kwa njia ya kumwamini.*

*~ Waefeso 3:11-12*

Je, umeshawahi kuuliza swali hili, "Kusudi langu maishani ni lipi?" Swali hili liko ndani ya moyo wa kila mtu. Ungamo la Westminster la 1647 linauliza swali hili, "Ni nini hatima kuu ya mwanadamu?" kisha linajibu, "Hatima kuu ya mwanadamu ni kumtukuza Mungu, na kumfurahia daima."

Watu wana kiu cha kujua jibu la swali hili la zamani sana. Kitabu cha Rick Warren cha mwaka wa 2002, The Purpose Driven Life: What on Earth Am I Here For? (Maisha Yanayoelekezwa na Kusudi: Niko Hapa Duniani Kufanya Nini?), kinathibitisha hili. Kitabu hicho kinawasilisha yale ambayo Warren anasema ni makusudi matano ya Mungu kwa maisha ya mwanadamu hapa duniani na zaidi ya nakala milioni 18 ziliuzwa!

Hakuna shaka kwamba Mungu ana kusudi katika kila jambo alifanyalo. Tunaona hili katika Biblia nzima. Ayubu alisema haya kuhusu Mungu, "Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika" (Ayubu 42:2). Katika bustani ya Gethsemane Yesu alimwomba Baba ayaokoe maisha Yake asipitie wakati wa mateso, lakini hatimaye alisema, "...Lakini ni kwa kusudi hili nimeufikia wakati huu" (Yohana 12:27 NEN). Petro na Yohana walisema katika Matendo 4 kwamba watu wengi walikuwa wamekusanyika Yerusalemu kumdhuru Yesu, wakiwemo, "Ni kweli Herode na Pontio Pilato pamoja na watu wa Mataifa na Waisraeli, wakafanya yale ambayo uweza wako na mapenzi yako yalikuwa yamekusudia yatokee tangu zamani" (Matendo 4:27-28 NEN). Paulo alisema "Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu" (Matendo 20:27). Yohana alitwambia, "Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi" (1

Yohana 3:8b). Vifungu hivi vyote vinaonyesha kwamba Mungu hutenda mambo kulingana na yale aliyokusudia kutenda.

Kusudi lina maana kwamba kuna sababu ya jambo fulani kufanyika. Hatupaswi kushangaa kwamba Mungu hutenda mambo kulingana na kile alichokusudia. Yeye hafanyi mambo yake ovyo ovyo. Kwa vile ana sababu ya kufanya yote ayafanyayo, tunaweza kusema Mungu ana kusudi katika kila jambo. Hili linadhihirishwa tangu mwanzo alipomuumba mwanamume na mwanamke wa kwanza. Tunajua kwamba aliwaambia Adamu na Hawa "Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi" (Mwa. 1:28). Kwa upande mmoja tunaweza kusema kwamba hii ilikuwa sehemu ya kusudi la Mungu kwa Adamu na Hawa. Lakini kuna jambo lingine la kutambua kuhusu hadithi hii lililo muhimu sana kwani linahusiana moja kwa moja na kusudi la Mungu kwa Adamu na Hawa.

Mwanzo 2:9 inasema,

> BWANA Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

Kisha Mungu akamwagiza Adamu akisema,

> Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika (Mwa. 2:16-17).

Fahamu kwamba Adamu alikuwa huru kabisa kula matunda ya mti wowote uliokuwa ndani ya bustani isipokuwa mmoja. Hii ina maana kwamba alikuwa huru kula matunda ya mti wowote ule katika bustani—pamoja na mti wa uzima. Kwa kweli, Mungu aliuweka mti huo katikati ya bustani ili Adamu asikose kuuona. Sababu ya Mungu kuuweka mti wa uzima mahali ambapo Adamu angeweza kuupata kwa urahisi inafichua jambo fulani kuhusu kusudi la Mungu kwa Adamu.

Mwanamume na mwanamke wa kwanza wanawakilisha wanadamu wote. Adamu na Hawa walipokula tunda la mti usiokubalika, Mungu aliwafukuza katika bustani na akaweka Makerubi na upanga wa moto kuilinda njia ya mti wa uzima (Mwa. 3:24). Kile kitendo cha Mungu kumweka malaika kuulinda mti huo kinaonyesha kwamba mti huo ulikuwa muhimu sana katika mpango na kusudi la Mungu. Walipokula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya, Mungu aliwafukuza Adamu na Hawa katika bustani mpaka wanadamu wapate nafasi nyingine ya kula tunda la mti wa uzima. Hili lilifanyika Yesu alipokuja kuleta uzima kwa watu wote (Yohana 1:4; Yohana 10:10; Rum. 5:18).

Kusudi kuu la Mungu halingefunuliwa mpaka, "ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe" (Gal. 4:4). Mpaka wakati huo kusudi la Mungu lilikuwa limefichwa. Paulo alipokea ufunuo wa siri hiyo (Efe. 3:3) aliouita "siri yake Kristo" (Efe. 3:4). Kulingana na Paulo, siri hii haikufunuliwa kwa watu katika vizazi vilivyotangulia, lakini sasa imefunuliwa na Roho. Jambo moja la siri hii ni kwamba Mataifa wangekuwa sehemu ya mwili wa Kristo (Efe. 3:6). Lakini hiki si kiini cha siri hii. Paulo aliendelea kusema kwamba aliitwa kuhubiri "utajiri wake Kristo usiopimika; na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote" (Efe. 3:8-9).

Mungu aliificha siri hiyo kwa vizazi vingi "ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho" (Efe. 3:10). Yote haya yalifanywa "kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Efe. 3:11). Kifungu hiki cha maneno, "kusudi la milele;' lina maana ya "kusudi la nyakati." Hili ndilo kusudi la makusudi yote!

Acha tuanze kuweka msingi huu pamoja. Paulo alisema,

> …tsiri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake; ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu (Kol. 1:26-27).

Je, umeiona? Kufichuliwa kwa siri, inayolingana na kusudi la nyakati, ni Kristo aliye ndani yako, tumaini la utukufu.

Yesu alisema kwamba alikuja ili tuwe na uzima, na tuwe nao tele (Yohana 10:10). Mojawapo ya vifungu maarufu sana katika Biblia kinasema, "…ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16). Uzima wa milele haumaanishi tu wingi (au urefu) wa uzima. Ni ubora wa uzima ambao Yesu anatupatia. Ni uzima wa Mungu usiokoma. Kile ambacho Mungu alitamani tangu mwanzo kupitia mti wa uzima uliokuwa katika bustani ya Edeni sasa kinawezekana kupitia Bwana Yesu Kristo. Kusudi la nyakati lilikuwa kwamba tuweze kushiriki katika uzima wa Mungu pamoja naye. Kumbuka swali lililo mwanzoni mwa sura hii, "Kusudi langu maishani ni lipi?" Sasa tutaanza kulizingatia jibu la swali hilo. Paulo alisema,

> Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo; kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo (Efe. 1:3-4).

Tazama mambo matatu katika vifungu hivi. Kwanza, Mungu "alituchagua." Pili, alituchagua "katika yeye" (Yesu). Tatu, alituchagua ndani yake "kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hii ina maana kwamba Mungu aliamua kutuchagua ndani ya Kristo kabla ya kukiumba kitu chochote. Hili ni wazo la ajabu na pia lenye nguvu.

Tazama mambo matatu katika vifungu hivi. Kwanza, Mungu "alituchagua." Pili, alituchagua "katika yeye" (Yesu). Tatu, alituchagua ndani yake "kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hii ina maana kwamba Mungu aliamua kutuchagua ndani ya Kristo kabla ya kukiumba kitu chochote. Hili ni wazo la ajabu na pia lenye nguvu.

Lakini Paulo hakukomea hapo. Aliendelea kusema kwamba "Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake" (Efe. 1:5). Hatupaswi kushikilia maneno haya "alitangulia kutuchagua." Mijadala imechacha katika historia yote ya kanisa kuhusu maana ya maneno haya. (Jambo nisiliotaka kufanya ni kunaswa katika mjadala huo.) Maneno hayo yana maana ya "kuamua jambo kabla." Mungu bado anatupa uhuru wa kuchagua na hatakiuka uwezo wetu wa kufanya hivyo. Huu ni msingi wa uhusiano. Lazima kila mara kuwe na chaguo. Lakini kweli inabaki kuwa hii, kabla ya Mungu kuumba chochote, kwanza aliamua kutuchagua sisi ndani ya Kristo! Hii ni kweli iliyo nzuri sana.

Paulo anaendelea kusema katika kifungu hiki kwamba Mungu alituchagua kuwa wana na binti zake kwa sababu ya ukarimu wake na kwa utukufu wa neema Yake. Alimalizia vifungu hivi vya kwanza vya Waefeso 1 kwa kusema kwamba Mungu alituchagua "sawasawa na kusudi la Mungu" (Efe. 1:11). Ni nini hasa maana ya kuchaguliwa sawasawa na kusudi? Muhimu kabisa, ina maana kwamba tuna sababu ya kuishi na sababu hiyo inatoka kwa Mungu. Mungu alihakikisha kwamba tuna kusudi kabla ya kuiumba dunia. Sasa wacha tufanye unganisho la mwisho ili tuone kusudi kuu la Mungu kuhusu maisha yetu ni lipi.

Warumi 8:28 hutajwa sana na Wakristo wanapohitaji kuhakikishiwa kwamba Mungu anaweza kusababisha mema kutokea katika hali ngumu. Kifungu hiki kinasema, "Nasi twajua ya kuwa


katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake". Hii ni ahadi nzuri kabisa kwamba Mungu hufanya kazi katika mambo yote kuwapatia mema. Lakini angalia vile kifungu hicho kinamalizika. Hufanyika kwa wale wampendao Mungu, kwa wale walioitwa "kwa kusudi lake." Tumeitwa kwa kusudi Lake.

Hapa ndipo wengi wetu hufanya kosa la kawaida wakati wa kusoma Biblia. Sisi huachia katikati ya dhana. Tunapenda tunachosikia na tunabaki hapo tu. Lakini tuendelee kusoma. Kifungu kinachofuata kinasema,

> Maana wale Mungu aliowajua tangu mwanzo, pia aliwachagua tangu mwanzo, wapate kufanana na mfano wa Mwanawe, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi (Rum. 8:29).

Tena kuna haya maneno "aliwachagua tangu mwanzo." Ni maneno yale tuliyoyaona katika Waefeso 1. Na sasa Paulo anatwambia kwamba Mungu aliamua kabla, kwamba tungepata kufanana na mfano wa Mwanawe.

Kabla ya dunia kuumbwa, Mungu alituchagua ndani ya Kristo. Alifanya hivyo kwa sababu alikuwa na kusudi la kutimiza. Kusudi lake lilikuwa ni sisi kushiriki katika uzima Wake. Ni kile alichotaka tangu mwanzo alipoweka mti wa uzima katikati ya bustani. Anataka tushiriki katika uzima Wake na vilevile kufanana naye. Mungu anataka tujue na tudhihirishe uzima wake kama wana na binti zake, na Yeye hutumia kila kitu kinachofanyika maishani mwetu ili kutimiza kusudi hili. Hebu nieleze kwa mifano tunavyoweza kutumia Warumi 8:28:




Tukikiona kifungu hiki hivi, "mema" yanayofanyika ni kutufananisha na mfano wa Yesu. Haimaanishi kwamba kila kitu kinafanyika kwa njia nzuri na ya furaha na tunapata tunachotaka. Ina maana kwamba mema yanayotendeka ni kule kufanana na Yesu! Hili linaifanya ahadi ya Warumi 8:28-29 kuwa yenye maana zaidi.

Mungu hana kusudi linguine linalozidi lile la Mwanawe kutukuzwa ndani ya vitu vyote na kupitia kwa vitu vyote, hasa maisha yetu! Anataka watoto Wake wafanane na Mwana Wake ili aweze kuwa na familia nzuri kabisa ya wana na binti. Mungu ana shauku kuu kuhusu kusudi hili na hatakomesha kazi ndani ya maisha yetu mpaka sote tuwe na mfano Wake na tudhihirishe maisha Yake.

Kusudi hili likiushika moyo wako, hutabaki vile ulivyo tena. Hili si wazo bora la kiteolojia. Ni ufafanuzi halisi kabisa wa shauku kuu ya Mungu na kusudi lake kuu kuhusu wanadamu. Ni kusudi moja linalosababisha kila kitu afanyacho Baba. Atamwona Mwanawe akitukuzwa ndani ya vitu vyote na kupitia vitu vyote (Kol. 1:16, 18). Na kinachofurahisha mno kuhusu jambo hili ni kwamba utashiriki katika mambo hayo yote. Kwa kweli, "Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu" (Rum. 8:19). Hii ina maana kwamba kila kitu kilichoumbwa na Mungu kinangoja kwa hamu na ghamu wewe uweze kukomaa kama mwana na binti anayedhihirisha uzima wa Kristo.

Tunaweza kukosa maana kamili ya kusudi la Mungu katika maisha yetu ikiwa tutalifahamu tu kuhusu (1) wokovu wetu; (2) hatima yetu; au (3) tunachofanya. Wokovu si kusudi la msingi la Mungu kwa wanadamu. Haina maana kusema kwamba lengo kuu la Mungu ni sisi kuokoka. Hii inachukulia kwamba Mungu alipomuumba mwanamume na mwanamke aliwaumba ili waokoke. Lakini hapo mwanzo Adamu na Hawa hawakuhitaji wokovu walipoumbwa—wokovu hauwezi kuwa kusudi la msingi la Mungu kuwaumba wanadamu. Kweli ni sehemu ya njia ya Mungu kutufikisha katika kiwango cha sisi kushiriki katika mpango wake wa mwanzo, lakini si kusudi Lake la mwanzo na la msingi. Wokovu bila shaka unahitajika kama njia ya kurekebisha mambo ili kushughulikia athari haribifu za dhambi ulimwenguni. Lakini hatupaswi kulichukulia kuwa kusudi kuu zaidi la Mungu kwa maisha yetu kwa sababu Mungu ana mpango mkubwa zaidi. Kiini cha mpango huu ni Yesu kuingia ndani ya mambo yote.

Neno kusudi, halina maana sawa na bahati. Tangu kuwa Mkristo, mara nyingi nimewasikia watu wakiongea kuhusu bahati. Wao huzingatia haja ya kuandama bahati yao ili waweze kupata yote ambayo Mungu amewatengea. Wao hujishughulisha mno na dhana hii; Mungu ana njia maalumu, ya pekee kuhusu maisha yao na kwamba mambo yote wanayopitia yanatakiwa kuwafikisha katika bahati yao. Sina hakika kabisa, bali kwangu mimi inaonekana watu wanazungumzia wazo bora kuhusu vile maisha yao yatafanana wakati fulani katika siku za usoni. Watakapofika kule watapata bahati waliyotengewa na Mungu.

"Bahati" inahusu nguvu zisizoonekana zinazoaminika kutawala kile kitakachofanyika katika siku za usoni (yaani, majaliwa). Biblia haisemi mengi kuhusu bahati. Ukitafuta neno hilo utagundua kwamba neno "bahati" linapatikana tu katika kifungu kimoja katika Biblia ya Kiingereza. Isaya 65:11-12 inasema,

> "Bali ninyi mmwachao BWANA, na kuusahau mlima wangu mtakatifu, na kuandika meza kwa ajili ya Bahati, na kuijazia Ajali vyombo vya divai iliyochanganyika; mimi nitawaandikia kuuawa kwa upanga, na ninyi nyote mtainama ili kuchinjwa."

Kurejelea neno "bahati" mara moja katika Biblia ya Kiingereza kunazungumzia wale waliomwacha Bwana kwa kukataa kumtafuta. Badala yake, wamegeuka na kujiandalia meza kwa ajili ya Bahati, na kuijazia Ajali vyombo vya divai. Hili si jambo zuri.

Neno "Bahati" katika kifungu hiki cha Isaya ni neno la Kiebrania Meni na linarejelea muungu wa kale wa kipagani wa bahati nzuri-huenda ikawa ni Pleiades uliopatikana katika unajimu wa kale. Inaaminika watu wa kale waliabudu vikundi vya nyota vinavyoambatana na majira ya mvua wakitumaini kupata bahati nzuri katika siku zao za usoni. Kwa hiyo, bahati yao ilikuwa ndani ya nyota! Wazo hili ni sawa na kile ambacho watu wengi siku hizi hukiita ishara ya zodiaki. Mungu hataki tuzitazame nyota kwa ajili ya kutafuta kusudi letu.

Mwishowe, watu wengi hufikiria kwamba kusudi lao ni kile wafanyacho. Nafikiri haya ni mawazo ambayo wengi wetu wanaweza kujihusisha nayo. Nilipokuwa mdogo, nilitaka kujua ni nini ambacho ningefanya baadaye maishani. Kwa sababu singeweza kulijibu swali hilo nikiwa katika umri wa miaka ya mwanzo ya 20, nilijitahidi kuwa na mwelekeo na mara nyingi nilijiuliza kusudi langu ni lipi. Tukisema kuhusu mtu mwingine, "Hana kusudi lolote," hatumaanishi kwamba ingekuwa heri kama angekufa. Tuna maana kwamba hawajapata "kitu fulani" cha kufanya kitakachowapa maana na motisha. Tunapofanya hivyo, huwa tunadhani kwamba kusudi ni utaalamu au kazi.

Tukilichukulia juu juu jambo hili linasikika kuwa zuri. Lakini nini hufanyika tunapobadilisha kazi, kitu ambacho watu wengi hufanya mara kadhaa katika maisha yao? Je, kusudi letu litakuwa limebadilika? Au hata vibaya zaidi, itakuaje ikiwa jambo fulani litafanyika na lituzuie kuendelea kufanya kazi yetu? Je, tutakuwa tumepoteza maana maishani? Tukielewa kwamba kusudi ni kitu tufanyacho,

tutang'ang'ana kupata kuridhika ambako Mungu anataka tupate. Yeye anajua sababu ya kutuumba. Alituumba tuwe kama Mwanawe. Kuwa kama Yesu ni kitu pekee kitakacholeta kuridhika na kutupa amani ndani ya mioyo yetu na nia zetu. Huu ndio mpango wa Mungu kutuhusu na kitu cha pekee kinachotupa kusudi la kuishi.

Jambo zuri kuhusu kusudi la Mungu ni kwamba anatenda kazi ndani ya maisha yako kila wakati (Flp. 2:13). Hauhitaji kungoja mpaka matukio fulani yatendeke ndipo uwe na kusudi. Kusudi la Mungu si mwito au utaalamu fulani. Si matokeo maalum ambapo unapata bahati yako halafu ghafla maisha yanaanza kuwa na maana maalumu kwa sababu ya hali zako.

Haya yote hayako mbali sana na kweli kuhusu kusudi la Mungu. Analitenda ndani ya maisha yako kupitia hali zako zote, nzuri na ngumu. Una haki na nafasi ya kufungamana na kusudi lake kila siku.

*Kusudi la Mungu ni kwako wewe kuupata uzima Wake na kuwa kama Yesu kila siku.*

Jambo zuri kuhusu kusudi la Mungu ni kwamba halibadiliki kamwe. Si kitu unachotakiwa kung'ang'ana ili ukijue. Ni rahisi—bali la maana sana. Lengo lake ni kwamba umjue zaidi na anapoishi maisha yake kupitia kwako, uweze kupata nguvu zake za mgeuzo ndani ya maisha yako kila siku.

Unapoelewa dhana hii katika nia na moyo wako, kila kitu kitabadilika. Utazingatia jinsi Mungu anatenda kazi ndani yako na kupitia kwako katika hali zote ndani ya maisha yako ili kutimiza kusudi Lake la wewe kuwa kama Yesu. Kila mara mimi huwaambia watu, unapopata ufunuo huu na kuanza kuishi maisha kulingana na kusudi la Mungu, kuna swali moja tu lililo muhimu? Mimi hujiuliza swali hili karibu kila siku, "Ni nini ambacho Mungu anataka kufanya maishani mwangu kupitia hali hii ili kunisaidia kuwa kama Yesu?"

Unapojiuliza swali hili, utaacha kuzingatia hali yako au kile unachofanya maishani na kuanza kufungamana na malengo ya Mungu. Naweza kukiri kwamba hili ni gumu kufanya. Si rahisi kwa sababu Mungu atafunua sehemu za maisha yako zisizofanana na Yesu!

Nakumbuka wakati fulani ambao mimi na Stephanie tulikuwa na matatizo fulani katika uhusiano wetu. Nilikuwa nimefadhaika sana na nilikuwa namlilia Mungu. Nilimuuliza kwa nini tulikuwa tunang'ang'ana sana katika ndoa yetu. (Fahamu nilikuwa nauliza swali lisilo sahihi. Lakini Mungu ni mvumilivu na mwenye huruma na atasaidia kutuongoza kufika mahali panapofaa.) Naamini nilimsikia Mungu akininenea wazi kabisa kwa hali ambayo sikuwa nimewahi kumsikia hapo awali. Aliniuliza swali hili; "Cliff, je, ungependa kujua ni kwa nini unaendelea kung'ang'ana katika ndoa yako?" Nikasema, "Ndiyo!" Kisha akaniambia, "Tatizo ni kwamba haufanani nami"

Jibu hilo lilinivunja kabisa! Nilikuwa nimekaa ndani ya Ukristo kwa zaidi ya miaka ishirini. Nilikuwa nafanya huduma wakati wote na nilikuwa nimefunza watu kuhusu mambo ya Mungu. Nilkuwa nimetumia miaka mingi kukua na kukomaa katika uhusiano wangu na Mungu. Na sasa Bwana anasema kwamba sifanani naye. Hiyo ndiyo siku ambayo Mungu alianza kunifunza ninachoshiriki nawe katika sura hii. Alinionyesha kwamba Yesu ni mume aliye kamili kwa mkewe (kanisa) na kwamba kama ningefuata mfano wake zaidi, angekuwa mume wa Stephanie kupitia kwangu! Nilipata ufunuo huo, nikajinyenyekeza, nikatubu, na nikaanza kumruhusu Yesu ampende Stephanie kupitia kwangu. Hapo ndipo safari hii ilianza kwangu mimi na hapo ndipo Mungu alianza kuirejesha ndoa yangu.

Kusudi lako maishani ni kumpata Yesu kwa njia inayoyageuza maisha. Umeitwa ili wewe mwenyewe ushiriki katika uzima wa Mungu na uweze kupata mpango wa Mungu wa kukufanya uwe kama Yesu. Ni Mungu pekee ndiye anaweza kubadilisha moyo, mwenendo, mtazamo, na tabia yako. Hii ni ahadi ya injili. Umeitwa kulingana na kusudi Lake na kusudi hili ndiyo sababu kuu ya wewe kuishi. Naamini hii ndiyo shauku iliyo ndani ya moyo wa kila mtu kwa kuwa ndiyo sababu ya sisi kuumbwa. Sote tunataka kujua kwamba tunaweza kugeuzwa na kuridhika. Hili linapatikana tu ndani ya Yesu. Yeye

ndiye nguvu za Mungu za kuyageuza maisha na anaishi ndani yako kukufanya ufuate mfano wake. Hili ndilo kusudi la Mungu kwako wewe na ni kweli muhimu sana ya maisha ya Kikristo.

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Kila kitu afanyacho Mungu ndani ya maisha yako ni kwa mujibu wa kusudi Lake la milele aliloamua kabla ya kuuweka msingi wa dunia. Kusudi hili la nyakati zote ni kwamba upate uzima wake kupitia kwa Yesu na uwe kama Yeye.

**Tamko la imani:** Nimeitwa kwa mujibu wa kusudi la Mungu na anatumia kila hali maishani mwangu kunifanya nifuata mfano wa Kristo.

### *Kuenenda Katika Kweli*

Anza kuiandaa nia yako kuukubali ukweli huu kwamba Mungu ana kusudi la ajabu kwako wewe. Kila siku tambua kwamba Mungu anatumia kila hali, changamoto, na uhusiano kutenda kusudi Lake ndani ya maisha yako. Atatumia kila nafasi kukufanya uwe kama Yesu. Anza kumuuliza Bwana, “Je, ungependa kutumia vipi kile ninachopitia wakati huu kunifanya niwe kama Yesu?” Mwambie Bwana akupe hekima, ufahamu, na uzitambue hali zilizo ndani ya maisha yako anazozishughulikia kila siku. Kubali kweli hii kwamba uzima Wake uko ndani yako, unakugeuza, na kwamba unataka kujua na kudhihirisha uzima Wake kwa wengine kwa utukufu Wake.

# 2

# MTAZAMO

*Tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.*
*~ 2 Wakorintho 4:18*

Kuwa Mkristo kuna maana zaidi ya kusamehewa dhambi zako na kupokea "tikiti ya kwenda mbinguni" siku ambayo tutakufa. Ingawa hili ni jambo zuri, halitupatii maana kamili kuhusu yote ambayo Mungu amekufanyia kupitia kwa Yesu Kristo.

Kweli ni kwamba unapogeuka kuwa Mkristo unapitia mabadiliko makubwa katika maisha yako. Unapokomaa na kugundua maana ya kuwa Mkristo, unapata kuelewa jinsi ilivyo muhimu kuyaona mambo kwa mtazamo wa Mungu. Kabla ya wewe kumwamini Yesu, "mungu wa dunia hii alipofusha akili za wasioamini" (2 Kor. 4:4) ili wasione vizuri. Uwezo huu wa kuona huleta mtazamo mpya kabisa. Mungu hataki tubaki katika mienendo yetu ya kale ya kuyatazama mambo. Kuna mengi zaidi anayotaka tuyaone na hilo linawezekana tunapofahamu kile alichofanya ndani yetu kutupa mtazamo Wake.

Kadri niwezavyo kukumbuka, napenda sana kusafiri hewani kwa ndege. Kwenda juu angani na kutazama chini hukupa mtazamo tofauti sana kuhusu vitu. Mimi hujaribu kuwaza vile ilivyo kuyaona mambo vile Mungu anavyoyaona. Kuwa mahali pa Mungu pa kutazamia jambo fulani ni muhimu kabisa. La kusikitisha, hiki ni kitu ambacho wengi wetu hukosa kukifikiria kila siku. Unapoyaona mambo kwa njia tofauti na kuyaona kwa mtazamo wa milele wa kweli ya kiroho, hilo huleta tofauti kubwa sana katika maisha yako.

Katika mazungumzo yajulikanayo sana kati ya Yesu na Nikodemo katika Yohana 3, Yesu alimwambia, "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." (Yohana 3:3). Kwa zaidi ya miaka elfu mbili ya historia ya Ukristo, wazo la "kuzaliwa mara ya pili" huenda ikawa ndiyo njia inayojulikana sana ya kurejelea kile kinachofanyika mtu anapomwamini Yesu. La

kusikitisha ni kwamba, Wakristo wengi hawaelewi kabisa kina cha maana ya kuzaliwa mara ya pili. Sababu kuu ya jambo hili ni kwamba sawa na kweli nyingi inayohusu maisha ya Kikristo-kuzaliwa mara ya pili hunenea kweli ya kiroho isiyoweza kufahamika kwa kutumia nia ya kawaida. Lakini kutoweza kwetu kulifahamu jambo hili kupitia hisi za kawaida hakulifanyi likose kuwa kweli. Kweli ya kiroho ya kuzaliwa mara ya pili ni halisi kama kitu chochote unachokipata katika eneo la hapa duniani.

Maneno haya "kuzaliwa mara ya pili" yana maana kwamba kweli kuna maisha mapya ambayo hayakuweko kabla ya wewe kuwa Mkristo. Usisikie vibaya ikiwa huelewi mambo haya. Tukio la kusafiri ndani ya tundu la sungura linaweza kumchanganya mtu wakati mwingine. Hata Nikodemo alikuwa na tatizo la kuelewa alichokuwa akisema Yesu. Alimjibu Yesu vile wengine wetu wangetaka kujibu, je, unaweza kuingia tena tumboni mwa mama yako?! Kwa vile Nikodemo aliuliza swali hili ni thibitisho kwamba hakuwa anafikiria kiroho, bali kwa hali ya kidunia, ya kawaida.

Yesu anataka uyaone mambo anavyoyaona Yeye na sio unavyoyaona kwa hisi zako za kawaida. Ili jambo hili litendeke, lazima kuwe na kuzaliwa upya, Kuzaliwa upya kwa Roho hukupa uwezo wa kuuona ufalme wa Mungu. Kuzaliwa upya hufungua njia mpya kabisa ya kuyatazama mambo yote yanayotendeka katika maisha yako.

Kweli ni kwamba Mungu amesababisha kuzaliwa kiroho kufanyike ndani yako. Hii ina maana kwamba una uzima ndani ya Roho ambao ni mpya kabisa na utokao kwa Mungu Mwenyewe. Yesu alisema, "Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho" (Yohana 3:6), na Yohana alisema kwamba wanaoliamini jina Lake ni "waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu" (Yohana 1:13).

Maana ya jambo hili ni kuu sana. Sasa umefanywa kuwa hai na Roho, na roho yako imeungwa na Bwana na kuwa moja (1 Kor. 6:17). Una maisha mapya ya kiroho na lazima ujifunze kuubadili mtazamo wako ili uwe wa uzima huu mpya ulio ndani yako ikiwa utaishi kwa ukamilifu ambao Mungu anakutakia. Ikiwa hutaruhusu badiliko hili la mtazamo katika maisha yako, utabaki tu katika fikira za kawaida za dunia, na utayakosa mengi ambayo Mungu anataka uyaone na kuyapitia.

Katika 2 Wakorintho 5:17 Paulo anatwambia, "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya." Kifungu hiki pia kinazungumza kuhusu kuzaliwa upya. Kuzaliwa upya kunajidhihirisha katika uhalisi wa kiumbe kipya.

"Mtu mpya" ni njia aipendayo sana Paulo kurejelea uhalisi huu katika maisha ya muumini. Tusipokuwa waangalifu tutaingia katika mtego wa kufikiria kwamba Paulo ni mwenye taasubi za kiume na anazungumza tu kuhusu "mtu mpya" na sio "mwanamke mpya pia". Niamini ninaposema kwamba watu wengi sana wamekuwa na mawazo haya na wamesababisha madhara makuu katika mwili wa Kristo.

Katika lugha ya asili ya Agano Jipya, kuna maneno mawili yanayotafsiriwa "mtu." La kwanza ni neno la Kigriki aner. Neno hili lina maana ya "mwanamume" au "mtu wa kiume." Neno la pili ni neno la Kigiriki anthrópos. Neno hili lina maana ya "mwanadamu" au "wanadamu" kwa jumla; mwanamume na mwanamke. Paulo alitumia neno Anthrópos alipozungumza kuhusu "mtu mpya" (Efe. 4:24; Rum. 6:6; Kol. 3:9). Kwa kulitumia neno hili, Paulo alikuwa akisema kwamba sisi ni sehemu ya jamii mpya ya wanadamu! Hii ni kweli ya ajabu na ambayo inatuhijaji tugeuze fikira zetu. Pia ni kweli isiyohusiana kwa vyovyote vile na mwanaume na mwanamke (Gal. 3:28). Alipozungumza kuhusu "mtu mpya;" Paulo hakuwa akirejelea wanaume pekee, bali alirejelea wote walio sehemu ya jamii hii mpya katika Kristo, wanaume na wanawake.

Unapokuwa Mkristo, papo hapo unakuwa sehemu ya jamii hii mpya katika Yesu. Si kitu unachojaribu kupata baada ya kuwa Mkristo. Ni kitu ambacho Mungu anafanya ndani yako na kinafanyika kwa

njia ya imani. Mara tu unapofanya badiliko hili katika imani yako, basi utagundua jinsi linavyoaathiri maisha yako kwa njia halisi.

Paulo alisema,

> …mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani (anthrópos), unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya (anthrópos), ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli (anthrópos) (Efe.4:22-24).

Hii ni mojawapo ya vifungu nivipendavyo kuhusu mtu mpya. Nimekitumia kifungu hiki kama kifaa cha nguvu sana maishani mwangu kunisaidia kuingia katika kweli inayobadili maisha. Paulo alitumia sitiari rahisi katika vifungu hivi ya kuvaa na kuvua. Ni kitu cha kawaida sana ambacho sote tunaweza kuelewa kwa sababu tunakifanya kila siku kwa hali ya kawaida. Sisi huvua nguo na kuvaa nguo. Ili kutusaidia kuelewa kweli hii ya kiroho, Paulo alikuwa akisema kwamba kwa njia halisi/ya kiroho tunahitaji kuvua mtu wa zamani na kuvaa mtu mpya. Mtu mpya tayari ni halisi. Ndio maana Paulo alisema mtu mpya "ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli" (Efe. 4:24). Tunatakiwa tu kudhihirisha imani yetu kila siku na kumvaa. Mimi hufanya hivi wakati nina kipindi changu binafsi cha kumwabudu Bwana. Mimi hujiona nikivua mtu wa zamani na kuvaa mtu mpya. Ni muhimu sana tufanye kitu fulani halisi kila siku kinachotusaidia kuunganishwa na kweli hii.

Unapoamini kwamba wewe ni mwanadamu mpya, utaanza kufanya mabadiliko halisi katika maisha yako ya kila siku. Niseme hivi, lazima uamini kwamba wewe ni mtu mpya na kila mara uitumie imani yako kuelekea kwa kweli hii muhimu sana. Unapotumia imani yako na kuamini kweli hii, ufahamu wako wa kweli hii utaongezeka ndani yako na kuingiliana kwako binafsi na kweli hii kutaanza kukuweka huru.

Hivi ndivyo Mungu hufanya kazi katika maisha yako kuleta mgeuzo. Yeye hukuelekeza kwa kweli hiyo kisha akakwamba uiamini. Unapodhihirisha imani yako katika kweli hiyo, Mungu huanza kukifanya kile kitu unachoamini katika maisha yako. Kadri unavyozidi kuwa na imani katika kweli hiyo ndivyo kweli hiyo inavyozidi kuthibitika! Unapoelewa nguvu za imani yako kwa njia hii, kutakuwa na mgeuzo katika maisha yako.

Katika utaratibu huu unatakiwa kukumbuka kwamba imani yako haiwezi kuwa kubwa kuliko kweli hiyo. Kweli hiyo ina nguvu za kukuweka huru na imani yako ndio ufunguo wa kuzifikia nguvu hizo. Injili ya kweli ya Agano Jipya lazima iwe na ufahamu huu wa imani katika kiini chake. Imani ni kiini cha matukio yako ya Kikristo na bila imani huwezi kuipata kweli inayodhihirika maishani mwako na inayoleta mgeuzo.

Mara tu unapoanza kufahamu wewe ni nani kama kiumbe kipya, utabadilisha fikira zako na kuanza kuyaona mambo kwa hali tofauti. Ni kana kwamba umevaa miwani yaliyo sahihi na kisha kila kitu kikaanza kuonekana vizuri.

Badiliko tulilopata ndani ya nafsi yetu litaathiri maisha yetu ya kila siku kwa kiwango halisi. Namna kuu ya kufanyika kwa jambo hili ni wakati tutaanza kuziona hali zetu kwa njia tofauti. Sote tuna mwelekeo wa asili wa kuona kwa macho yetu, kwa njia ya kawaida na pia kwa ishara, kinachoendelea mahali tulipo. Tusipobadilisha mtazamo wetu, hatutapiga hatua muhimu katika ukuaji wetu wa kiroho. Niligusia jambo hili katika sura inayotangulia hii nilipoeleza vile Mungu hutumia hali zetu kutufanya tufanane na Yesu.

Paulo alisema,

> …tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya

> muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele (2 Kor. 4:18).

Hii ni mojawapo ya vile vifungu vinavyoonekana kuwa vya ajabu mwanzoni. Huenda ukauliza, "Ninawezaje kuacha kuviangalia vitu vinavyoonekana na kuanza kuviangalia vitu visivyoonekana?" Hili ni swali la kawaida kuuliza na vilevile kuna jibu zuri.

Jibu ni kwamba, lazima ujifunze namna ya kuishi kulingana na asili yako mpya kama mtu wa kiroho. Lazima ufanya uamuzi muhimu sana—na wakati mwingine uamuzi mgumu sana—wa kuacha kuviangalia vitu jinsi unavyoviona tu katika ulimwengu wa kawaida. Kuona kwako kwa kawaida ni hisi ya kufaa na ya lazima. Hata hivyo, hakukunuiwa kutumiwa kama njia ya wewe kuona na kuvifahamu vitu kutokana na mtazamo wa Mungu.

Kuongeza kwa macho yako, wewe pia hutumia akili na hisia yako kukadiria hali zako. Lakini Mungu hataki utumie kuona kwako kwa kawaida, akili yako, au hisia zako kuyaangalia mambo. Kinyume na hayo, Mungu amefungua macho ya moyo wako (Matendo 26:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18), na sasa unaweza kuona kwa njia tofauti kabisa. Unaweza sasa kuona na kutazama mambo kwa mtazamo wa milele. Hii haimaanishi kwamba upuuze unachoona na unachohisi. Inamaanisha ujifunze kwamba kuna njia bora zaidi.

Kuna kweli hapa ambayo hutakiwi kuikosa. Kweli hiyo ni kwamba vitu unavyoweza kuviona kwa macho yako ya kawaida ni vya muda tu na vitu unavyoona kwa macho yako ya kiroho ni vya milele. Hii ina maana yenye kina kwako wewe kama muumini. Maadamu unajishughulisha kuvitazama vitu kwa macho yako ya kawaida, unatazama tu vitu vya dunia ambavyo vitapita. Mtazamo wa muda hauwezi kamwe kukupa hadithi nzima. Unahitaji kujifunza kutazama kwa macho yako ya kiroho ili uweze kuona vitu vya kiroho. Vitu vya kiroho vina kweli na vinakusaidia kuishi kwa kuufuata mtazamo wa Mungu.

Hebu tuzingatie kweli hii kwa njia halisi. Hali zako wakati wowote ule ni halisi. Hutakiwi kuzipuuza na kujifanya kwamba haziko. Mungu hataki uenende katika hali ya kuyakana mambo. Hata hivyo, ukitazama tu hali zinazokuzingira, ufanye uamuzi wako, na uamue mambo kwa kutegemea kile unachoona kwa hali ya kawaida, nakuhakikishia kwamba hali hizo zitabadilika kila mara na uamuzi wako utategemea maarifa yaliyo na mipaka, na yasiyo kamili. Ndiyo maana unatakiwa kuwa na mtazamo mzuri na uliokomaa kuhusu yale unayoyaona yakifanyika karibu nawe.

Unapoimarisha uwezo wa kuvitazama vitu visivyoonekana, mtazamo wako huanza kubadilika. Vitu visivyoonekana ni vitu vinavyohusiana na Mungu na pamoja na mtazamo Wake wa milele. Tunajua kwamba mtazamo wa Mungu ni kamili kabisa kwa sababu yeye huviona vitu vyote kutoka mwanzo hadi mwanzo.

Paulo alitwambia pia,

> Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi (Kol. 3:1-2).

Hili ni himizo lingine kwetu sisi kubadilisha mtazamo wetu. Unaweza kuchagua mahali ambapo utaiweka nia yako. Unapofanya chaguo hilo na kubadilisha lengo lako kwa mambo yaliyo juu, utagundua kwamba uzima wako upo mahali ambapo Kristo ameketi!

Hii ilikuwa kweli ya kina kwa mke wangu na mimi kupitia maisha ya mtoto wetu wa kiume, Wesley aliyekuwa na ulemavu. Watu wengine watakaosoma kitabu hiki wanamjua Wesley. Yeye ni kijana mzuri ambaye huwafurahisha watu popote alipo. Lakini Wesley ana ugonjwa wa jenetiki unaojulikana kama X dhaifu (Fragile X) unaopunguza uwezo wake wa utambuzi wa mambo. Katika maisha ya hapa duniani, pasipo muujiza, hataweza kamwe kusoma, na kufikiria kama watu wengine ambao akili zao zinafanya kazi kikamilifu. Mwanzo wa maisha yake Mungu alituonyesha kweli kuhusu Wesley

ili kutuhimiza kama wazazi wake. Kweli ni kwamba Mungu anampenda Wesley jinsi alivyo na kile tunachoona katika maisha ya Wesley ni cha muda tu. Ni hali iliyo kweli katika maisha haya tu. Wesley atakuwa kamili, asiye na ulemavu, daima katika mbingu ya milele. Badiliko hili katika mtazamo limetupa amani na tumani kuu tunapoenenda katika safari hii na Wesley. Mtazamo wetu umebadilika, na tunapokea baraka ya kumwona Wesley— na thamani yake ya ajabu—jinsi anavyomwona Mungu.

Mojawapo ya hadithi nizipendazo sana katika Agano la Kale zinazoonyesha kweli hii wazi kabisa ni hadithi ya Elisha na mtumishi wake katika 2 Wafalme 6. Mtumishi wa Elisha aliondoka asubuhi na mapema kwenda nje na akaliona jeshi la watu pamoja na farasi na magari, limeuzingira mjia ule. Alijaa woga na akarudi kwa Elisha kumpasha habari ya yale aliyoyaona. Elisha alikuwa na jibu zuri sana:

> "Usiogope; maana walio pamoja nasi ni wengi kuliko wale walio pamoja nao. Elisha akaomba, akasema, Ee BWANA, nakusihi, mfumbue macho yake, apate kuona. BWANA akamfumbua macho yule mtumishi; naye akaona; na tazama, kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyomzunguka Elisha pande zote" (2 Wafalme 6:16-17).

Huu ni mfano bora zaidi wa tofauti iliyoko baina ya kutazama kwa macho ya kawaida vitu vinavyoonekana na kutazama kwa macho ya kiroho vitu visivyoonekana. Vilevile, Mungu ameyafungua macaho yako ili uweze kuona vitu visivyoonekana. Hii inakuruhusu ushiriki katika mambo ya milele ya Mungu. Unatakiwa kuubadilisha mtazamo wako na uanza kuvitazama vitu jinsi Mungu anataka uvitazame.

Hii haimaanishi kwamba kila mara utakuwa na hali ya kiroho, iliyo dhahiri kama ya mtumishi wa Elisha. Hilii huanza unapochukua hatua kwa hatua kuubadilisha ufahamu wako na kubadilisha lengo lako. Bwana atakusaidia kuziona hali zako kwa njia tofauti. Baada ya muda utajua vizuri utaratibu huu na utaweza kufahamu tofauti iliyoko baina ya kuyaona mambo kwa mtazamo wa kiroho, wa milele wa Mungu na mtazamo wako wa kawaida ulio wa muda.

Tuna nia ya Kristo (1 Kor. 2:16). Kuwa na nia ya Kristo hutuwezesha kujua yote ambayo Mungu ametupatia. Mambo haya hufunuliwa kwetu na Roho. Kuwa na nia ya Kristo pia kuna maana kwamba tunaweza kuona na kufahamu mambo jinsi anavyoyafahamu Mungu. Tunapokua na kujifunza namna ya kuishi katika kweli hii, tunaanza kuyatazama mambo kwa njia tofauti.

Alama ya kweli ya kukomaa kiroho ni kuyaona mambo kwa mtazamo wa Mungu. Paulo aliwaambia waumini wa Korintho kwamba hangeweza kusema nao kama "watu wa kiroho" kwa sababu wao walikuwa "watu wa mwilini" katika mawazo yao (1 Kor. 3:1-4). Walikuwa wakifanya uamuzi kati ya Petro, Paulo, Apolo, ni nani waliyempenda zaidi. Huu ni mfano halisi wa vile tunaweza kuyatazama mambo kwa njia isiyo sahihi kwa sababu ya fikira zisizo sahihi. Paulo aliwakosoa kwa kuwaambia kuwa yeye, Petro, au Apolo hawakuwa chochote, bali Kristo ndiye muhimu zaidi. Wao walikuwa watumishi tu waliowasaidia Wakorintho kumwamini Kristo (1 Kor. 3:5). Ilibidi mtu wa kiroho kama Paulo awasaidie waumini wa Korintho kuacha kuyatazama mambo kwa macho ya kawaida na kuanza kuyatazama kwa mtazamo wa kiroho.

Kuwa na nia ya Mungu katika maisha ni sehemu muhimu sana katika ukomavu wako wa kiroho. Mungu anafahamu kabisa kwamba uko katika dunia hii na kwamba huwezi kukwepa kuyaishi maisha katika kiwango cha kawaida, cha kimwili. Hata hivyo, anataka ujue kwamba kuna uhalisi ulioko sasa nje ya ulimwengu huu wa kawaida. "Kuzaliwa kwa Roho" (Yohana 3:5-6) na kuwa ndani ya Kristo hubadilisha kila kitu. Kufanya hivyo hukuelekeza kwa mtazamo mpya unaoingia ndani ya kila sehemu ya maisha yako.

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Maisha yako yamebadilishwa kabisa kwa ajili ya imani yako ndani ya Kristo. Wewe ni kiumbe kipya na Mungu anataka mtazamo wako maishani ujengwe kwa kujua kweli wewe ni nani katika Kristo.

**Tamko la Imani:** Mimi ni kiumbe kipya, nina nia ya Kristo, na ninaweza kutambua na kufahamu mambo kutokana na mtazamo wa Mungu.

### *Kuenenda Katika Kweli*

Kila siku inapoanza, fanya mazoezi ya hatua ya imani ya kumvaa mtu mpya. Fanya uamuzi leo kwamba hutazingatia tu yanayoendelea karibu nawe katika hali ya kawaida. Anza kuamini kwamba Mungu anajishughulisha kufanya mambo mengi usiyoweza kuyaona kwa hisi zako za kawaida. Kwa imani, muombe Mungu akupe mtazamo Wake. Amini kwamba una nia ya Kristo na unaweza kuyafahamu mambo kwa mtazamo wa Mungu. Badilisha mtazamo wako na uuache uathiri jinsi unavyoishi kila siku.

# 3

# NEEMA

*Kutokana na ukamilifu wake, sisi sote tumepokea neema juu ya neema.*
*~ Yohana 1:16 (NEN)*

*Kwa maana ikiwa kutokana na kosa la mtu mmoja, mauti ilitawala kupitia huyo mtu mmoja, zaidi sana wale wanaopokea wingi wa neema ya Mungu na karama yake ya kuhesabiwa haki, watatawala katika uzima kwa njia ya huyo mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo.*
*~ Warumi 5:17 (NEN)*

Kupeana zawadi ni mazoea ya kawaida katika tamaduni nyingi kote ulimwenguni. Iwe ni siku ya kuzaliwa, siku ya ukumbusho, Krismasi, au sherehe nyingine maalum, sisi hupeana zawadi kuonyesha upendo wetu kwa wengine. Zawadi zinaweza kuwa na thamani tofauti, lakini jambo muhimu sana kuhusu zawadi yoyote ni kile ambacho anayepeana zawadi hiyo angependa kuwasilisha kupitia zawadi hiyo. Kila mtu hufurahia kupokea zawadi inayomfanya ahisi kwamba anathaminiwa sana. Mungu huweka thamani kuu zaidi kwetu kupitia kipawa anachotupatia – kipawa cha uzima kupitia Mwanawe wa pekee.

Paulo alisema,

> Lakini karama ile haikuwa kama lile kosa; kwa maana ikiwa kwa kukosa kwake yule mmoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mungu, na kipawa kilicho katika neema yake mwanadamu mmoja Yesu Kristo kimezidi kwa ajili ya wale wengi (Rum. 5:15 SRUV).

Neema ya Mungu ndiyo njia ambayo kwayo Mungu anatupatia kipawa kikuu zaidi ya vyote vilivyowahi kutolewa. Katika sura hii utagundua maana ya kweli ya neema na athari kuu ambayo neema hiyo inayo juu ya maisha yako..

Najua nimeyasema haya zaidi, lakini yanastahili kusemwa tena na tena. Shauku kuu zaidi ya Mungu ni kwamba wewe ushiriki katika uzima Wake pamoja naye. Baba, Mwana, na Roho anataka kushiriki nawe kikamilifu na kwa uhuru. Petro alisema kwamba Mungu amekupa "ahadi kubwa mno, za thamani,

ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu" (2 Petro 1:4). Mungu anataka ushiriki-ushiriki kabisa-katika asili Yake! Hili hutendeka unapopokea uzima Wake anaokupa kwa neema.

Katika lugha ya kiingereza kuna akronimi hii: GRACE (NEEMA)

Katika lugha ya Kiingereza inaleta maana hii: Utajiri (au Ukombozi) wa Mungu kwa Gharama ya Kristo.

Kulingana na ufafanuzi huu wa neema, Yesu alilipa gharama kuu ili tuweze kupokea kitu cha thamani sana kutoka kwa Mungu. Kwa wengi wetu huu ndio ufahamu tulio nao kuhusu neema. Ni kweli kwamba Yesu alilipa gharama kubwa sana ili tuweze kupata wokovu. Lakini kuna mengi zaidi kuhusu neema kuliko hili. .

Kabla ya kuingia katika mazungumzo kuhusu neema ndani ya maisha ya muumini, ningependa kuweka msingi wa Biblia kuhusu kweli hii muhimi sana. Jambo muhimu sana kulijua ni kwamba neema hurejelea hasa shughuli ya Mungu ndani ya Yesu Kristo na kupitia kwake katika Agano Jipya.. Kwa sababu hii, kutokana na mtazamo wa Biblia/kiroho, hatustahili kuzungumza kuhusu neema kwa muktadha wa Agano la Kale. Najua kwamba hili litaonekana kuwa geni mara ya kwanza, lakini naamini ni wazo muhimu kusema tunapotaka kufahamu maana ya kweli ya neema.

Lugha ya Kiebrania na utamadauni wa Agano la Kale haikuwa na neno au dhana ya neema. Neno linalokaribia sana neema katika lugha ya Kiebrania ni neno "chen" lenye maana ya "kumpa mtu kibali au kumwonyesha mtu rehema." Aina mbalimbali za neno hili zinajitokeza karibu mara 200 katika Agano la Kale. Mifano mingine ya neno hili ni wakati Lutu alipata kibali machoni pa watu waliotumwa na Bwana kule Sodoma (Mwa. 19:19); Yakobo alipata kibali machoni pa Esau (Mwa. 32:5); Yusufu alipata kibali machoni pa Potifa (Mwa. 39:4); Ruthu alipata kibali machoni pa Boazi (Ruthu 2:10); na Daudi akapata kibali machoni pa Yonathani (1 Sam. 20:3). Katika mifano hii yote, watu walipata kibali machoni pa watu wengine.

Kuna mifano michache katika Agano la Kale ya watu kupata kibali machoni pa Mungu. Kwa mfano, Nuhu (Mwa. 6:8) na Musa (Kut. 33:12-13) walipata kibali machoni pa Mungu. Gideoni (Waamuzi 6:17) na Samweli (1 Sam. 2:26) pia akapata kibali machoni pa Bwana. Hii ndiyo njia bora zaidi ya kulitafsiri neno la Kiebrania "chen". Utata kuhusu neema katika Agano la Kale unatokea kwa sababu tafsiri nyingine za Biblia za Kiingereza zinatafsiri neno la Kiebrania "chen" kama "neema." Watafsiri waliamua tu kutumia "neema" badala ya "kibali" au "rehema" kutegemea muktadha wa kifungu hicho na ufahamu wao wenyewe kuhusu neema. Lakini huku si kusema kwamba Mungu alitoa neema katika Agano la Kale.

Mungu kuwapa watu neema Yake ni jambo la Agano Jipya. Hii ndiyo maana Yohana alianza injili yake kwa kutwambia mambo kadhaa muhimu kuhusu neema na vile inahusiana na Yesu. Alisema kwamba Yesu alijaa "neema na kweli" (Yohana 1:14); kwamba "kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema." (Yohana 1:16); na kwamba "Kwa kuwa sheria ilitolewa kwa mkono wa Mose, lakini neema na kweli imekuja kupitia Yesu Kristo" (Yohana 1:17 NEN). Paulo alithibitisha hili aliposema, "...Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa" (Tito 2:11).

Neema ilifanyika kweli wakati Yesu Kristo alitokea na ni kupitia kwake tu ndio Mungu anatupa neema Yake. Chukua dakika kadhaa usome maandiko yafuatayo kwa makini. Nimeongeza mkazo katika vifungu hivi kusisitizia kweli kuhusu neema.

- Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo (Yohana 1:17).
- "Bali twaamini kwamba tutaokoka kwa neema ya Bwana Yesu vile vile kama wao" (Matendo 15:11).

- Namshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu, kwa sababu ya neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu (1 Kor. 1:4).
- Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa (Efe. 1:5-6).
- Ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele (2 Tim. 1:9).
- Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina (Ufu. 22:21).

Neema ni ya Yesu Kristo, inatoka kwake, na inatolewa kupitia kwake! Ni vyema kukumbuka kila mara kwamba Yesu Kristo ndiye njia ya msingi na ya pekee ambayo Mungu anahusiana na mwanadamu (Ebr. 1:1-2). Wakati Yesu alikuja, kila kitu kilibadilika. Kuiona tofauti hii ni ufunguo unaofungua ufahamu wetu kuhusu neema.

Sasa ni wakati mzuri wa kuona tofauti iliyoko baina ya Agano la Kale na Agano Jipya. Nitafanya hivi katika kitabu hiki chote kwa sababu tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya inaathiri vile tunayafahamu maisha ya Kikristo. Ni wazi kutokana na waandishi wa Agano Jipya kwamba kulikuwa na badiliko kuu kwa vile uhusiano wa mwanadamu kwa Mungu unafanya kazi kutokana na Agano Jipya lililopatanishwa na Yesu Kristo (Ebr. 8:6; 9:15; 12:24). (Tutaangalia kinagaubaga maana ya kuwa katika uhusiano sahihi na Mungu katika Sura ya 5 kuhusu Haki.)

Paul alisema,

> …hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki (Gal. 2:16).

Tofauti hiyo ni dhahiri. Chini ya Agano la Kale "kazi ya Sheria" iliainisha uhusiano wa mwanadamu na Mungu. Chini ya Agano Jipya "imani ndani ya Yesu Kristo" inaainisha uhusiano wetu na Mungu. "Kazi" na "imani" ni mambo yenye uhusiano katika maagano hayo mawili (Rum. 3:27- 28; Gal. 2:16; 3:2).

Sababu kuu ya Mungu kuanzisha Agano Jipya katika Yesu Kristo kwa msingi wa imani ni kwa sababu tayari alikuwa amefanya ahadi kwa Abrahamu na kwa uzao wake kwa msingi wa imani ya Abrahamu. Hii ni mojawapo ya kweli muhimu kuhusu vile Mungu anataka kuhusiana nasi. Paulo alisema,

Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo. Nisemalo ni hili; agano lililothibitishwa kwanza na Mungu, torati iliyotokea miaka mia nne na thelathini baadaye hailitangui, hata kuibatilisha ile ahadi (Gal. 3:16-17).

Mungu alikuwa ameshafanya ahadi kwa Abrahamu kwa msingi wa imani yake na ahadi hiyo ilifanywa kwa Yesu! Ahadi ilikuwa kwamba yeyote ambaye angekuwa na imani kwa Yesu, sawa na vile Abrahamu alikuwa na imani kwa Mungu, angefanyika kuwa mwenye haki. Hii ndiyo maana ya kuhesabiwa haki. Na ndio maana maandiko yanafunza kwamba tunahesabiwa haki kwa kuwa na imani ndani ya Kristo Yesu na sio kwa matendo ya sheria (Rum. 3:20; Gal. 2:16; 3:11). Hili lingefanyika tu kwa imani ndani ya Kristo (Rum. 3:26).

Jambo muhimu ni kwamba shauku la Mungu kila mara limekuwa sisi kuhusiana naye kwa imani. Sura muhimu kuhusu imani katika Waebrania 11 inasisitiza wazi ukweli huu. Tangu mwanzo ni imani

iliyotofautisha dhabihu ya Abeli na ile ya Kaini. Na mwandishi wa Waebrania alikariri mifano mingi ya imani katika maisha ya watu wengine katika Agano la Kale. Kweli ni kwamba Mungu hajawahi kamwe kututaka tuhusiane naye kupitia juhudi zetu wenyewe (yaani, matendo). Anajua kwamba yeyote anayejaribu kufanya hivyo hatafaulu, kwa hivyo yeye hutuhesabia haki "wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu" (Rum. 3:24). Mungu hutufanyia kitu ambacho hatungeweza kujifanyia wenyewe—na hiyo ni neema! Huu ni msingi wa injili na habari nzuri zaidi ambayo mtu anaweza kuisikia. Mungu ametupa riziki kamili kwa neema Yake kupitia kwa Yesu Kristo na tunachotakiwa tu kufanya ni kuamini.

Uzima na kazi ya Yesu iliyokamilika inawarejesha wanadamu wote mahali pa kuhusiana na Mungu kwa imani. Hii ni kazi ya neema. Imani ndiyo itikio letu kwa kile tulichopewa na Mungu katika Kristo.

Tunapofahamu kwamba Mungu ameturejesha mahali pa kuhusiana naye kwa imani, tunaweza kuanza kuamini kina cha neema Yake. Amesamehe dhambi zetu zote" sawasawa na wingi wa neema yake" (Efe. 1:7), na "dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi" (Rum. 5:20). It is "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu" (Efe. 2:8). Kila kitu ambacho Mungu amefanya kutusamehe dhambi zetu na kutuokoa amefanya kwa neema Yake. Lakini neema haikomei hapo.

Kumbuka, msukumo wote wa kila kitu afanyacho Mungu ni ili tuweze kupokea uzima Wake. Hii ndiyo sababu Yesu alikuja. Alikuja ili tupate uzima, na uzima tele tele (Yohana 10:10). Alizungumzia kusudi hili katika huduma yake yote. Sikiza alichosema Yesu:

- "Maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake. "Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima" (Yohana 5:39-40).
- "Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho" (Yohana 6:40).
- "...Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu" (Yohana 10:28).
- Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana l4:6).
- "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana I7:3).

Yohana mwenyewe alitwambia, "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu" (Yohana 1:4) na kwamba "ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye." (Yohana 3:15). Alifanya muhtasari wa injili yake yote kwa maneno haya:

> . . . Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake (Yohana 20:31).

Haya yote yanatuelekeza kwa kiini cha neema. Paulo alieleza mambo haya yote wazi aliposema kwamba wote "wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo" (Rum. 5:17) na kwamba "neema itawale hata uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu." (Rum. 5:21). Uzima wa milele sio kurejelea tu kitu tupokeacho baada ya kufa. Mungu ametuunganisha na uzima sasa! Uzima wa milele ni ubora wa uzima wa milele tunaopata katika maisha haya nao huendelea katika umilele wote. Hii ndiyo sababu ya Yesu kufufuka kutoka kaburini. Alikuwa "mzaliwa wa kwanza" kutoka kwa wafu (Kol. 1:18; Rum. 8:29) ili aweze kuwa "roho yenye kuhuisha"

(1 Cor. 15:45). Hii ni kazi ya neema ya Mungu kwa wanadamu wote. Hii ndiyo maana neema ni neno geni katika Agano la Kale. Ilibidi Yesu afe na afufuliwe kwa nguvu za "uzima usioharibika" (Heb. 7:16 NEN) ili aweze kuwaYule anayewapa uzima wote waaminio!

Nadhani wengine wetu huamini neema ni nguvu za kiajabuajabu ambazo Mungu hutupa wakati mwingine ili tuweze kuyavumilia maisha haya. Namkumbuka mhusika fulani anayejulikana kama Luke Skywalker katika sinema za "Star Wars". Vita vinapochacha, yeye husikia sauti ya mnasihi wake, Obi-Wan Kenobi, mawazoni mwake akinena kwa sauti ya kuogofya, "Luke, tumia nguvu." Hivi ndivyo wengi wetu huiona neema kuwa. Tunadhani ni "nguvu" tunazopewa zitusaidie wakati tuna hitaji fulani.

Paulo aliiona neema ya Mungu kuwa njia halisi kabisa ya yeye kuyaishi maisha yake. Hakikuwa tu kitu fulani ambacho Mungu alimpa ili aweze kuvumilia hali zenye changamoto. Ni kweli kwamba alipokuwa akisumbuliwa na mwiba uliokuwa mwilini mwake, Bwana Yesu alimwambia, "Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu" (2 Kor. 12:9). Hebu tazama alichosema Paulo mwisho wa kifungu hicho: "Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangue" (2 Kor. 12:9). Hiyo ndiyo neema! Ni nguvu za uzima wa Kristo zinazokaa ndani ya Paulo.

Napenda alichosema Paulo katika 1 Wakorintho 15:10:

> Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami..

Paulo alikuwa na ufunuo kamili wa neema. Alijua neema ndiyo ilifanya awe alichokuwa; kwamba neema aliyopewa ilikuwa ya kufaa; na kwamba ni neema iliyotimiza kila kitu. Neema hutuunganisha kwa uzima wa Kristo, na sababu yote ya Yesu kuja ni ili sisi tupate uzima. Ni lazima tuuzingatie ukweli huu. Mungu anataka kutupa uzima naye anafanya hivyo kwa neema (Efe. 2:8-9; Rum. 5:21; Tito 3:7).

Paulo na Petro waliandika nyaraka kumi na tano kati ya nyaraka ishirini na moja katika Agano Jipya. (Nyaraka ni barua ambazo mitume waliandikia makanisa ya Agano Jipya baada ya Pentekoste.) Kila moja ya barua hizi ina salamu ambayo ni mtindo wa kuandika uliojulikana sana nyakati hizo. Katika salamu za kila moja ya barua hizi, Paulo na Petro wanaongeza maneno haya "neema na amani." Paulo mara nyingi alisema, "…Neema na iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo" (Rum. 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2). Je, yaweza kuwa sadfa kwamba barua hizi zote zinaanza kwa kuwakumbusha wasomaji juu ya neema na amani? Sidhani. Paulo alisema katika Warumi 5:1-2:

> Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu.

Paulo alijua kwamba tuna amani kwa ajili ya neema ya Mungu. Amani hutujia tunapojua kwamba tuko katika uhusiano ulio sahihi (yaani tumehesabiwa haki) na Mungu, na njia pekee ya kuwa katika uhusiano sahihi na Mungu ni kwa neema Yake. Tukiamini kwamba kusimama kwetu mbele za Mungu kunahusiana na utendaji wetu kupitia matendo, hatutapata amani kamwe. Neema ya Mungu imeondoa hitaji la sisi kufanya matendo ili kupata kibali Chake. Hili linatuondolea mzigo mkubwa na kutupatia amani. Bila neema hakuna amani. Tunapata amani yetu kwa sababu tumehesabiwa haki kwa imani na "tunashangilia katika tumaini la utukufu wa Mungu" ambalo ni "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu!" (Kol. 1:27).

Neema si njia ya kueleza mwenendo au silika ya Mungu kwetu sisi. Tukiichukulia neema kwa jinsi hii, tutaelekea kuieleza sawa na vile tunavyoueleza uhusiano wetu na wengine. Sisi husema kwamba "tunamwonyesha neema" au "tunampa neema" mtu fulani. Tunaponena hivi, tunadunisha maana halisi ya neema katika mawazo yetu. Biblia haisemi lolote kuhusu watu kuwapa wengine neema. Ni mara moja tu ndipo inaunganisha neema kwa matendo yetu. Wakati Paulo alisema, "Maneno yenu yawe yamejaa neema siku zote, yanayofaa, ili mjue jinsi iwapasavyo na inavyofaa kumjibu kila mtu." (Kol. 4:6 NEN). Tunapoingiliana na wengine, Paulo anatwambia pia,

> Kwa hiyo, kwa kuwa ninyi mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao sana, jivikeni moyo wa huruma, utu wema, unyenyekevu, upole na uvumilivu. Vumilianeni na kusameheana mtu akiwa na lalamiko lolote dhidi ya mwenzake. Sameheaneni kama vile Bwana alivyowasamehe ninyi. Zaidi ya maadili haya yote jivikeni upendo, ambao ndio unaofunga kila kitu pamoja katika umoja mkamilifu (Kol. 3:12-14).

Zote hizi ni sifa nzuri za hulka ya Mungu zinazopaswa kudhihirika tunapoingiliana na wengine. Tunaweza kusema kwamba zote ziko chini ya kunda la kuwa "mwenye neema." Tunaposema mtu fulani ni mwenye neema, tuna maana kwamba mtu huyo anadhihirisha aina hizi za sifa anapoingiliana na wengine. Sote tunapaswa kufanya kila jitihada kuwa watu wenye neema. Kudhihirisha sifa hizi bainishi ni kudhihirisha hulka ya Mungu. Biblia haituagizi tuwape wengine neema. Hii haiwezekani kwa sababu Mungu pekee ndiye anaweza kuwapa watu neema.

Sababu ya kusema kwamba Mungu pekee ndiye anaweza kutupatia neema ni kwa vile neema ni Mungu kutupatia nafsi yake Mwenyewe. Neema si kitu bali ni Mtu! Tunapomwamini Kristo mara ya kwanza, tunapokea neema tele na kipawa cha uzima wa Mungu. Kuanzia hapo, tunasimama ndani ya neema hii (Rum. 5:2) na kuilenga imani yetu kwa uzima Wake ulio ndani yetu (Gal. 2:20; Kol. 2:6-7). (Tutazingatia mada hii kinagaubada katika Sura ya 4 kuhusu Imani.) Wajibu wetu ni kukubali na kupokea neema ya Mungu wakati wote na kuiruhusu ifanye kazi ndani yetu na kupitia kwetu. Huu ndio msingi wa maisha ya Kikristo.

Napenda ukweli huu kwamba kupitia neema Mungu daima anatupa uzima Wake. Anaishi ndani yetu. Tuna uwezo wa kuitikia uzima Wake anaotupatia kila siku. Hata tukijipata katika hali gani, neema Yake iko nasi na inatosha (2 Kor. 12:9).

Ukijaribu kuishi bila kweli hii kujikita ndani yako, utaingia katika mtego wa kujaribu kuyaishi maisha ya Kikristo kwa nguvu zako mwenyewe. Hutaweza kukubali na kutambua kwamba kwa neema Mungu amekupa kipawa kilicho kikuu zaidi ya yote—uzima wa Kristo ulio ndani yako, tumaini la utukufu.

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Neema ni uhalisi wa uzima wa Kristo unaondelea kuwa ndani yako ili uweze kuhisi uzima Wake ukiishi ndani yako, kupitia kwako, kama wewe.

**Tamko la Imani:** Nimepokea kutoka kwa ukamilifu wa Yesu, neema juu ya neema, na ninapopokea wingi wa neema na kipawa cha haki, nitatawala maishani kupitia kwa Yule Mmoja, Yesu Kristo (Rum. 5:17).

### *Kuenenda Katika Kweli*

Unapoishi kila siku, chagua kuikubali neema ya Mungu iliyo ndani ya maisha yako. Zingatia kweli hii kwamba kupitia kwa neema ya Yesu Kristo, uzima Wake ulio ndani yako unatosha kwa kila

hali utakayokabiliana nayo. Ishi ukifahamu kwamba uzima Wake ulio ndani yako unakupa kila kitu unachohitaji. Kwa ajili ya neema, uzima Wake unaishi ndani yako na unaweza kumhisi akiishi maisha Yake kupitia kwako kila siku!

Fikiria juu ya hali halisi ya maisha yako kama vile: uhusiano, hali kazini, au changamoto lako binafsi. Amua kupokea neema Yake katika hali hiyo ya maisha yako na umwambie Yesu adhihirishe uzima Wake ndani yako na kupitia kwako katika hali hiyo.

# 4

# IMANI

*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, "Mwenye haki ataishi kwa imani."*

*~ Warumi 1:16-17*

*Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu.*

*~ Wagalatia 2:20*

Ikiwa neema ni kipawa cha Mungu kinachotupatia uzima Wake, basi imani ni njia ya kuipokea. Imani lazima iwe kiini cha kila mazungumzo yanayohusu maisha ya Kikristo. Tunapozingatia kwamba "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao" (Ebr. 11:6), tunaona wazi kwamba imani ni ya lazima kabisa. Si kitu cha kujadiliwa. Tunaitwa "waumini" kwa sababu tuna imani. Imani daima imekuwa na daima itakuwa msingi wa jinsi tunavyotakiwa kuhusiana na Mungu. Uwezo wetu wa kudhihirisha imani unatufanya tuwe wateule katika viumbe wote wa Mungu. Alituumba na uwezo wa kuidhihirisha imani kwake.

Nina hakika unakubali kwamba imani inahitajika ili mtu awe Mkristo. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kubaki tu katika ufahamu wa mwanzo kuhusu imani na kukosa kweli muhimu sana ya nini maana kamili ya "kuishi kwa imani" (Hab. 2:4, Rum. 1:1 7). Kwa miaka mingi iliyopita imenisaidia kufahamu imani kwa njia tatu halisi: (1) imani ya wokovu; (2) imani ya kupokea; na (3) imani ya kuishi. Hii haimaanishi kwamba ninaamini kuna "imani" mbalimbali. Kuna "imani moja" tu (Efe. 4:5), lakini itakuwa muhimu kuangalia njia tatu ambazo imani inatenda kazi katika maisha yetu.

Labda umeyasikia maneno haya "imani inayookoa". Yanatoka kwa Waefeso 2:8-9 ambapo Paulo alisema,

> Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.

Tumeokolewa kwa neema kwa kuitikia injili kwa imani. Paulo alisema, "...Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. " (Rum. 10:9). Vifungu hivi vinazungumzia imani yetu ya mwanzo katika Bwana Yesu Kristo. Paulo aliita hii "tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake" (Rum. 5:2). Tunapoitikia mara ya kwanza kwa imani ndivyo tunavyoanza uhusiano wetu na Mungu. Lakini hii inaashiria tu mwanzo wa maisha yetu ya Kikristo. Kuna mengi zaidi tunayohitaji kufahamu kuhusu imani.

Baada ya kuanza uhusiano wetu na Mungu, tunakua katika imani yetu. Imani yetu inahitaji kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Hiii ina maana kwamba tunaanza kumwamini Mungu katika hali halisi za maisha. Ninaiita hii "imani ya kupokea." Mungu anataka tumwamini kwa kila kitu tunachohitaji. Tunajifunza kumtegemea kupata mahitaji ya msingi ya maishani (angalia Mat. 6:25-34). Kuishi kwa imani kunapaswa kuwa njia ya kawaida ya maisha yetu. Hii ina maana kwamba tumwamini Mungu na kuwa na amani kwamba anajua tunachohitaji na anaweza kutupatia kwa wakati Wake na kwa njia Yake. Hiki ni kitu ambacho mimi na mke wangu tumekusudia katika maisha yetu kwa miaka mingi iliyopita, na tumejjifunza kwamba Mungu ni mwamini kwa kila namna.

Kumwamini Mungu atupe vitu katika kila sehemu ya maisha yetu hakupasi kuwa zingatio kuu la safari yetu ya imani. Ni rahisi kuingia katika mtego wa kutumia nguvu zetu nyingi "kumwamini" Mungu atupe vitu. Ni rahisi kuichukulia imani kuwa kifaa tunachotumia kupata vitu. Tunadhani kwamba tukiwa tu na imani ya kutosha kupata kitu chochote hatimaye tutakipokea kutoka kwa Mungu. Hii ndiyo ninayoiita "imani iliyoendelezwa kupita kiasi" na inaweza kuleta matatizo kwa njia kadhaa.

Kwanza, imani iliyoendelezwa kupita kiasi mara nyingi humzingatia mwanadamu. Hakuna shaka kwamba Mungu anaweza na huwa anatupatia vitu kutokana na imani yetu. Tunaona hili mara nyingi katika vitabu vya injili Yesu anapofanya miujiza. Mara nyingi aliwaambia watu walipokea kwa ajili ya imani yao (Mat. 9:22, 29; 15:28; Marko 5:34; 10:52; Luka 7:50; 8:48; 17:19). Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba tunaweza tu kuwa na imani na tukapata kila kitu tunachotaka na tunachotarajia Mungu atende. Mara nyingi tunaweza kuziacha tamaa zetu za kutaka kitu fulani ziongoze imani yetu. Yakobo alisema, "Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu." (Yakobo 4:3). Mungu anaweza kuona nia zilizo ndani ya moyo wako na mara nyingi yeye anajali sana kuhusu hali ya moyo wako kuliko anavyojali kuhusu kukupa tu kitu unachotaka (angalia Ebr. 4:12; I Kor. 4:5). Yeye atafanya kazi maishani mwako kufichua nia mbaya na kukuleta mahali pa kumtegemea. Ikiwa atakupa tu kila kitu ulichokuwa na imani utapata, hungemhitaji kwa kweli. Mungu anataka umhitaji Yeye jinsi alivyo kuliko wewe umtumie kupata anachoweza kukupa.

Pili, imani iliyoendelezwa kupita kiasi inaweza kupuuza umuhimu wa kulisikiza neno la Mungu kuhusu maisha yetu. Kuna kanuni rahisi lakini inayopuuzwa mara nyingi.. "Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo" (Rum. 10:17). Hii inamaanisha kwamba kabla ya kuwa na imani lazima tusikie kwanza. Hii inatumika kwa kila sehemu ya maisha. Hatuwezi kuingia katika uhusiano na Mungu kwa imani tusiposikia kwanza neno la Kristo likinenea mioyo yetu. Hii vilevile ni kweli tunapoendelea kukua katika uhusiano wetu na Mungu. Tunahitaji kwanza kusikia neno tulilonenewa, na tunaposikia neno Lake, tunaweza kuitikia na kumwamini Yeye kwa imani.

Hakuna mipaka ya kile Mungu anaweza kuinenea mioyo yetu. Huenda baadhi ya mambo

atakayounenea moyo wako yatakuwa magumu kwako kuyaamini mwanzoni, lakini mara tu unapopata hakikisho kwamba umemsikia Yeye utakuwa na imani ya kumwamini. Tatizo huja usipokuwa na hakika kwamba umelisikia neno Lake na ukaamua kuanza kuamini hata hivyo. Hapa ndipo "imani" yako inaweze kuteleza na kuingia katika kudhania. Unahitaji kujifunza kuweka imani yako kwa kile unachojua Mungu amenena na kuyaacha mambo mengine nyuma ikiwa huna hakika umemsikia Mungu.

Imani ya wokovu na imani ya kupokea yote ni lazima katika maisha ya kila Mkristo. Hata hivyo, kuna ufahamu wa kina zaidi wa kuishi kwa imani ambao Mungu anataka kutupatia.

Mojawapo ya kweli kuhusu maisha ya Kikristo iliyo ya mwanzo zaidi—lakini ya uchochezi—ni kwamba hatukutakiwa kuyaishia maisha kwa nguvu zetu wenyewe. Ndiyo, hilo ni sahihi! Wewe na mimi hatuwezi kuyaisha maisha ya Kikristo kwa juhudi zetu wenyewe. Tumeona katika sura iliyoitangulia hii kwamba Mungu hutupatia neema Yake ili itufanyie kile tusichoweza kujifanyia. Kweli hii inatakiwa kuingia ndani ya maisha yetu kwa hali halisi.

Paulo alisema,

> Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu (Gal. 2:20 NEN).

Paulo hakujiona tena kuwa ni yeye aliyekuwa hai na aliyeyaishi maisha yake. Badala yake, Kristo ndiye aliyeishi ndani yake na uhai aliokuwa nao Paulo aliishi kwa imani ndani ya Mwana wa Mungu. Hii ni kauli yenye maana kuu na ni badiliko kuu la mtazamo. Kabla ya Bwana kunisaidia kuiona kweli hii ya ajabu sana, nilifikiri kwamba maisha ya Kikristo yalikuwa kitu nilichohitaji kufanya kwa nguvu zangu mwenyewe na kupitia kwa juhudi zangu mwenyewe.

Ninakumbuka mtindo wa "Je, Yesu Angefanya Nini" (WWJD) uliokuwa maarufu sana miongoni mwa Wakristo katika miaka ya 1990. Dhana hiyo ilikuwa kwamba Wakristo wangevaa bangili yenye herufi hizi WWJD. Herufi hizi zinatoka kwa maneno ya Kiingereza "What Would Jesus Do?" (Je, Yesu Angefanya Nini?) Dhana hiyo ilikuwa kwamba ungejiuliza swali hili katika kila hali. Kisha ungejaribu kutenda sawa na vile ulidhani Yesu angetenda ikiwa angekuwa katika hali hiyo hiyo.

Sidhani kwamba dhana ya "WWJD" ni mbaya, lakini ni tofauti kabisa na kuishi kwa imani. Kwa Paulo, mtu hawezi kuishi maisha ya Kikristo kwa kujaribu kujua kile Yesu angefanya iwapo angekuwa katika hali sawa na yetu. Kweli ni kwamba Yesu anaishi maisha Yake kupitia kwetu sisi. Anataka kuyadhihirisha maisha Yake kila wakati ndani ya maisha yetu na kupitia kwa maisha yetu. Njia pekee ambayo jambo hili hufanyika ni kupitia kwa imani yetu na kumwamini kabisa. Je, unaiona tofauti hiyo?

Hii ni tafsiri yangu binafsi ya Wagalatia 2:20:

> Mimi (nafsi yangu ya dhambi iliyokuwa ikiishi kama mtu wa kale) nilisulubiwa na Kristo (ile sehemu yangu ya kale ilikuwa ndani ya Kristo alipokufa msalabani nami nilikufa naye alipokufa) wala si mimi tena ninayeishi (nafsi yangu ya dhambi iliyokuwa ikiishi kama mtu wa kale) bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu (ili ayahuishe maisha yangu kwa uhai Wake ulio ndani yangu); Uhai nilio nao sasa (maisha yangu ya kawaida katika dunia hii) ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu (inayomaanisha kwamba kila siku na kila dakika ninaweza kufahamu, naamini kwamba anaishi maisha Yake ndani Yangu kufanya, kutenda, na kunena ili adhihirishe uzima Wake kupitia kwangu) aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu (ananifanyia haya kwa sababu ananipenda na aligharamia kila haki ya maisha yangu).

Mungu ananuia Yesu awe uhai wako. Hakukusudia kwamba ujaribu kwa bidii sana kuishi maisha ya Kikristo au hata kutenda mambo kama Kristo. Yesu anaishi ndani ya mwili wako kwa Roho Wake ili awe chemchemi ya uzima.

Vifungu hivi vyote vinawasilisha kweli hii. Chukua muda uvisome na utafakari kile ambacho vinasema nini.

- Lakini tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu (2 Kor. 4:7 NEN).
- …siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. 11Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti (2 kKor. 4:10-11 NEN).
- Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida (Flp. 1:21 ).
- Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu (2 Kor. 12:9).
- Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu (Gal. 2:20 NEN).
- Kwa maana ninyi mlikufa, nao uhai wenu sasa umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Wakati Kristo, aliye uzima wenu, atakapotokea, ndipo nanyi mtakapotokea pamoja naye katika utukufu (Kol. 3:3-4).

Hii inatoa maana mpya kabisa ya kuishi kwa imani. Sio tu kumwamini Mungu kututimizia mahitaji yetu. Kuishi kwa imani ni kumwamini Yesu aishi maisha Yake ndani yetu na kupitia kwetu. Ndiyo maana unahitaji kutumaini na kuamini (yaani kuwa na imani) kwamba Yesu anaishi maisha Yake ndani yako na kupitia kwako wewe kila siku. Unapomtegemea kwa ukamilifu na kujiweka chini ya uhai Wake ulio ndani yako kwa imani, Yeye ataanza kudhihirisha uhai Wake ndani yako na utaanza kuuona uhai Wake ukiishi kupitia kwako u (2 Kor. 4:10-12).

Hili linaturudisha kwa ushuhuda wangu katika Sura ya 1 kuhusu ndoa yangu. Mungu alinisaidia kuifahamu kanuni hii. Nilianza kuweka tumaini langu ndani ya Yesu ili aishi kupitia kwangu kama mume wa Stephanie. Kufanya hivyo kulifaulu. Yesu aliishi ndani yangu naye ni mume wa ajabu.

Mimi sikuwahi kufurahia majaribio shuleni, lakini sote twajua kwamba ni mojawapo ya vitu ambavyo ni lazima tufanye. Pia kuna majaribio yetu sisi waumini ambayo tunatakiwa kufanya. Hili ni jaribio la kujua ikiwa tunafahamu kiini cha imani. Paulo aliwaambia waumini wa Korintho:

> Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa? (2 Kor. 13:5).

Jaribio unalotakiwa kufanya ni kujua ikiwa uko "katika imani" au la. Jaribio hili ni rahisi sana kwa sababu lina swali moja tu. Swali hilo ni hili "Je, wajua kwamba Yesu Kristo yuko ndani yako?" Jibu la swali hili litaamua ikiwa utapita au utaanguka jaribio hilo. Ikiwa jibu lako ni "Ndiyo," uko katika imani na umepita jaribio hilo. Ikiwa jibu lako ni "La," hauko katika imani na umeanguka jaribio hilo. Kujua kwamba uko katika imani kunamaanisha kwamba unajua, unaamini, na una tumaini kwamba Yesu yuko ndani yako kuishi

Maisha yake Kupitia kwako. Hii ndiyo maana ya kuishi kwa imani na hii ndiyo maana ya kuwa Mkristo.

Hii ndiyo hali halisi kabisa ya kuishi maisha ya Kikristo. Yesu yuko ndani yako kuishi maisha Yake kupitia kwako. Unapomwamini kufanya jambo hili, anakufanya uufuate mfano Wake. Unachohitaji kufanya tu ni kuendelea kuamini kwamba Yesu ni uhai wako. Kadri unavyoamini zaidi kweli hii, ndivyo unavyopata zaidi uhalisi wa uhai Wake ndani yako. Mungu anapoiona imani yako na vile unavyomtegemea Yesu, anaanza kuyageuza maisha yako. Unafanywa kuwa na mfano wa Yesu na hili ni jambo la ajabu sana! Mwenendo, mawazo, nia, na matendo yako yanaanza kubadilika. Huu ni muujiza wa maisha ya Kikristo. Mungu kwa kweli ndiye "atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema" (Flp. 2:13).

Mojawapo ya vifungu nivipendavyo vinavyonisaidia kuifahamu imani yangu katika Yesu ni Wakolosai 2:6-7. Paulo alisema,

Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani.

Tunavyoenenda katika Kristo Yesu ndivyo tunavyompokea Yeye. "Kuenenda" ni isitiari inayoeleza utaratibu wa kuyaishi maisha ya Kikristo. Tunajua kwamba njia pekee ya kumpokea Kristo Yesu ndani ya maisha yetu ni kwa imani—imani ya wokovu. Hakuna tunachoweza kufanya ili tuokoke ila kuwa na imani katika Yesu. Na hakuna tunachoweza kufanya ili kuishi maisha ya Kikristo ila kuwa na imani katika Yesu.

Mimi hushangaa kwamba huwa tuko radhi kuhubiri ujumbe wa injili wa wokovu ulio rahisi na kuwaambia watu kwamba wanachohitaji tu kufanya ili waokoke ni kuamini; lakini tunageuka baada ya wao kuokoka na tunawaambia mambo yote wanayohitaji kufanya ili waishi maisha ya Kikristo. Hii ndiyo maana Wakristo wengi huhisi kuchoka sana, kuvunjika moyo, kukata tamaa, na hatimaye "hurudi nyuma." Hawawezi kutimiza masharti yote ya kuwa Mkristo kwa kujaribu kufanya mambo yote yaliyo sahihi kwa nguvu zao wenyewe. Hawajasikia hadithi nzima. Jinsi unavyompokea Yesu ndivyo unavyoenenda ndani Yake. Na njia pekee ya kuenenda ndani Yake ni kwa imani.

Ufahamu wako kuhusu imani unatakiwa kufikia kiwango cha kina zaidi cha kumwamini Kristo aliye ndani yako. Kiini cha uhai wako ni "kujifunza Kristo" kwa kumsikia na "mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu" (Efe. 4:20-21). Hili hutendeka unapolenga imani yako kwake, unapoamini kwamba Yeye ni uzima wako na kumwamini aishi kupitia kwako kila siku.

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Kuishi kwa imani kunamaanisha kuamini uhai wa Yesu ulio ndani yako uishi ndani yako, kupitia kwako, kama wewe.

**Tamko la Imani:** Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu. (Gal. 2:20).

### *Kuenenda Katika Kweli*

Lelekeze imani yako leo kwa kweli hii kwamba Yesu Kristo anaishi ndani yako. Amini kwamba Kristo ataishi kupitia kwako katika kila hali na jambo. Ikiwa kuna uhusiano au hali unayoijua katika maisha yako unayotambua kuwa unang'ang'ana kutenda, kunena, au kufikiri kwa njia inayoleta uhai, tumaini kwa imani kwamba Yesu anaishi kupitia kwako katika hali au jambo hilo. Kristo, aliye uhai wako, atafanya kupitia kwako kile usichoweza kufanya kwa nguvu au juhudi zako mwenyewe. .

# 5

# HAKI

*Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.*

*~ 2 Wakorintho 5:21*

*Na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*

*~ Waefeso 4:23-24*

Mnamo Oktoba 31, 1517, Martin Luther alipigilia tasinifu zake tisini na tano juu ya mlango wa kanisa kule Wittenberg, Ujerumani. Matendo yake siku hiyo yalianzisha kile kilichojulikana kihistoria kama Mageuzo ya Protestanti. Katika kiini cha mageuzo hayo kulikuwa na mjadala unaohusu kuhesabiwa haki kwa imani na pamoja na haki ya Mungu. Wakati wengi wetu hawawezi kueleza kwa ufasaha tofauti ndogo za matukio haya katika historia ya kanisa, nakuhakikishia kwamba sote tumeathiriwa nayo. Kanuni za kiteolojia zilizoibuka kutoka kwa kipindi hiki cha wakati zimeathiri fikra za Wakristo kuhusu Mungu kwa miaka 500 iliyopita. Wewe na mimi tukiwemo, na mambo mengi ambayo tunaamini kuhusu kupokea wokovu kwa imani, kuhesabiwa haki, na haki yameundwa na maoni ya waleta mabadiliko kama Martin Luther na John Calvin.Righteousness is one of the most common themes in the Bible.

Haki ni mojawapo ya maudhui katika Biblia yanayojulikana sana na wengi. Waandishi wa Biblia wanataja haki zaidi ya mara 300. Ni neno moja linaloeleza kiini cha hulka ya Mungu kuliko neno lingine lolote. Ikiwa "Mungu ni pendo" (1 Yohana 4:16) ni kauli sahihi kabisa kuhusu kile Mungu alicho, basi "haki ya Mungu" (Rum. 3:21) ni kauli sahihi kabisa kuhusu vile Mungu alivyo.

Teolojia mara nyingi huwa na njia ya kufanya mambo yawe ya tata badala ya kuyafanya yaeleweke vizuri zaidi. Wanateolojia wamejadiliana kwa karne nyingi kuhusu ufafanuzi wa haki na nafasi

inayochukua katika uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Wakati mwingine mimi huegemea kwa mtazamo wa "Teolojia kwa walio wapumbavu" kufanya mambo yawe halisi na ya kueleweka. Huo ndio mtazamo wangu ninaposhughulikia mada kama vile haki.

Fafanuzi nyingi za haki husisitiza sana juu ya maadili. Kwa mujibu wa hizi fafanuzi, haki ni hali ya hulka ya Mungu inayoleta sifa za kiwango cha uadilifu Wake. Tukiitazama haki kwa njia hii, tunazingatia kiwango cha uadilifu ambacho Mungu anataka tuweze kukifikia katika mitazamo na matendo yetu. Bila shaka kuna hali ya uadilifu katika haki, lakini siamini kwamba hicho ndicho kiini muhimu sana. Neno hilo lina maana ya "kuwa sahihi au mwenye haki." Mara ya kwanza neno "haki" linaonekana katika Biblia ni wakati Mungu alikuwa akizungumza na Abrahamu. Abrahamu "Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki" (Mwa. 15:6). Uhusiano kati ya Abrahamu na Mungu haukuhusu mwenendo wa uadilifu wa Abrahamu. Yeye alimwamini tu Mungu na Mungu akamtangaza kuwa "sahihi." "Kuwa sawa" kwake au "haki" kulitegemea imani yake na sio matendo yake.

Kuna sababu inayofanya tuwe na tatizo la kuiona haki kwa mtazamo wa Mungu. Fikira zetu zimetiwa doa na dhambi. Dhambi iliingia ulimwenguni Adamu na Hawa walipokula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya (Rum. 5:12). Hili lilipofanyika, mtazamo wao wote ulifafanuliwa kulingana na uadilifu, hii ni sawa na kanuni zinazohusu tofauti iliyoko baina ya mema na mabaya—sahihi na isiyo sahihi. Mungu hakumuumba mwanamume na mwanamke waishi na uwezo huu. Ndiyo maana kikawa kitu cha kwanza ambacho Mungu aliwazuia kufanya. Alijua madhara ambayo yangeletwa kwa wanadamu. Lakini kwa ajili ya upendo, Mungu alimpa Adamu na Hawa uhuru wa kuchagua. Mengine ni historia!

Mungu hakunuia uhusiano wetu na Yeye utegemee shughuli zetu za uadilifu na uwezo wetu wa kufanya mambo yaliyo sahihi. Anataka uhusiano wetu naye utegemee uzima. Tangu mwanzo wa nyakati, alitaka kushiriki nasi uzima Wake ili tuweze kuishi naye katika uhusiano ulio salama na wa kudumu. Tangu mambo yalipohabirika katika bustani, Mungu alianza kuelekea kwa kusudi lake kuu la kuwarejesha wanadamu mahali ambapo wangeshiriki katika uzima wake.

Hii ni kweli muhimu sana katika uhusiano wetu na Mungu. Kile ambacho Mungu alitaka ni kuwa katika uhusiano wa kumpa mwanadamu uzima. Hakunuia kufanya utendaji wetu uwe msingi wa uhusiano wetu naye. Lakini, Adamu na Hawa walipofanya uamuzi wa kula tunda kutoka kwa mti waliokuwa wamekatazwa, walibadilika kabisa na pia uhusiano wao na Mungu ukabadilika. Mungu alipowapa uhuru wa kuchagua, alifanya mambo katika muktadha wa uamuzi wao.

Hii ni kweli muhimu inayotusaidia kuona jinsi tunaweza kuielewa vibaya haki. Mungu huchagua kuruhusu uamuzi wetu uendeleze vile tunavyohusiana na Yeye. Yeye habadiliki kamwe, lakini mtazamo wetu kumhusu Yeye hubadilika. Mara kwa mara, nathubutu kusema mara nyingi zaidi-mtazamo wetu kumhusu huwa si sahihi.

Kwa mfano, Mungu hakunuia wana wa Israeli wawe na mfalme. Lakini walisisitiza kwamba walitaka mfalme ili wawe kama mataifa yote yaliyowazingira na Mungu akawapa mfalme (1 Sam. 8:4-9). Tangu wakati huo, inaonekana kana kwamba katika sehemu iliyofuata ya Agano la Kale Mungu "anakubali wawe na mfalme." Mungu aliitaka Israeli imtazamie Yeye kama mfalme wao na wamwamini awalinde na kuwapa walichohitaji. Lakini aliwaruhusu wawe na mfalme na akaruhusu ule mtazamo wao kwamba yeye "anakubali wawe na mfalme"uendelezwe na uamuzi wao wenyewe.

Daudi alisema,

> Kwa mtu mwenye fadhili
> utakuwa mwenye fadhili;
> Kwa mkamilifu

utajionyesha kuwa
mkamilifu;
Kwake ajitakasaye
utajionyesha kuwa mtakatifu,
Ka kwa mpotovu
utajionyesha kuwa
mkaidi (Zaburi 18:25-26).

Hivi ndivyo Mungu huhusiana nasi na hili huathiri vile tunavyoifahamu haki. Wakati Adamu na Hawa waliamua kuhusiana na Mungu kwa msingi wa mema na mabaya, sahihi na yasiyo sahihi, Mungu alikubali kuhusiana nao kwa jinsi hiyo. Lakini je, hivyo ndivyo Mungu alitaka uhusiano huo uwe?

Nafikiri labda unalijua jibu la swali hilo. Jibu hilo ni "La." Mungu alitaka uhusiano wetu na Yeye udhihirishwe na uzima. Alitaka kutupatia uzima Wake ili tuweze kufurahia uhusiano kamili milele. Hapa ndipo pangekuwa mahali pa kuwa katika uhusiano mwema na Mungu—kushiriki naye katika uzima Wake. Uwoga haukunuiwa kuwa sehemu ya uhusiano wetu na Mungu, ila tu usalama unaotokana na kujua kwamba Mungu amefurahishwa nasi. Lakini tukiamini kwamba uhusiano wetu na Yeye unategemea kufanya mambo yaliyo sahihi, kila mara tutang'ang'ana kwa hofu kwa sababu hatutawahi kujua ikiwa tunafanya mambo vizuri au la. Tunapojua na kuamini kwamba Mungu hakunuia tuhusiane naye kupitia utendaji wetu, tutaanza kuifahamu haki kwa mtazamo tofauti.

Paulo ana mengi ya kusema kuhusu haki ya Mungu kuliko mwandishi yeyote yule wa Biblia, na mengi ya yale ayasemayo kuhusu haki yako katika kitabu cha Warumi. Kitabu cha Warumi, kuliko vitabu vingine vyovyote, ni tasnifu ya Paulo ya injili. Alisema, "Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye" na "haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake" (Rum. 1:16-17).

Warumi 3:21-26 ina baadhi ya kweli muhimu zaidi kuhusu haki ya Mungu:

> Lakini sasa, haki itokayo kwa Mungu imedhihirishwa pasipo sheria, ambayo Sheria na Manabii wanaishuhudia. Haki hii itokayo kwa Mungu hupatikana kwa Yesu Kristo kwa wote wamwaminio. Kwa maana hapo hakuna tofauti, kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, wanahesabiwa haki bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu. Yeye ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake. Alifanya hivi ili kuonyesha haki yake, kwa sababu kwa ustahimili wake aliziachilia zile dhambi zilizotangulia kufanywa. Alifanya hivyo ili kuonyesha haki yake wakati huu, ili yeye awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu.

Kuna mambo mawili ya kutambua kuhusu haki ya Mungu katika vifungu hivi. Kwanza, Inadhihirishwa kwa kumwamini Yesu Kristo. Pili, Mungu alionyesha haki yake msalabani wakati Yesu alimwaga damu Yake kwa ajili ya msamaha wa dhambi. Hii ina maana kwamba Mungu alionyesha haki Yake na akaiweka wazi ili watu wote waione kupitia kwa dhabihu ya Yesu.


Paulo anasema kwamba wakati Mungu alichagua kuonyesha haki Yake msalabani na wakati alichagua kuzisamehe dhambi zote (hata zile zilizofanywa kabla ya Yesu kufa), alifanya jambo sahihi kwa sababu dhabihu kamili ya Yesu ililipa deni hiyo kwa ukamilifu. Alionyesha haki Yake. Hii inamfanya Mungu kuwa "mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu." (Rum. 3:26). Paulo anatwambia kwamba matendo aliyofanya Mungu kaitka matukio ya injili yanatuonyesha kwamba Mungu yuko sahihi kwa yote ayatendayo, na yeye ndiye ana haki ya kutangaza wenye haki kwa mujibu wa imani yetu katika yale ayafanyayo.

Kisha Paulo anaionyesha kweli hii ya ajabu katika sura mbili zinazofuata za Warumi. Msingi wa wasilisho hili umejengwa juu ya tofauti kuu iliyoko baina ya chaguo alilofanya Adamu na chaguo alilofanya Yesu. Adamu (na Hawa) walichagua kuishi bila kumtegemea Mungu na wakala tunda la mti ambao walikuwa wamekatazwa. Kutokana na matendo ya Adamu, mauti yaliwajia wanadamu!

Lakini Yesu alifanya chaguo tofauti. Alichagua kuishi kwa kumtegemea Baba Yake kabisa na kuuweka chini uhai Wake kama dhabihu iliyo kamili kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Paulo alielezea kukubali kwake kuwa dhabihu ya mwisho kama "tendo la haki." Alisema,

> Kwa maana ikiwa kutokana na kosa la mtu mmoja, mauti ilitawala kupitia huyo mtu mmoja, zaidi sana wale wanaopokea wingi wa neema ya Mungu na karama yake ya kuhesabiwa haki, watatawala katika uzima kwa njia ya huyo mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo. Kwa hiyo, kama vile kosa la mtu mmoja lilivyoleta adhabu kwa watu wote, vivyo hivyo pia kwa tendo la haki la mtu mmoja lilileta kuhesabiwa haki ambako huleta uzima kwa wote (Rum. 5:17-18).

Ni muhimu tuelewe kweli hii ya ajabu (angalia mchoro ulio katika ukurasa unaofuata). Kwanza, hakuna jambo tulilofanya ili kuhukumiwa mbele za Mungu. Ni kupitia kosa la Adamu la uasi ndiyo watu wote wakapata hukumu. Vivyo hivyo, hakuna tunaloweza kufanya ili kuhesabiwa haki mbele za Mungu. Tunahesabiwa haki kwa sababu ya kile ambacho Yesu ameshakifanya kupitia tendo lake moja la haki.




Pili, na hili ni jambo muhimu sana kulielewa, Paulo alisema kwamba, "kwa tendo la haki la mtu mmoja lilileta kuhesabiwa haki ambako huleta uzima kwa wote" (Rum. 5:18). Tukiiangalia kauli hii mara ya kwanza huenda ikaonekana kana kwamba Paulo anasema, kila mtu amehesabiwa haki. Ufafanuzi wa aina hii umewafanya watu wengine kukuza falsafa ya kilimwengu. Hii ni imani inayosema kwamba watu wote wataokoka haijalishi kama wataamini au la. Lakini Paulo hakuwa anasema hivyo. Kuna

tofauti kati ya kuhesabiwa haki "kwa watu wote" na kuhesabiwa haki "ya watu wote." Yeye anasema kwamba tendo moja la haki alilofanya Yesu msalabani lilileta kuhesabiwa haki ambako huleta uzima kwa watu wote. Hasemi kwamba tendo hilo lilisababisha watu wote kuhesabiwa haki. Anatwambia kwamba Mungu amefanya kila kitu kilichohitaji kupitia kifo cha Yesu kusababisha kuhesabiwa haki ambako huleta uzima kwa watu wote. Halafu anawapa kuhesabiwa haki watu wote watakaopokea kwa imani. Mungu amefanya kila kitu alichohitaji kufanya ili watu wote waweze kuhesabiwa haki, lakini lazima tupokee kipawa hicho kwa imani (Rum. 5:17). Tunapofanya hivyo, tunapata haki-kuwa sahihi mbele za Mungu.

Sasa kwa vile tunajua Mungu ameonyesha haki Yake kupitia kifo cha Yesu Msalabani na ametupatia hakikisho la uzima kwa kitendo hiki cha haki, tunaweza kuitumia kuona vile haki inaathiri maisha yetu kwa kiwango cha mtu binafsi. Paulo alionyesha hili kwa nguvu zaidi katika 2 Wakorintho 5:21. Alisema, "Kwa maana Mungu alimfanya yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu kwake yeye.." Angalia maneno haya mawili, "alimfanya" na "kuwa." Paulo anasema Mungu "alimfanya" Yesu, asiyekuwa na dhambi, kujua dhambi kwa niaba yetu. Yesu hakufanyika kuwa dhambi. Kigiriki cha asili katika kifungu hiki hakina maneno haya "kuwa". Mungu hakumfanya Yesu "kuwa" dhambi, Alimfanya yule asiiyekuwa na dhambi "kujua" au "kuipitia" dhambi kwa niaba yetu.

Lakini kuhusu kile ambacho Mungu alitufanyia, Paulo anasema kitu cha kushangaza. Alisema kwamba "tunakuwa" haki ya Mungu katika Kristo. Hili ni neno tofauti kabisa katika sehemu hii ya kifungu hiki. Neno "kuwa" katika lugha ya Kigiriki lina maana "kufanyika kuwa." Ni neno sawa na lile alilotumia Yohana aliponena akisema kwamba Yesu aliviumba vitu vyote. Alisema, "Vitu vyote viliumbwa kwa yeye, wala pasipo yeye hakuna chochote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa" (Yohana 1:3 NEN). Neno hili linamaanisha kwamba kitu fulani ambacho hakikuweko hapo awali kimeumbika. Paulo anasema kwamba sisi, ambao hatukuwa wenye haki, kweli tumekuwa haki ya Mungu katika Kristo. Kweli ya ajabu iliyoje!

Yesu alifanya alichofanya msalabani ili uwe mwenye haki. Pokea kweli hii ya ajabu kwa imani na "mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli" (Efe. 4:23-24).

Paulo alieleza kwa njia nyingine aliposema,

> Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanyika kwetu hekima itokayo kwa Mungu, yaani haki, na utakatifu na ukombozi. Hivyo, kama ilivyoandikwa: "Yeye ajisifuye na ajisifu katika Bwana" (1 Kor. 1:30-31).

Hauko katika njia ya kufanywa mwenye haki kwa kufanya mambo mengi zaidi yaliyo sahihi. Kristo ni haki yako na ukiwa ndani Yake wewe ni mwenye haki. Kuna tofauti kubwa kati ya wewe kuwa mwenye haki kwa kutegemea vile unatenda mambo na kuwa mwenye haki kwa kutegemea ukweli kwamba uko ndani ya Kristo!

Tunapoingia katika sura chache zinazofuata, itakuwa wazi vile Mungu ametupatia kila kitu kwa yale ambayo Yesu Kristo amefanya. Kuamini uhalisi wa haki yako ndani ya Kristo ni msingi wa wewe kuishi katika ukamilifu wa kuwa katika uhusiano mwema na Mungu. Amekufanya kuwa mwenye haki ili uwe na amani ipatikanayo kwa kujua bila shaka kwamba Mungu anapendezwa nawe kabisa. Mungu amekufanya kuwa mwenye haki kwa msingi wa kile ambacho Kristo amefanya na sio kwa kile unachofanya. Ni kwa msingi wa hulka yake, sio yako. Umekubalika na umethibitishwa kwa ajili ya haki Yake aliyoshiriki nawe bure.

*Kupata Kweli*

**Kweli:** Wewe ni haki ya Mungu katika Kristo Yesu.

**Tamko la Imani:** Naamini kwamba Mungu amenifanya kuwa mwenye haki kabisa, na najua kwamba hakuna ninachoweza kufanya ili kuwa mwenye haki na kupata kibali cha Mungu. Kwa ajili ya imani yangu katika Yesu, mimi niko ndani ya Kristo, ambaye ni haki yangu. Mimi ni mwenye haki!

*Kuenenda Katika Kweli*

Kila siku tafakari kuhusu maana ya kuwa mwenye haki. Uko katika uhusiano sahihi na Mungu na ameridhika kabisa na amependezwa nawe kwa sababu ya imani yako katika Kristo. Wakati wowote unapohisi kwamba Mungu hapendezwi nawe, chagua kuamini kweli kwamba amekufanya kuwa mwenye haki. Jikumbushe kwamba hauhitaji kujitahidi au kutenda mambo ili ukubalike na Mungu. Tulia katika kweli hii kwamba umekubalika ndani ya Yule aliye mpendwa leo!

# 6

# MSAMAHA

*Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote, Aukomboa uhai wako na kaburi, Akutia taji ya fadhili na rehema.*

*~ Zaburi 103:3-4*

*"Kwa hiyo ndugu zangu, nataka ninyi mjue kwamba kwa kupitia huyu Yesu msamaha wa dhambi unatangazwa kwenu. Kwa kupitia yeye, kila mtu amwaminiye anahesabiwa haki kwa kila kitu ambacho asingeweza kuhesabiwa haki kwa sheria ya Mose."*

*~ Mdo 13:38-39 (NEN)*

Labda umewahi kusikia msemo huu, "Ikiwa kitu kinasemekana kuwa kizuri kupita kiasi, huenda sivyo." Sote tumeusikia msemo huu mara nyingi na tumekuwa na nadharia ya kushuku vitu vinavyosikika kuwa vizuri kupita kiasi, hasa ni kwa sababu hatutaki kupitia hali za kuvunja moyo maishani. Hivi ndivyo watu wengi hufanya wanaponisikia nikifunza kuhusu msamaha wa Mungu. Wao huwa na shaka wanaposikia kweli hii kwa sababu inasikika kuwa nzuri kupitia kiasi.

Msamaha ni kiini cha injili. Daudi alitamka tamko la kinabii, "Heri aliyesamehewa dhambi, kusitiriwa makosa yake" (Zab 32:1). Zakaria, babake Yohana Mbatizaji, alitabiri maneno haya kuhusu Yohana baada ya kuzaliwa kwake:

"Nawe, mtoto, utaitwa
nabii wake Aliye juu,
Kwa maana utatangulia
mbele za uso wa Bwana
umtengenezee njia zake;
Uwajulishe watu wake wolovu,
Katika kusamehewa
dhambi zao" (Luka 1:76-77).

Wakati Bwana aliyefufuka alimkuta Paulo akiwa njiani kuelekea Dameski, alimwambia Paulo kwamba anamtuma kwenda kwa Wayuda na Mataifa

> "...uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi" (Matendo 26:18).

Yesu alitukomboa kwa damu Yake na akatusamehe dhambi zetu zote (Efe. 1:7, Kol. 2:13). Ujumbe wa injili ni wa msamaha wa dhambi.

Baada ya kusoma kile ambacho waandishi wa Agano Jipya wanasema kuhusu msamaha, nimetayarisha kauli tano ambazo ni muhtasari wa kile ninachokiona kuwa kiini cha mafunzo yao juu ya msamaha. Nitazitumia kauli hizi kama mwongozo wa majadiliano yangu. Nazo ni:

1. Msamaha ni kitu alichofanya Mungu hata kabla hatujazaliwa, au hata kabla ya kumwamini Yesu.
2. Yesu alipokufa msalabani, Mungu alizisamehe dhambi zote za nyakati zote.
3. Kwa vile Mungu amezisamehe dhambi zote za nyakati zote, dhambi zako za zote—za kale, za sasa, na za siku za usoni—zimesamehewa.
4. Baada ya kuwa Wakristo, hakuna tunachotakiwa kufanya ili kupata msamaha wa Mungu kwa sababu ni kitu ambacho tayari amekifanya.
5. Dhabihu ya Yesu na msamaha wa dhambi zetu vinaondoa hali ya kujiona kwamba tuna dhambi.

Hebu tuangalie kwa makini kila mojawapo ya kauli hizi tukitumie kile Maandiko yanafunza kuhusu msamaha.

*1. Msamaha ni kitu alichofanya Mungu hata kabla hatujazaliwa, au hata kabla ya kumwamini.*

Napenda kuwauliza watu swali hili, "Je, Mungu husamehe dhambi kwa misingi ipi?" Hii inamaanisha kwamba Mungu ana sababu gani au haki gani kusamehe dhambi. Jibu lake ni hili, Mungu husamehe dhambi kwa msingi wa Yesu kufa msalabani. Mungu amesamehe dhambi zote kwa ajili ya Mwanawe kutii na kumwaga damu Yake na kufa. Labda hujawahi kusikia maelezo haya, kwa hivyo hebu tutazame kwa makini.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania—Sitaanza kukisia huyo ni nani—anatwambia kwamba Yesu Kristo ni mpatanishi wa Agano Jipya. Wengi wetu tumesikia kuhusu "hati ya wasia." Kwa maneno ya kibinadamu hii ni hati ya kisheria inayoelezea mapenzi ya mwisho ya mtu kuhusu mali yake ya hapa duniani. Hati za wasia zinaweza kutofautiana kwa njia nyingi, lakini kuna kitu kimoja cha msingi kilicho sawa kwa zote. Hakuna kinachoweza kufanyika katika hati ya wasia mpaka mwenye wasia hiyo afe. Kuna kifungu muhimu cha Maandiko kinachoeleza kweli hii kuhusiana na msamaha wa dhambi. Mwandishi wa waraka wa Waebrania alisema,

Kuna kifungu muhimu cha Maandiko kinachoeleza kweli hii kuhusiana na msamaha wa dhambi. Mwandishi wa waraka wa Waebrania alisema,

> Na kwa sababu hii ni mjumbe wa agano jipya, ili, mauti ikiisha kufanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipokee ahadi ya urithi wa milele. Maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo mauti yake aliyelifanya. Kwa maana agano la urithi lina nguvu palipotukia kufa kwa mtu; kwa kuwa halina nguvu kabisa, akiwa yu hai yeye aliyelifanya (Ebr. 9:15-17).

Hapa kuna tofauti mbili muhimu kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Kwanza, Agano Jipya ni

bora zaidi kuliko Agano la Kale (Ebr. 8:7, 13). Ni bora kwa sababu Yesu alikuwa kuhani bora zaidi (Ebr. 7:22) na dhabihu bora zaidi (Ebr. 9:11-14). Pia lilifanyika kwa ahadi bora zaidi (Ebr. 8:6).

Pili, Agano Jipya lilikuwa fupi zaidi na lenye muhtasari kuliko Agano la Kale. Agano la Kale linarejelea agano alilofanya Mungu na watu wa Israeli alipompa Musa Sheria kule jangwani. Agano hili lilikuwa lenye masharti kwa kutegemea utendaji mambo wa wana wa Israeli na lilikuwa na amri 613. Mungu alijua tangu mwanzo kwamba wana wa Israeli wangemwacha na kukosa kudumisha agano hili (Kumb. 31:16). Baada ya mamia ya miaka ya kutotii, Mungu aliahidi kwamba angefanya Agano Jipya na Israeli (Yer. 31:31).

Agano hili halina masharti na lina mambo mawili tu. Mwandishi wa Waebrania alisema,
"Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana,

> "Nitatia sheria zangu mioyoni mwao,Na katika nia zao nitaziandika; ndipo anenap, Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa" (Ebr. 10:16-17).

Mambo mawili ya Agano Jipya ni haya:

1. Mungu atatia sheria Zake mioyoni mwetu na katika nia zetu.
2. Mungu atazisamehe dhambi zetu na hatazikumbuka tena.

Sasa hebu turudi kwa vifungu vinavyozungumzia Yesu kuwa mpatanishi wa Agano Jipya. Mwandishi huyu anatwambia kwamba Mungu alipoingiliana na Israeli alijua kwamba watu hawa hawakuwa na uwezo wa kudumisha aina yoyote ya mapatano na Yeye. Kila mara walikosea vibaya. Hii ilikuwa historia ya Israeli iliyoendelea (Kumb. 31:14-18). Mungu aliamua kufanya mapatano mapya (agano).


Agano Jipya alilofanya Mungu halikuwa kati ya Mungu na mwanadamu. Lilikuwa naye Mwenyewe. Mungu Baba na Mungu Mwana walifanya mapatano. Mungu aliamua kwamba angezisamehe dhambi zote za wanadamu milele. Kitendo hicho kilikuwa ni kutoa hati ya wasia. Lakini ili sharti la wasia huo litimie, aliyeandika wasia huo alitakiwa kufa. Kwa hivyo Mungu Mwana akafa.

Yesu alipokufa, agano alilotoa Mungu lilianza kufanya kazi. Sasa kuna swali kuu. Mimi na wewe tulifanya kazi gani katika utaratibu huu wote? Jibu ni "Hakuna." Hatukuhusika katika utaratibu huu hata kidogo. Je, maneno haya yanasikika kuwa mazuri kupitia kiasi? Hata yatakuwa mazuri zaidi. Ndiyo maana inaitwa injili, habari njema.

Yesu alipokufa, Mungu alizisamehe "dhambi kwa wakati wote" (Ebr. 10:12). Mungu alizisamehe dhambi kwa sababu Yesu alikufa. Aliheshimu agano alilofanya na Mwana (Isa. 42:6), na wakati Yesu alikufa, agano hilo lilianza kufanya kazi. Hili ni tukio la "mara moja tu" (Ebr. 10:10) ambalo halitawahi kurudiwa tena. Msingi wa Mungu kuzisamehe dhambi na wakati alisamehe dhambi ni vitu vinavyohusiana kwa hali isiyotenganishwa. Mungu alizisamehe dhambi kwa sababu Yesu alikufa, na Yesu alikufa takribani miaka 2000 iliyopita. Kutokana na ukweli huu tunajua msamaha ni kitu ambacho Mungu alifanya kitambo sana kabla ya sisi kuzaliwa, au hata kumwamini Yesu.

*2. Yesu alipokufa msalabani, Mungu alizisamehe dhambi zote za nyakati zote.*

Sasa kwa vile tunajua msingi wa Mungu kuzisamehe dhambi na wakati ambao Mungu alizisamehe dhambi, hebu tuone alisamehe dhambi ngapi. Picha ndogo iliyo hapa chini itakufanya ulione jambo hilo kwa urahisi.




Picha hii inaonyesha dhambi zote zilizowahi kutendwa wakati wote wa historia ya mwanadamu kutoka wakati wa "Uumbaji" hadi "Kurudi kwa Kristo." Tunajua kwamba kuna wakati fulani hapo kale wakati dhambi ya kwanza ilitendwa na Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni, na tunajua kwamba kutakuwa na wakati katika siku za usoni ambapo dhambi zitaisha. Kuna maoni mengi kuhusu vile "mwisho" unafanana, lakini kwa ajili ya majadiliano yetu tutasema tu kutakuwa na mwisho na watu wataacha kutenda dhambi. Hii ina maana kwamba kuna idadi iliyo na kikomo ya dhambi zilizotendwa kwa muda ambao wanadamu wameishi. Idadi hiyo ni kubwa, lakini ina kikomo kwa sababu kulikuwa na mwanzo na kutakuwa na mwisho.

Tutaendelea kusoma kitabu cha Waebrania kujua ni dhambi ngapi zilisamehewa na Mungu. Waebrania 10:11-12 inasema,

> Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi. Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu.

Vifungu hivi vinaeleza wazi kwamba chini ya Agano la Kale dhabihu zilizotolewa hazikuweza kuondoa dhambi. Lakini, kinyume na dhabihu hizo, Yesu alijitoa mwenyewe kama dhabihu moja ya dhambi za nyakati zote! Hii inamaanisha kwamba dhabihu ya Yesu ilitosha kuziondoa dhambi zote zilizowahi kutendwa kuanzia mwanzo wa dunia hadi mwisho. Hii ndiyo maana mwandishi wa Waebrania anasema kwamba Yesu alipata "ukombozi wa milele" (Ebr. 9:12). Mungu alizisamehe dhambi milele!

Ukombozi ni njia nyingine ya kusema msamaha wa dhambi. Paulo alisema, "Ndani yake tunao ukombozi kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake" (Efe. 1:7 NEN), tena, "ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi" (Kol. 1:14). Kusema Mungu ametukomboa kuna maana kwamba amezisamehe dhambi zetu. Neno ukombozi lina maana ya "kukinunua kitu" au "kukimiliki kitu baada ya kulipa gharama." Hii ina maana kwamba Mungu alitununua ili ayamiliki maisha yetu. Wakati Yesu alimwaga damu yake na kufa msalabani, alilipa gharama iliyohitajika kwa Mungu kutununua (Matendo 20:28; Ufu. 5:9). Umwagaji wa damu Yake ulidhamini msamaha wa dhambi s (Ebr. 9:22). Malipo kamili yametolewa kwa hivyo dhambi zote zimesamehewa.

Huu ni ufafanuzi mzuri sana wa kile ambacho Mungu amefanya kwa tendo moja la Yesu kujitoa kama dhabihu iliyo kamili. Katika tendo hili moja la utiifu lililofanywa na Yesu, Mungu alizisamehe dhambi zote. "Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!" (2 Kor. 9:15).

*3. Kwa vile Mungu amezisamehe dhambi zote za nyakati zote, dhambi zako zote—za kale, za sasa, na za siku za usoni—zimeshasamehewa.*

Tunajua msingi wa Mungu kuzisamehe dhambi, wakati ambao Mungu anasamehe dhambi, na ni dhambi ngapi alizozisamehe. Sasa hebu tuone dhambi zako ziko wapi katika hadithi hii. Hili linaweza

kuonekana kwamba ni dhahiri, lakini nimewaona watu wengi wakitatizika kuitumia kweli hii yenye nguvu kwa uhalisi. Hebu itazame tena picha hii.

Wewe unawakilishwa na picha ya mtu mdogo aliye na nusu duara juu ya kichwa chake. Mimi kama mchanganuzi, napenda kuifafanua picha hii kwa msamiati wa hisabati, wa seti na seti ndogo. Seti ni mkusanyiko wa vitu vilivyobainishwa vizuri. Katika hali hii, mkusanyiko wa vitu ni dhambi zote za ulimwengu zilizowahi kutendwa, zinazowakilishwa na nusu duara iliyo kubwa. Nusu duara ndogo iliyo juu ya maisha yako inaashiria mkusanyiko wa vitu vya seti nyingine inayowakilisha dhambi zote utakazotenda maishani mwako. Sasa kwa uzuri wa hisabati. Ufafanuzi wa seti ndogo ni, seti ambayo mkusanyiko wake wa vitu, pia ni sehemu ya seti nyingine. Na kile kinachohusu seti pia kinahusu seti ndogo.

Kutokana na hisabati tunafikia hitimisho kwamba kwa vile Mungu alizisamehe dhambi zote—seti—za nyakati zote, pia alizisamehe dhambi zetu—seti ndogo—za nyakati zote. Hauhitaji kushangaa, kuwa na wasiwasi, au kuwa na matarajio kwamba dhambi zako zimesamehewa. Mungu alizisamehe Yesu alipokufa msalabani.

*4. Sisi kama Wakristo, hakuna tunachotakiwa kufanya ili kupata msamaha wa Mungu kwa sababu ni kitu ambacho tayari amekifanya.*

Kadri ninavyoshiriki zaidi kweli hii na Wakristo, ndivyo ninavyogundua zaidi kwamba kuna waumini wengi wanaofikiri bado kuna kitu fulani wanachotakiwa kufanya ili kupokea msamaha wa Mungu baada ya wao kuwa Wakristo. Wazo hili linatoka kwa mafundisho mbalimbali yanayotuathiri mwanzoni mwa maisha yetu ya Kikristo. Watu wengine hudhani msamaha wa Mungu unategemea hisia zao. Wanaweza tu kupokea msamaha wa Mungu kiasi cha wao kuhisi kwamba amewasamehe. Kwa mfano, wengine hudhani kwamba wakihisi wana hatia na wanasikitika ya kutosha kwa ajili ya dhambi zao, basi Mungu atawasamehe upesi sana. Wao hudhani kusamehewa kwao kunategemea huzuni au toba yao ya kweli.

Wengine wanaweza kuhisi kwamba ukubwa wa dhambi zao unaweza kuamua ni wakati gani wanaweza kutarajia msamaha. Ikiwa dhambi hiyo ni "mbaya" sana basi itabidi wangoje muda fulani kabla ya kuhisi kuwa Mungu amewasamehe. Aina hii ya imani huwafanya Wakristo waunde viwango vya dhambi, na dhambi ikiwa mbaya zaidi basi itawabidi wahisi vibaya kwa muda mrefu zaidi kabla ya kuhisi wamesamehewa.

Watu wengine hata huamini kwamba dhambi zao huwatenganisha na Mungu. Wazo hili ndilo lilifanya kanisa la Katholiki kuanzisha kile wanachokiita "dhambi saba mbaya zaidi." Wao wanaamini kwamba dhambi hizo ni mbaya sana kiasi cha kumwondoa mtu katika neema ya Mungu. Wao wanafunza kwamba dhambi za tamaa, ulafi, uroho, uzembe, ghadhabu, wivu, na majivuno ndizo dhambi mbaya zaidi kwa mtu kuzitenda na zina uwezo wa kusababisha mtu apate adhabu kali zaidi, hivyo kumfanya mtu atakiwe kuungama ili aweze tena kuunganishwa na Mungu.

Imani za aina hii zimekita mizizi katika fikira za Agano la Kale zinazosema kwamba hatuwezi kuwa na hakika kwamba tumesamehewa dhambi zetu kwa sababu kila mara kuna "kumbukumbu la dhambi" (Ebr. 10:3). Lakini kweli ni kuwa Mungu tayari amezisamehe dhambi zote, kwa hivyo hakuna chochote tunachotakiwa kufanya ili kupata msamaha Wake wala hakuna kitu tunachoweza kufanya kuupata. (Nitaeleza kinagaubaga mengi kuhusu jambo hili katika sura inayofuata hii inayohusu Kukiri.) Msamaha ni kitu ambacho tayari amekifanya. Mungu anataka tuwe na hakikisho kamili kwamba tumesamehewa kabisa. Anataka tuwe salama na tuwe na hakika ili tuweze kufurahia ushirika wa siku zote naye, haijalishi tunachofanya. Tukihisi kwamba Mungu yuko mbali sana tunapotenda dhambi, hili hukatisha tamaa zaidi na lina madhara kwa uhusiano wetu naye. Mungu anataka tujue kwamba tumesamehewa ili wakati tunatenda dhambi "tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa " (Ebr. 4:16).

Mitume wanasaidia kubainisha jinsi msamaha hufanya kazi katika maisha ya muumini. Petro na Paulo wote walitamka kauli sawa kuhusu msamaha katika mahubiri yao kwenye kitabu cha Matendo. Petro alisema katika Matendo 10:43 (NEN), "Manabii wote walishuhudia juu yake kwamba kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika Jina lake " Paul akasema katika Matendo13:38-39 (NEN):

> "Kwa hiyo ndugu zangu, nataka ninyi mjue kwamba kwa kupitia huyu Yesu msamaha wa dhambi unatangazwa kwenu. Kwa kupitia yeye, kila mtu amwaminiye anahesabiwa haki kwa kila kitu ambacho asingeweza kuhesabiwa haki kwa sheria ya Mose."

Katika hotuba hizo mbili kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kuamini na kupokea msamaha wa dhambi. Petro na Paulo walielewa kwamba Mungu alikuwa amezisamehe dhambi zote, na kazi yao ilikuwa kutangaza msamaha wa dhambi popote walipoenda. Hii ndiyo maana ya kuhuburi injili. Tunawaambia watu habari njema! Tunawaambia kwamba dhambi zao tayari zimesamehewa. Habari njema ni kwamba Mungu amewasamehe katika Kristo. Ili kupokea msamaha Wake, wanachotakiwa tu kufanya ni kuamini.

Yesu alisema, "Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu" (Yohana 3:18). Hii ndiyo njia ya Yesu kusema kile ambacho Petro na Paulo walisema. Tukiamini, sisi binafsi tutapokea msamaha wa dhambi zetu na hatutapata hukumu. Tusipoamini, sisi binafsi hatutapokea msamaha wa dhambi zetu na hatimaye tutapata kuhukumiwa. Hii ni njia nyingine ya kulisema hili. Mbinguni (milele na Mungu) kutajaa watu waliosamehewa ambao waliamini, na jehanamu (kutenganishwa na Mungu) itajaa watu waliosamehewa waliokosa kuamini! Hatutahukumiwa kwa kutegemea dhambi zetu. Mungu amezisamehe zote. Tutahukumiwa kulingana na vile tuna imani au la

Msamaha ni mada inayojitokeza mara chache sana katika barua za mitume za Agano Jipya. Naamini sababu ya hilo ni dhahiri kwa ajili ya kile ambacho nimeshiriki katika sura hii. Mitume walijua kweli kwamba msamaha wa Mungu wa dhambi ulikuwa umemalizikia msalabani. Wanapozungumza kuhusu msamaha wa dhambi, wanafanya hivyo kwa wakati uliopita (Efe. 4:32; Kol. 2:13; 3:13; I Yohana 2:12), au ni kitu tulichonacho tayari (Efe. 1:7; Kol. 1:14).ol. 1:14).

Paulo alitaja tu msamaha mara moja katika Warumi aliponukuu Daudi kutoka Zaburi 32:1 aliposema,

> "Heri waliosamehewa
> makosa yao,
> Na waliositiriwa
> dhambi zao.
> Heri mtu yule ambaye
> Bwana hamhesabii dhambi" (Rom. 4:7-8).

La sivyo, Paulo hakutaja msamaha wa Mungu wa dhambi mahali pengine katika Warumi au katika 1 & 2 Wakorintho, Wagalatia, Wafilipi, 1 & 2 Wathesalonike, 1 & 2 Timotheo, Tito, na Filemoni. Petro hakutaja msamaha katika 1 & 2 Petro. Katika vitabu vinne alivyoandika Yohana, 1, 2, & 3 Yohana na Ufunuo, alitaja msamaha mara mbili pekee (1 Yohana 1:9; 2:12); na Yakobo alitaja msamaha mara moja pekee (Yakobo 5:15).

Mitume hawakuendelea kuzungumza kuhusu msamaha kwa sababu walijua ulikuwa umeshafanyika. Walijua kwamba tukishapokea msamaha wa ajabu wa Mungu tunaweza kuishi tukiwa huru na tuendelee kuchunguza zaidi sisi ni nani katika Kristo.

*5. Dhabihu ya Yesu na msamaha wa dhambi zetu vinaondoa hali ya kujiona kwamba tuna dhambi.*

Kila mara mimi huhuzunishwa na jinsi waumini wengi wanafahamu dhambi zao kupita kiasi. Mimi huiita hali hii kujiona una dhambi (Ebr. 10:2). Kama Wakristo wengi wangekuwa wasema kweli, wangesema kwamba ni kweli wana dhambi maishani mwao na kwamba wao hufikiria juu ya dhambi hiyo mara nyingi. Kwa kweli, wao hujawa na mawazo kuhusu dhambi hiyo. Wao huzingatia dhambi yao kila mara kwa sababu wanataka kufanya kila wawezalo kujinasua kutoka kwa dhambi hiyo na kukosa kuifanya tena, au wanayumbayumba na wamebeba mzigo huo pamoja na hatia ya dhambi waliyofanya. Kwa hali yote ile wao huishia kuifikiria sana. Watu wengi huzingatia kutotenda dhambi, wakiamini kwamba wasipofanya hivyo wataishia kutenda dhambi wanayojitahidi sana kutoitenda!

Waebrania 9:9 (NEN) inatwambia kwamba sadaka na dhabihu zilizotolewa chini ya Agano la Kale hazikuweza "kusafisha dhamiri ya mtu anayeabudu." Dhabihu zilizotolewa chini ya Agano la Kale zingekoma ikiwa zingeweza kuwasafisha wanaoabudu, na kama wangesafishwa "wasingejiona tena kuwa na dhambi" (Ebr. 10:2 NEN). Badala yake, dhabihu walizotoa "zilikuwa ukumbusho wa dhambi kila mwaka" (Ebr. 10:3 NEN). Kuishi hivi kulikuwa mzigo mkubwa. Lakini habari njema ni kwamba dhabihu moja kamili ya Yesu ilimaliza hali ya kuendelea kutoa dhabihu zilizokuwa ukumbusho wa dhambi zao. Na dhabihu Yake ilimaliza hali ya sisi kuendelea kukumbushwa dhambi zetu.

Dhamiri yetu ikisafishwa haimaanishi tupuuze dhambi ndani ya maisha yetu. Tunapaswa kutembea kama watoto wa Nuru kila mara "mkihakiki ni nini impendezayo Bwana" (Efe. 5:10, 1 The. 4:1). Jambo muhimu ni kwamba tunapokosea hatuhitaji kubeba hatia na utambuzi wa makosa yetu. Huenda kukawa na athari ya kawaida inayotukumbusha, lakini hakuna tunachoweza kufanya kuhusu jambo hilo. Hata hivyo, katika uhusiano wetu na Mungu, yeye hakumbuki dhambi zetu na hataki hata sisi tuzikumbuke. Hii ndiyo mojawapo ya ukweli mzuri kuhusu dhabihu ya Yesu. Tumesamehewa kabisa na damu ya Yesu imeondoa hisia zetu za dhambi.

Katika kiwango halisi, watu wengi huzifahamu dhambi walizotenda zamani. Huwa hatuketi chini na kufikiria juu ya dhambi tutakazotenda siku za usoni, iwe ni leo, wiki mbili zijazo, au miaka kumi ijayo. Sisi huweka ndani ya dhamiri zetu mambo tuliyofanya zamani, na Mungu anataka kutuweka huru kutokana na ufahamu wa makosa hayo. Msamaha wake umetuweka huru kabisa na tunaweza kufurahia uhuru wetu bila hatia au aibu yoyote. Hii ni njia inayoelekea kwa uzima tele: Kweli ni kwamba Mungu amezisamehe dhambi zetu zote na tukijua kwamba tumesamehewa kabisa, hilo linatuweka huru na hatutafikiria juu ya dhambi zetu kila mara. Katika safari yangu binafsi, hili lilikuwa mojawapo ya mambo magumu kwangu kukubali kwa sababu kila kitu katika nia yangu kiliniambia kwamba hii haikuwa kweli. Lakini kupitia utaratibu wa kukubali kweli hii, kuiamini, na kufanywa upya katika roho ya nia yangu, nimepata uhuru wa kiwango kikubwa. Hii ni njia ya ajabu ya kuyaishi maisha na nina shauku ya kushiriki na watu wengine kweli hii kila nipatapo nafasi.

Kipengele halisi cha mwisho kuhusu msamaha kinafaa kabla ya kumaliza sura hii. Utakumbuka kwamba tangu mwanzo wa kitabu hiki lengo langu limekuwa juu ya kweli ya msingi inayotegemea kabisa kile ambacho Mungu ametufanyia kupitia kwa Yesu Kristo.Lakini majadiliano yoyote kuhusu msamaha hayawezi kuwa kamili bila kutaja umuhimu wa kuwasamehe wengine wanapotukosea na kuwaomba wengine watusamehe tunapowakosea. Paulo alisema wazi kwamba tunapaswa kusameheana, "kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi" (Efe. 4:32; Col. 3:13). Mtazamo wa Paulo hapa unaashiria kweli hii kwamba kwa vile Mungu ametusamehe bure katika Kristo, tunapaswa kusameheana vivyo hivyo. Nimegundua kwamba watu wanapoelewa kabisa msamaha wa Mungu katika maisha yao, ni rahisi kuwasamehe wengine.

Tunajua kwamba kuna athari mbaya za kutosamehe katika maisha yetu kama vile: machungu, kuhukumu, na hata magonjwa ya mwili, lakini Mungu hakosi kutusamehe! Ili Mungu afanye hivyo itabidi apuuze damu ya Mwanawe iliyomwagwa na agano alilofanya na Yeye, na hili ni jambo ambalo hawezi kufanya kamwe.

Huu ni wakati mzuri wa kujadili tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Tayari nimegusia maagano hayo mawili, lakini ningependa kuingia kwa kina zaidi kwa sababu ni muhimu kwa ufahamu wetu kuhusu msamaha, na vilevile sehemu nyingi za uhusiano wetu na Mungu.

Nafikiri waumini wengi hung'ang'ana katika uhusiano wao na Mungu kwa sababu wao huwa na mguu mmoja ndani ya Agano Jipya huku mguu mwingine ukiwa ndani ya Agano la Kale. Hili huleta matatizo makubwa katika mfumo wao wa imani, ambayo huathiri moja kwa moja vile tunahusiana na Mungu.

Agano Jipya linawakilisha njia mpya na yenye uhai iliyoanzishwa na Mungu kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo. Wakristo wengi ninaozungumza nao hukubali kwamba kuna Agano Jipya. Hata hivyo, mambo hukosa kuwa dhahiri kidogo unapoendelea zaidi ukitaka kujua ufahamu wao kuhusu tofauti iliyoko kati ya maagano hayo mawili.

Hebu tuangalie tofauti zilizoko kati ya maagano hayo mawili kulingana na waandishi wa Biblia. Agano la Kale lilitegemea andiko la sheria, lakini Agano Jipya lilitegmea Roho (2 Kor. 3:6).Agano la Kale la andiko huua na ni huduma ya mauti, lakini Agano Jipya la Roho huleta uzima (2 Kor. 3:6). Agano la Kale halikukosa kasoro na lilihitaji Agano Jipya linalofaa (Ebr. 8:7). Agano Jipya lililifanya Agano la Kale kuwa kuukuu (Ebr. 8:13). Dhabihu za Agano la Kale hazingeweza kuondoa dhambi (Ebr. 10:4, 11), lakini damu ya Agano Jipya (Mat. 26:28) inaondoa dhambi (1 Yohana 3:5). Agano la Kale lilitegemea matendo ya sheria, na Agano Jipya linategemea neema inayofanya kazi kwa njia ya imani (Gal. 3:5). Agano la Kale lilitegemea masharti ya sheria ambayo Musa alipewa na Agano Jipya linategemea neema na kweli iliyodhihirishwa ndani ya Yesu Kristo (Yohana 1:17).

Agano Jipya lilianza Yesu Kristo alipomwaga damu yake msalabani. Hii inamaanisha kwamba Yesu alipokuwa hai hapa duniani alikuwa anaishi chini ya Agano la Kale. Alikuwako "kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria" (Gal. 4:4-5). Yesu mwenyewa alisema, "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Mat. 15:24). Tunajua kutoka kwa hadithi yote kwamba wokovu ulikuwa wa ulimwengu mzima, lakini Yesu alipokuwa hapa duniani alikuwa akiwazingatia Wayahudi. Yesu aliingiliana na Wayahudi sanasana kama Masihi aliyeahidiwa kwa Wayahudi , wakati wa huduma yake ya miaka mitatu. Tumerekodiwa kipindi hiki katika vitabu vinne vya injili—Mathayo, Marko, Luka, na Yohana.

Ni muhimu tuelewe kwamba waandishi wa injili walikuwa wakirekodi matukio ya maisha ya Yesu alipokuwa duniani kabla ya Agano Jipya kuanza kufanya kazi. Alifunza kama Myahudi aliyekuwa chini ya Sheria, kwa wale waliokuwa chini ya Sheria. Yote ambayo Yesu aliwaambia Wayahudi wakati wa huduma Yake hapa duniani yalionyesha yale yaliyokuwa kweli chini ya Agano la Kale.

Mengi ya mambo yaliyorekodiwa katika vitabu vya injili ni mambo aliyofanya Yesu miongoni mwa Wayahudi. Kuna mara chache tu ambapo anazungumza na MataifaMwanamke aliyekuwa kisimani alikuwa Msamaria (Yohana 4) na mwanamke Mkanaani alikuwa wa Mataifa (Mat. 15:21-28; Marko 7:24-30). Yesu alimponya pia mtumishi wa Jemadari wa Kirumi (Luka 7:2-10) na mwana wa afisa wa mfalme (Yohana 4:46-54). Matukio haya yote yanaonyesha hali ambazo Yesu alionyesha huruma na kudhihirisha nguvu zake za miujiza kuponya au kutoa unabii. Hata hivyo, wakati wa kufunza na kutoa maagizo, pasipo kwa mwanamke aliyekuwa kisimani aliponena naye kuhusu ibada ya kweli, Yesu aliwafunza tu Wayahudi na kuwapa maagizo. Lazima kila mara tulikumbuke hili tunaposoma vitabu vya injili na kutaka kuelewa kweli katika yale ambayo Yesu alikuwa akiwaambia wasikilizaji wake waliokuwa Wayahudi. Kisha tunaweza kutambua jinsi inatumika kwetu chini ya Agano Jipya.

Mtazamo huu ni wa msingi katika usomaji wa Biblia na ufafanuzi wa Maandiko ulio mzuri na wa kuwajibika. Kuyatumia Maandiko nje ya muktadha wake kumeleta matokeo mabaya kotekote katika

historia ya Kanisa. Hatutaki kufanya kosa hilo hilo. Hata hivyo, watu wengi bado wanataka kutumia mafunzo ya Yesu chini ya Agano la Kale na kuyatumia katika Agano Jipya. Hili litaleta madhara makubwa. Tunatakiwa kuwa na tumaini la kutosha katika uhalisi wa Agano Jipya kukubali kwamba hata yale ambayo Yesu anasema chini ya Agano la Kale hayatumiki kwa watu wanaoishi katika Agano Jipya-na hata wewe.

Hata Yesu alikuwa anajua mambo ambayo yangetokea baada ya Agano Jipya kuanzishwa, lakini hakuyanena kwa ukamilifu kabla ya mambo hayo kufanyika. Alijua mambo yangebadilika tu baada ya Yeye kukamilisha alichokuwa amekuja kukifanya kupitia kifo chake, kuzikwa na kufufuka.

Hii haimaanishi kwamba Maandiko yaliyo na mafunzo ya Yesu hayakutolewa na Roho! Inamaanisha kwamba yana mahali pake panapofaa katika kufahamu utaratibu kamili wa Mungu kwenye historia. Tunajifunza kuhusu hulka na nafsi ya kweli ya Mungu kupitia vile Yesu alihusiana na watu kwa huruma na upendo. Alijawa "neema na kweli" (Yohana 1:14) naye alikuwa mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi yake (Ebr. 1:3).

Mtazamo huu unatusaidia kulinganisha kile Yesu alifunza kuhusu msamaha katika "Sala ya Bwana." Yesu alisema kwamba tunapaswa kumwomba Mungu atusamehe makosa yetu kama tunavyowasamehe wengine na kwamba "msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu" (Mat. 6:9-14). Kuishi hivi kunaogofya sana. Kunaweka sharti kali kwa msamaha ambalo wengi wetu hatuwezi kulitimiza. Lakini lazima tufahamu kwamba kwa Myahudi sharti la aina hii lilikuwa limekita mizizi ndani ya ufahamu wao kuhusu vile Mungu alihusiana nao. Myahudi hangeshangaa kusikia Yesu akieleza msamaha kwa njia hii. Hata hivyo, hili si sharti linaloingizwa katika Agano Jipya. Hakuna sharti kwa msamaha katika mafunzo ya mitume ya Agano Jipya. (Tutaliangalia jambo hili kinagaubaga katika sura inayofuata ya Kukiri.)

Msamaha ni kipawa cha bure kutoka kwa Mungu kwa ulimwengu mzima kwa ajili ya kile Yesu alifanya msalabani. Yeyote aaminiye, atapokea msamaha (Matendo 10:43; 13:39). Chini ya Agano Jipya msamaha unategemea damu ya Yesu iliyomwagika!

Mungu anajua kwamba katika maisha haya tutaweza kutenda dhambi, na ni kwa ajili hii ndiyo ametupatia msamaha. Haiwezekani kutenda dhambi zinazozidi msamaha wa Mungu! Na papo hapo mtu atauliza swali hili, "Je, utasemaje kuhusu dhambi isiyosamehewa?" Yesu alisema,

> "Amin, nawaambia, Dhambi zote watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote; bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele" (Marko 3:28-29; Mat. 12:31-32).

Kama tutakavyoona katika Sura ya 10, kazi ya Roho Mtakatifu ni kuwasadikisha watu wasio Wakristo kuhusu dhambi yao ya kutoamini. Wakisikia na kukubaliana na Roho, wawe na imani na wakiri, watapokea msamaha. Wakipuuza kusadikisha kwa Roho—hii ndiyo maana ya kumkufuru Roho—hawawezi kupokea msamaha kwa sababu hawaamini. Ndiyo maana dhambi ya kutoamini haiwezi kusamehewa. Mungu anatafuta imani na anatupa uhuru wa kuchagua.

Sisi kama wana wa Mungu, tunaendelea kufurahia msamaha wa Mungu. Ni kitu ambacho kila mara kiko maishani mwetu. Haijalishi tunachofanya, tayari tumesamehewa. Kwa kweli, hatuwezi kukosa kusamehewa.

Najua kuna vile utaitikia mara moja unaposikia kweli hii kwa mara ya kwanza. Huenda ukasema, "Siwezi tu kutenda dhambi nitakavyo na Mungu anisamehe kila mara." Kweli ni kwamba unaweza na tayari Yeye amefanya hivyo. Ingawa kweli hii ni nzuri sana, ni sehemu moja tu ya kweli yote. Bado kuna sehemu nyingine inayomwelekeza mtu kupata mgeuzo mkuu na uhuru wa kweli unapopata ushindi dhidi ya mielekeo ya dhambi. (Tutajadili kweli hii katika Sura ya 8 kuhusu Dhambi.) Kwa sasa, kweli

hii ymuhimu sana inayohusu msamaha inahitaji kukita mizizi ndani ya fikira zako unapoiamini kwa imani. Ingawa inaweza kusikika kuwa nzuri kupita kiasi, ni kweli kabisa. Unatakiwa kuwa na imani yenye ujasiri kuamini kile Mungu anakwambia kuhusu msamaha Wake ili uweze kufurahia makuu ambayo amekutendea kupitia Yesu Kristo.

*Kupata Kweli*

**Kweli:** Yesu alipokufa msalabani, Mungu alizisamehe dhambi zote za nyakati zote; kwa hivyo, dhambi zako zote-za kale, za sasa, na za siku za usoni- zimesamehewa.

**Tamko la Imani:** Dhambi zangu zote zimesamehewa na ninaweza kuishi katika uhuru na imani kamili na Mungu. Nitasongea kiti cha neema kwa matumaini kupokea rehema na kupata neema ya kunisaidia nikiw**a na hitaji.**

*Kuenenda Katika Kweli*

Anza kila siku kwa kumshukuru Mungu kwa kazi yake kamili ya msamaha kupitia kwa damu ya Yesu iliyomwagika. Amini kwamba dhambi zako zote-za kale, za sasa, na za siku za usoni- zilisamehewa msalabani. Unapofanya kitu unachoamini ni dhambi, mshukuru Mungu kwa msamaha Wake na amini kwamba anataka usonge karibu naye. Ikiwa unasumbuliwa na hali ya kuifahamu dhambi yako, kiri na uamini kweli ya msamaha wa Mungu na damu ya Yesu katika maisha yako. Hataki uishi ukiwa na hatia na hukumu.

# 7

# KUUNGAMA

*Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*

*~ 1 Yohana 1:9*

*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.*

*~ Yakobo 5:16*

Thomas Dewar alikuwa Lodi wa Skoti na mtonesha wa wiski ya Skoti karne ya ishirini ilipoanza. Alinukuliwa akisema, , "Kuungama kwa kweli ni jambo zuri kwa nafsi, lakini baya kwa sifa ." Ni kisa cha kuchekesha kinachofichua athari ya kuungama kwa muda mrefu. Historia ya kuungama ndani ya kanisa ni ya ajabu iliyoathiriwa sanasana na desturi za Wakatholiki wa Roma na ilianza takriban karne ya 5 kisha ikawa desturi ya kawaida katika karne ya 11. Uamuzi wa Baraza la nne la Laterani katika mwaka wa 1215 ulianzisha kanuni ya kwamba kila Mkristo anapaswa kuungama kwa kasisi angalau mara moja kwa mwaka.

Desturi ya kawaida ya kuungama ndani ya kanisa hailingani kabisa na kile Biblia inafunza kuhusu kuungama. Katika Agano la Kale kuungama dhambi kunatajwa mara chache tu. Katika Sheria ya Musa, kuna tukio moja ambapo anayeabudu "ndipo atakapoliungama jambo hilo alilolikosa" (Lawi. 5:5; Hes. 5:7). Haruni anaagizwa aweke mikono yake miwili juu ya kichwa cha mbuzi na "kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli" (Lawi. 16:21). Na mara mbili katika Zaburi, Daudi anataja kuungama upotovu na dhambi zake (Zaburi 32:5; 38:18).

Neno la Kigiriki la "ungama" ni homologeo. Hili ni neno ambatani lililo na maneno mawili homo na logeo. Homo ina maana ya "-a jinsi moja" na logeo ina maana ya "kunena." Likiunganishwa pamoja neno hilo lina maana ya "kunena kwa jinsi moja." Kuungama ni njia ya kuja katika makubaliano na Bwana na kunena kwa jinsi moja naye. Mara nyingi waandishi wa Agano Jipya hutumia neno kuungama

kimsingi kama tamko au kutangaza. Wanatuhimiza kumkiri Yesu mbele ya watu (Mat. 10:32), kumkiri Yesu kama Bwana (Rum. 10:9), kumkiri Mwana (1 Yohana 2:23), na kukiri kwamba Yesu Kristo alikuja katika mwili (1 John 4:2). Inaweza kumshangaza mtu kwamba kuna mifano michache sana katika Agano Jipya inayotaja kuungama dhambi. Mifano miwili iko katika vitabu vya injili na miwili iko katika nyaraka.

Mathayo na Marko wanatwambia kwamba Wayahudi walikuja kwa Yohana Mbatizaji kando ya mto wa Yordani awabatize "huku wakiziungama dhambi zao" (Mat. 3:5; Marko 1:5). Kuungama dhambi ambako Wayahudi walifanya hakukuhusiana na wokovu na kukubali kile ambacho Yesu alifanya msalabani. Hii ilikuwa miaka kadhaa kabla ya msalaba. Bila shaka kuungama huko hakukuhusiana na wokovu. Tutakuwa tumekosea tukisema kwamba kuungama ambako Wayahudi walifanya kando ya mto wa Yordani ni mfano wa kuwaelekeza Wakristo. Kuungama dhambi kwa Wayahudi kuliunganishwa na njia ya desturi, ya utaratibu ambayo Wayahudi waliijua vizuri sana wakati huo.

Nyaraka za Agano Jipya zimetumika kama chanzo cha maagizo na desturi kwa Wakristo kwa miaka 2000 iliyopita. Kuna waandishi sita waliobandika nyaraka ishirini na moja kwa makanisa. Katika nyaraka hizo, Paulo, Petro, Yuda, na waandishi wa Waebrania hawakutaja kuungama dhambi. Yohana na Yakobo walitaja kuungama dhambi mara moja (1 Yohana 1:9 na Yakobo 5:16).

Yakobo 5:16 anaeleza wazi. Anatwambia "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa." Jambo tunalotambua kuwa wazi katika kifungu hiki ni kwamba tunaambiwa tuungame dhambi zetu sisi kwa sisi. Huku si kuziungama dhambi zetu kwa Mungu. Yakobo alituhimiza tufanye hilo, lakini ni kitu kigumu sana kukifanya. Mara nyingi huwa ni vigumu kunyenyekea na kuleta dhambi zetu katika nuru. Hata hivyo, ni mazoea mazuri, na Yakobo alitwambia tukiungama dhambi zetu sisi kwa sisi na kuombeana, tutapata uponyaji.

Ni muhimu kujua kwamba Yakobo alikuwa anashughulikia hali ya maisha ya ushirika ndani ya kanisa. Maisha ya ushirika yanahusu namna ya kuingiliana na pia kuhusiana na wengine katika mwili wa Kristo. Aliuliza swali hili, "Vita vyatoka wapi, na mapigano yaliyoko kati yenu yatoka wapi?" (Yakobo 4:1). Aliendelea kuzungumza juu ya sababu mbalimbali za kuwa na matatizo katika kanisa alililoliandikia barua. Hasa aligusia vile walikuwa wakineneana mabaya wao kwa wao ndani ya kanisa (Yakobo 4:1 1). Haya yote yalielekea kwa hitimisho lake katika sura ya tano alipowahimiza waungame dhambi zao wao kwa wao. Ugomvi wao na vita vilikuwa vimesababisha mateso ya kiroho na kimwili. Yakobo hakuwa akizungumzia dhambi za mtu binafsi kama vile kudanganya, uzinzi, na ulevi. Alikuwa akizungumza kuhusu dhambi zilizokuwa ndani ya kanisa kama vile migawanyiko, ugomvi, na wivu. Hizi ni dhambi za kumhuzunisha Mungu kwa sababu Mungu ni Mmoja (Efe. 4:4-6), naye anapenda umoja. Umoja huo ukivunjika kwa njia ya migawanyiko na ugomvi mwili Wake huumia (1 Kor. 1:10-13; 3:3; 2 Kor. 1 2:20). Yakobo alikuwa anatusaidia kuelewa kwamba iwapo mambo haya yatafanyika tunapaswa kuungama sisi kwa sisi ili sote tuweze kuponywa na kurejeshwa katika hali ya kuwa na umoja.

Yakobo alikuwa anaelezea kweli muhimu sana kuhusu jinsi tunapaswa kuhusiana sisi kwa sisi katika mwili wa Kristo. Tunang'ang'ana kuelewa na kuwa na aina hii ya mahusiano kwa sababu kadhaa. Kwanza, sisi ni watu wenye nia ya ubinafsi. Kila mmoja wetu ana uhusiano wake mwenyewe na Bwana, lakini hilo hufanyika katika mazingira ya mwili wa Kristo ulio na sehemu nyingi na sisi ni sehemu moja tu (1 Kor. 12:12; 14). Uhusiano wetu na Mungu ni wa mtu mwenyewe, bali si wako binafsi. Yakobo alikuwa anatusaidia kuelewa umuhimu wa kuungama katika mazingira ya mwili wa ushirika na vile kuungama kunaathiri kila mmoja wetu. Hii ndiyo maana katika Yakobo 5:15-16 alitumia viwakilishi vya hali ya umoja na hali ya wingi katika mazungumzo yake. Waliokuwa wanaumia katika mwili wangepata uponyaji walipoungama dhambi wao kwa wao. Washirika katika mwili wa Bwana wangemsamahe

yeyote ambaye alikuwa amekosa.

Alisema,

> Je, kuna yeyote miongoni mwenu aliye mgonjwa? Basi inampasa awaite wazee wa kanisa wamwombee na kumpaka mafuta kwa Jina la Bwana. Kule kuomba kwa imani kutamwokoa huyo mgonjwa, naye Bwana atamwinua na kama ametenda dhambi, atasamehewa (Yak 5:14-15). (NEN)

Fahamu Yakobo hakushuku ikiwa dhambi za mtu huyu zingesamehewa. Alitambua kwamba washirika wengine wangeitikia hivyo kwa vile tayari walielewa walikuwa wamesamehewa na Mungu na kwamba wangepaswa pia kuwasamehe wengine jinsi walivyosamehwa na Kristo (Efe. 4:32; Col. 3:13).

Pia, maisha ya kanisani katika Agano Jipya yalikuwa tofauti na yalivyo sasa. Kanisa lilifanyiwa nyumbani na mara nyingi katika makundi madogo ya waumini walioendesha mambo ya imani yao kwa hali ya kupenda wao kwa wao. Kanisa halikuwa kama la siku hizi ambapo unakuja, unashiriki katika ibada, kisha unaenda nyumbani. Mara nyingi, huwa hatuingiliani sana na wengine. Haikuwa hivi katika makanisa ya Agano Jipya. Tatizo lilipotokea miongoni mwa waumini, liliathiri washirika kwa kiwango kikubwa. Ndiyo maana Yakobo akazungumza kuhusu umuhimu wa kutembea pamoja kwa njia ya uwazi na unyenyekevu. Umoja na amani katika mwili vilikuwa vitu halisi sana na vya lazima ili mwili wa kiroho uendelea kuwa na afya. Jambo hilo ni kweli hata sasa.

Hii inabakisha 1 Yoh 1:9 kama kifungu pekee katika nyaraka zote kinachozungumza juu ya kuungama dhambi. Katika kifungu hiki Yohana alisema, “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” Hiki ndicho kifungu kinachotumiwa sana na mtu yeyote anayewafundisha waumini kwamba kuna haja ya kuungama dhambi zao ili wasamehewe. Lakini je, Yohana alikuwa akilifunza jambo hilo? Muktadha wa waraka wa Yohana utatusaidia kuelewa alichomaanisha..

Yohana alikuwa analiandikia kanisa lililokuwa limeathiriwa na mafunzo ya mwanzoni ya kundi la dini la “Gnostics” (watu waliosisitiza sana mafunzo ya falsafa). Gnosticism (mfumo uliozingatia mafunzo ya falsafa) ulikuwa mfumo wa imani ngumu kufahamika uliojaribu kudhoofisha imani ya msingi ya Ukristo. Hali moja ya “Gnosticism” hasa ni muhimu iwapo tunataka kuelewa maoni ya Yohana katika 1 Yohana 1.

Katika harakati yao ya kuelewa maovu waliyoona duniani, wana “Gnostics” walianzisha imani ya ajabu kusema kwamba watu ni nafsi za kiungu zilizonaswa ndani ya mwili wa kawaida. Waliunda mgawo wa sehemu mbili zinazokinzana kati ya maeneo ya kimwili na ya kiroho. Waliamini kwamba Mungu hakushughulika na mwili kwa sababu ulikuwa mwovu. Walihitimisha kwamba wangeweza kufanya chochote wapendacho na miili yao bila tatizo lolote. Kilichokuwa muhimu kilikuwa nafsi yenye uungu.

Imani hii iliwafanya watu wa “Gnostic” wafunze kwamba Yesu hangeweza kuwa mwanadamu aliye na mwili wa kawaida, la sivyo angekuwa mwovu. Walifunza kwamba alikuwa tu nafsi yenye uungu na “alijitokeza” kwa watu kama dhihirisho la kile alichokuwa kama roho. Wangetumia mifano kama ya Yesu kutembea juu ya maji (Mat. 14:22-27; Marko 6:47-52); Yesu alipotoweka watu walipotaka kumrusha chini ya ukingo wa kilima (Luka 4:28-30); na Yesu alipopita katika milango iliyokuwa imefungwa na kuingia katika chumba cha juu (Yohana 20:19; 26) kama thibitisho la imani yao. Unaona vile waumini wachanga wangeshawishiwa na aina hiyo ya mafundisho.

Baadhi ya hao walimu wa ‘gnostic’ walikuwa wameingia kanisani. Yohana akalishughulikia jambo hili katika 1 Yohana. Alianza waraka wake wa kwanza hivi:

> Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tulililoliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima; na uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu); hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi (1 Yoh 1:1-3a).

Tunatambua mara moja alichokuwa akisema Yohana. Bila shaka alikuwa akiwazungumzia hawa walimu wa uwongo. Kitu cha kwanza alichosema ni kwamba yeye alkuwa amemgusa Yesu kwa mikono yake mwenyewe! Haingewezekana kamwe Yohana kuamini kwamba Yesu hakuwa na mwili. Yohana ndiye alikuwa ameegema kifuani pa Yesu wakati wa chakula cha jioni cha mwisho (Yohana 13:23).

Yohana aliendelea kusema kwamba yale wao, mitume, walikuwa wameona na kusikia kutoka kwa Baba waliwatangazia, wana "Gnostic". Aliwataka wana "Gnostic" waamini kweli ili waweze pia kuwa waumini. Haya yalikuwa mahubiri mazuri sana ya kiinjilisti yaliyoelekezwa kwa walimu wa uwongo ambao hawakuamini kweli kuhusu Yesu. Hii pia ndiyo maana Yohana alisema baadaye, "Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu" (I Yoh 4:2).

Yohana aliwaambia kwamba ujumbe huu ndio yeye na watendakazi wenzake waliusikia kutoka kwa Mungu, na ndio waliowatangazia. Alitaka hawa walimu wa uwongo wasio Wakristo wafahamu namna ya kutembea katika kweli na kupokea msamaha. Ni katika muktadha huu ndio aliwaambia walimu hao wa uwongo walichopaswa kufanya.

Walitakiwa tu kufanya kile ambacho kila mtu asiye muumini anatakiwa kufanya ili kupokea msamaha. Walitakiwa kuamini, kuungama dhambi zao, na kupokea msamaha. Mungu ni mwaminifu na angewasamehe maovu yao yote kwa sababu ya agano Lake la kufanya hivyo kulingana na damu ya Yesu iliyomwagika. Hili ndilo tunalopaswa kutarajia kulingana na kile ambacho tayari tumeona katika sura iliyotangulia inayohusu msamaha. Mungu hawezi kumnyima msamaha mtu yeyote aaminiye na kukiri kweli. Hili ni jambo linalotakiwa kufanyika kwa kila mtu katika tukio lao la kupokea wokovu. Kila mtu lazima afikie kiwango cha kutambua kwamba ametenda dhambi ndani ya maisha yake na "anene kwa jinsi moja." Hii ndiyo maana ya kuungama. Wakifanya hivyo, Mungu ni mwaminifu na atawasamehe. Hakuna chochote katika kifungu hiki kinachopendekeza kwamba kuungama ni jambo linalofanyika mara tena na tena ndani ya maisha ya muumini. Kweli ni kwamba, hakuna vifungu vingine vya Maandiko katika Biblia vinavyopendekeza jambo hili kwa njia yoyote ile. Hilo lilikuwa tu wazo geni kwa mitume walioandika nyaraka za Agano Jipya.

Ukiendelea kusoma 1 Yohana, utagundua kwamba Yohana anawazingatia waumini walio kanisani katika sura ya pili. Katika 1 Yohana 2:1-2 alisema,

> Watoto wangu wapendwa, nawaandikia haya ili msitende dhambi. Lakini kama mtu yeyote akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba: ndiye Yesu Kristo, Mwenye Haki. Yeye ndiye dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, wala si kwa ajili ya dhambi zetu tu, bali pia kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote.

Angalia vile Yohana aliwaita watoto wake wadogo. Hii ilikuwa lugha ya kawaida kwa watu waliokuwa wa imani. Pia, angalia kile Yohana aliwaambia ikiwa watatenda dhambi. Yohana alisema, "kama mtu yeyote akitenda dhambi" anaye Mwombezi, Yesu Kristo, ambaye ni dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, maneno 'dhabihu ya upatanisho' yanamaanisha Yesu ameshachukua adhabu yetu na amelipia gharama ya msamaha wetu. Na Yohana alisema kwamba Yesu amefanya hivyo si kwa ajili ya dhambi zetu tu bali pia za uliwemwengu mzima! Fahamu kwamba Yohana hakuwaambia watoto wake wadogo waungame dhambi zao ili wapate kusamehewa. Hii haingeambatana na ufahamu wa mtume kuhusu msamaha na kuungama.

Haya yote yana maana gani hasa katika maisha yetu. Kuna maana kadhaa tunapoanza kuelewa kweli kuhusu kuungama. Naamini neno la kutukumbusha linafaa wakati huu. Kumbuka kitabu hiki chote kinahusu maisha ya Kikristo. Kila kitu ninachoshiriki ni cha waumini ili waweze kupata kila kitu ambacho Mungu amewatengea kama watoto Wake. Kama ilivyokuwa katika sura iliyotangulia inayohusu msamaha, ningependa kuzingatia mambo machache kuhusu kuungama, yatakayotusaidia kuelewa kwa hali halisi. Fahamu kwamba kauli hizi zote tatu zinahusu maisha ya Mkristo.

1. Wakristo hawahitaji kuungama dhambi zao ili wasamehewe.
2. Hakuna uhusiano wa sababu na matokeo kati ya kuungama na msamaha katika maisha ya Mkristo.
3. Kuamini kwamba kuungama ni lazima ili mtu asamehewe kutasababisha woga na shaka katika maisha ya Mkristo.

Hebu tuingalie kila kauli kinagaubaga.

*1. Wakristo hawahitaji kuungama dhambi zao ili wasamehewe.*

Hili ni jambo la ujasiri sana kulitamka tukizingatia kwamba kuna mafunzo mengi ya desturi ya kanisa. Lakini kabla ya kufanya uamuzi kulihusu, hebu tuzingatie tulichojifunza kufikia sasa. (katika Sura hii na Sura ya 6 inayohusu Msamaha). Kwa mujibu wa Maandiko, yeyote anayetaka kuwa Mkristo lazima aamini tu- awe na imani – katika kazi iliyokamilika ya Yesu Kristo. Ninaposema kazi iliyokamilika, ninamaanisha kifo Chake msalabani, kuzikwa kwake, na kufufuliwa kwake kutoka kwa wafu (1 Kor. 15:3-5). Sehemu ya njia hii ni pamoja na kila mtu kukubaliana na Mungu kwamba ana dhambi maishani mwake na kwamba anahitaji msamaha wa Mungu. Kumbuka kwamba kuungama kuna maana ya "kunena kwa jinsi moja." Mtu anasema tu kile ambacho Mungu tayari anajua kumhusu mtu huyo. Jambo hili linapotendeka, Yeye ni mwaminifu na atawasamehe. Yeye ni mwaminifu kufanya hilo kwa sababu msamaha Wake unategemea kile Yesu alifanya msalabani. Msamaha Wake hautegemei kitu kingine kile. Mtu huyo sasa anaingia katika uhusiano na Mungu na anakua mtoto Wake. Anapokea msamaha wa dhambi zake zote.

Iwapo umefanya niliyoeleza, basi imani yako imekuleta katika uhusiano wako mwenyewe na Mungu kupitia Yesu Kristo. Kuishi kama Mkristo maisha yako yote, unafurahia kweli kwamba umesamehewa kabisa. Hata unatenda dhambi, unajua kwamba tayari Mungu amekusamehe. Pia unajua kwamba hazikumbuki dhambi zako tena (Ebr. 10:17). Hii ndiyo maana hufunzwi mahali popote katika Maandiko uungame dhambi zako tena ukishakuwa Mkristo. Unaendelea tu kutoka kwa makosa yako ukiwa na hakika kamili ndani ya moyo wako kwamba hauhitaji kuzizingatia dhambi zako tena.

*2. Hakuna uhusiano wa sababu na matokeo kati ya kuungama na msamaha katika maisha ya Mkristo.*

Ikiwa unaamini kwamba ni sharti uungame dhambi zako ili usamehewe dhambi zako baada ya kuwa Mkristo, hujaelewa kikamilifu msamaha wa Mungu. Msamaha wa Mungu ni kamili. Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zote za nyakati zote, na alipofanya hivyo, Mungu alizisamehe dhambi zote za nyakati zote (kumbuka picha iliyo katika Sura ya 6). Mungu hana tatizo na dhambi tena. Tatizo lipo wakati unakataa kuamini kweli hii na kuzifanya dhambi zako kuwa tatizo kati yako na Mungu. Unadhani Mungu anajibu vipi unapoungama dhambi zako na kuomba msamaha? Naamini jibu lake ni "Nimeshafanya hivyo!"

Hebu nibainishe ninachosema. Sisemi kwamba huwezi kukiri dhambi zako kwa Mungu. Ningependa ijulikane kuwa ninasema, ikiwa unataka kuendelea kuungama dhambi zako, ni sawa. Nakuhimiza

usiamini kwamba lazima uungame dhambi zako ili upokee msamaha wa Mungu. Hakuna uhusiano wa sababu na matokeo kati ya kuungama na msamaha katika maisha ya Mkristo. Msamaha wake ni kipawa alichokupa ulipoamini mara ya kwanza. Kuanzia siku hiyo unatakiwa tu kufurahia kweli kwamba umesamehewa. Hakuna masharti kwa msamaha wa Mungu, kwako wewe kama mtoto Wake. Hakuna unachoweza kufanya ili kuupata msamaha wake. Hii ndiyo habari njema ya injili!

*3. Kuamini kwamba kuungama ni lazima ili mtu asamehewe kutasababisha woga na shaka katika maisha ya Mkristo.*

Utawezaje kupata matumaini na hakika kamili kwamba umesamehewa kabisa ikiwa msamaha wako unategemea kuungama kwako? Na je, ukisahau dhambi moja? Je, unahitajika kutaja kila dhambi unayotenda ili ujue Mungu amekusamehe zote? Je, unatakiwa tu kutamka ombi moja la kuungama linalofunika dhambi zozote ambazo huenda ikawa umezitenda kila siku? Au unaweza kufanya hivyo kila wiki? Je, unaona maswali haya yote yanaelekea wapi? Yanaanza kusikika kama upuuzi. Maisha ya Kikristo hayafanani hivi, na sivyo Mungu anavyotaka uishi. Ndiyo maana waandishi wa Agano Jipya hawawaambii Wakristo waungame dhambi zao. Hautakiwi kuzingatia dhambi zako na kuungama mara tena na tena kila siku. Mitume walielewa nguvu za kazi iliyokamilika ya Yesu, na walijua kwamba ilitosha kutupa msamaha, mara hiyo moja.

Kuwa huru kutokana na mzigo wa kuungama hubadilisha vile tunahusiana na Mungu. Mungu haketi mbinguni akiwa na ubao wa kuhesabu ili ahakikishe kwamba umeziungama dhambi zako zote kwake. Alimaliza suala la wewe kupokea msamaha msalabani. Usifanye kuungama kuwe sharti lingine katika uhusiano wako na Mungu. Pokea kweli hii, "na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani," na "mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu" (Ebr. 10:22-23).

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Kuziungama dhambi zako ni sehemu muhimu ya tukio lako la wakovu, lakini baada ya kupokea msamaha wa dhambi zako zote na kuwa Mkristo, kuungama si lazima kwa ajili ya kupokea msamaha wa Mungu.

**Tamko la Imani:** Mimi kama mtoto wa Mungu, sihitajiki kuungama dhambi zangu ili nisamehewe. Nimesamehewa tayari kama dhihirisho lisilo na sharti la upendo wa Mungu kwangu, alilodhihirisha msalabani wakati Yesu alimwaga damu Yake.

### *Kuenenda Katika Kweli*

Endelea kuifanya upya nia yako katika kweli hii kwamba wewe kama muumini tayari umesamehewa kabisa na Mungu. Tambua Mungu hakuwekei sharti la kuungama dhambi zako ili uweze kufurahia msamaha Wake. Ukitenda dhambi, shikilia kweli hii na umtazame Yesu, ambaye ni Mwombezi wako kwa Baba. Amini kwamba Mungu daima ataliheshimu agano alilofanya na Mwanawe kwa niaba yako. Uko huru kutokana na woga, hatia, na hukumu, na hauhitaji kuendelea kukariri makosa yako mbele za Mungu.

# 8

# DHAMBI

*"Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde."*

*~ Mwanzo 4:7b*

*Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?*

*~ Warumi 6:1-2*

Mojawapo ya kweli inayoniliwaza mno ambayo nimeijua na kuiamini sasa ni kwamba Mungu ametukirimia kila kitu tunachohitaji ili kuishi maisha ya Kikristo. Yeye hatuachi tuishi sehemu nyingine za maisha yetu ya Kikristo kwa nguvu au juhudi zetu wenyewe, halafu tung'ang'ane na tukose kufaulu na pia tuvunjike moyo. Habari nzuri zaidi ni kwamba "Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa" (2 Pet. 1:3). Hii ina maana kwamba kila kitu tunachohitaji kuishi katika ukamilifu kama waumini tumeshakirimiwa kwa kumfahamu yule aliyetuita. Hili ndilo lengo la kitabu hiki kutambua ufahamu wa kweli wa Yesu na kisha kutembea katika uhalisi wa ufahamu huo ndani ya maisha yetu. Tunapofanya hivyo, tunapata kiwango kikuu cha uhuru maishani na usalama katika uhusiano wetu na Mungu alioutaka tangua mwanzo wa wakati. Hakutuumba tuwe watu wenye kufuata dini bali tuwe katika uhusiano.

Wakati fulani katika maisha yetu sisi hung'ang'ana na dhambi. Hii kwa kawaida si mada inayopendwa sana kuzungumziwa. Lakini kama ndovu aliye chumbani, tunahitaji tu kuikubali na kuizungumzia. Labda wewe umekwama katika sehemu fulani ya dhambi, na unatafuta "mpenyo" ambao moyo wako unatamani (angalia Warumi 7:21-25). Mkondo huo unaweza kuwa wa dhambi ambayo imeyashikilia maisha yako na imekuwa "dhambi ile ituzingayo kwa upesi" (Ebr. 12:1). Pengine inaweza kuwa ni kiburi, ubinafsi, au mawazo yoyote au mienendo yenye dhambi. Ikiwa unalifahamu jambo hili, basi ninajitayarisha kushiiki nawe habari njema zaidi ambayo utawahi kuisikia!

Ungesema nini iwapo ningekukuliza, "Ni tofauti gani iliyopo kati ya dhambi (katika hali ya umoja) na dhambi (katika hali ya wingi)?" Unapolitazama mara ya kwanza unaweza kusema kwamba neno dhambi, la kwanza, liko katika umoja na neno la pili ni wingi. Hayo ndiyo majibu nipatayo kutoka kwa watu wengi ninaowauliza swali hili. Kweli ni kwamba kuna tofauti kubwa kati ya dhambi (katika hali ya umoja) na dhambi (katika hali ya wingi), na kuiona tofauti hiyo ndio ufunguo wa kwanza wa kujifunza vile unaweza kupata uhuru kamili na kamilifu kutoka kwa dhambi, katika maisha yako.

Tumeshaona kwamba kupitia kwa kazi iliyokamilika ya Yesu msalabani, tumepokea msamaha kamili wa dhambi zetu zote—za kale, za sasa, na za siku za usoni. Hii inamaanisha kwamba kila kitendo cha dhambi ambacho tumewahi kufanya au tutawahi kufanya tayari kimesamehewa. Yesu alikufa ili tupate msamaha wa "dhambi (katika hali ya wingi)." "Dhambi" hizi zote ni mambo tuyafanyayo maishani, yasiyomfurahisha Bwana, yanayofanywa katika mwili, pasipo imani, na kinyume na hulka na asili ya Mungu, Hata hivyo, "dhambi (katika hali ya umoja)" ni jambo lingine tofauti.

Hadithi ya Kaini na Abeli inatusaidia kuona tofauti iliyoko kati ya dhambi (katika hali ya umoja) na dhambi (katika hali ya wingi). Tunaijua vizuri hadithi hiyo. Kaini na Abeli walileta sadaka zao mbele za Mungu. Kaini alileta baadhi ya mazao ya shamba, na Abeli akaleta fungu nono kutoka baadhi ya wazaliwa wa kwanza wa mifugo yake. Mungu akamkubali Abeli pamoja na sadaka yake, lakini hakumkubali Kaini pamoja na sadaka yake. Alilofanya Kaini lilikuwa jambo la kawaida. kwa hali ya kawaida. Hisia zake ziliumia, akapata mtazamo fulani na na "akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana" (Mwa. 4:5).

> Bwana akamwambia Kaini, "Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde" (Mwa. 4:6-7).

Hapa ndipo dhambi inatajwa kwa mara ya kwanza katika Biblia. Mungu alimwambia Kaini kwamba dhambi ilikuwa inamuotea mlangoni na kwamba ilikuwa ikimtamani yeye. Haya ni matumizi mazuri sana ya uhuishi ambapo mwandishi anaipatia Dhambi nafsi kana kwamba ni aina fulani ya kitu chenye uhai. (Nitaanza kwa herufi kubwa ninapotaja Dhambi katika sehemu iliyosalia ya kitabu hiki ili kutusaidia kuibainisha kama kitu cha pekee ambacho ni tofauti na dhambi (katika hali ya wingi ambazo sisi hutenda.) Kisha Mungu akamwambia Kaini kwamba kama angetenda vyema angeishinda Dhambi, lakini kama hangetenda vyema, Dhambi ilikuwa inangoja kumshambulia kwa sababu ilikuwa inamtamani. Kaini alipaswa kuishinda.

Ni wazi kulingana na kifungu hiki kwamba Dhambi ni kitu kilichokuwa nje ya Kaini na kitu kilichokuwa na tamaa zake. Ni kitu ambacho Kaini alitakiwa kukishinda. Katika hadithi hii Dhambi ilipata nafasi nzuri ya kutumia hasira ya Kaini kuchochea ndani yake hamu ya kumuua ndugu yake. Nasi twaijua sehemu iliyosalia ya hadithi hii ya huzuni. Dhambi ilifanya ilivyotaka kwa Kaini na ikamsababisha amuue Abeli. Mauaji yakawa mojawapo ya dhambi (katika hali ya wingi) za Kaini alizofanya maishani mwake, ilhali Dhambi (katika hali ya umoja) ilikuwa kitu halisi kilichomshawishi kufanya hivyo. Wengi wetu tumemsikia mtu akisema, "Shetani alinifanya nitende jambo hilo." Kweli ni kwamba, Dhambi ndiyo ilimfanya atende kitu hicho, na Dhambi si shetani. Dhambi ni nguvu zilizo hai na pia halisi zinazofanya kazi ulimwenguni kutusababisha kufanya matendo ya dhambi.

Wakati huu katika mazungumzo yetu tunahitaji kurudi nyuma na kukumbuka kile ambacho tumesema mpaka sasa. Mungu alichagua kusamehe dhambi zote za nyakati zote kupitia dhabihu ya Mwana Wake, Yesu (kumbuka Sura ya 6). Hii ina maana kwamba dhambi zote tulizotenda maishani mwetu zimeshasamehewa. Lakini hii haimaanishi kwamba Mungu ameondoa Dhambi (katika hali ya umoja) ulimwenguni. Kweli ni kwamba, Dhambi iko hai sasa kama ilivyokuwa katika siku za Kaini na

Abeli. Dhambi (katika hali ya umoja) hutumia chombo chochote na kile chombo kinachopatikana ili kujaribu kuwafanya watu watende dhambi (katika hali ya wingi).

Hapo mwanzo nilisema kwamba Mungu ameshatukirimia kila kitu tunachohitaji kuishi maisha kwa wingi ndani Yake. Alichotukirimia ni pamoja na kila kitu tunachohitaji kuishinda Dhambi ndani ya maisha yetu. Tukielewa kwa usahihi hii ina maana gani, tunaweza kuenenda katika kweli na kuwekwa huru.

Kosa ambalo wengi wetu hufanya ni kufikiri kwamba tatizo letu ni matendo yenye dhambi ambayo sisi hutenda kama Wakristo. Sisi huzingatia mambo tuyafanyayo ambayo tunajua ni dhambi na kujaribu kuyashinda kwa kile ninachokiita kuidhibiti dhambi. Sisi hujaribau mikakati mbalimbali kama vile kujiwekea nidhamu, kuwajibika kwa wengine, au hata kufunga na kuomba ili tuache kutenda dhambi (katika hali ya wingi). Naamini kwamba ikiwa tutasema ukweli, tutakubali tumejaribu kuidhibiti dhambi lakini hatujafaulu. Hatimaye sisi huishia kufanya jambo lile lile tena. Hili hutufanya tuvunjike moyo na kukata tamaa na hatimaye linaweza kutufanya tushuku uhusiano wetu na Mungu. Sababu ya hili ni kuwa hatuioni Dhambi kwa mtazamo unaofaa (kumbuka umuhimu wa mtazamo katika Sura ya 2.

Lazima tukumbuke kila mara kwamba dhambi zetu binafsti sio tatizo. Mungu amezishughulikia hizo kwa kufanya kile ambacho Yeye pekee anaweza kufanya. Alizisamehe-kabisa na bila masharti. Hata hivyo, bado kuna tatizo la Dhambi ambalo lazima tulishughulikie. Hapa ndipo tunapata tiba kamili ya Mungu. Mungu alijua katika hekima Yake isiyo na kikomo kwamba, sawa na Kaini, sisi pia tungeshindwa kuishinda Dhambi. Alijua kwamba kama tungekabiliwa na nguvu za Dhambi, tungeshindwa kila mara na tungeishia kutenda dhambi (katika hali ya wingi). Hata hivyo, kwa kutupenda mno, alizisamehe dhambi zetu zote na msamaha Wake daima utafunika dhambi yoyote tunayoitenda. Hiki ni kipawa kisichopimika cha neema ya Mungu!

Je, kweli hii ya ajabu ya msamaha wa Mungu usio na masharti ina maana kwamba tuendelee kudumu katika dhambi ili neema na msamaha wa Mungu viweze kuongezeka zaidi? Paulo aliliuliza swali hili katika Warumi. Alisema,

> Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? (Rum. 6:1-3).

Vifungu hivi vina mojawapo ya kweli yenye nguvu mno tunayoweza kujua kama Wakristo. Inaondoa zingatio lote kwa suala la dhambi na kulielekeza kwa tiba kamili ya Mungu dhidi ya nguvu za Dhambi.

Mungu alifanya jambo lisilofikirika. Alitufanya tuwe ndani ya Kristo alipokufa msalabani ili tufe na Yeye. Yesu alipokufa msalabani kwa ajili ya ukombozi wetu, msamaha wa dhambi zetu, sisi pia tulikufa na Yeye ili tuifie nguvu ya Dhambi. Hii ina maana kwamba badala ya Mungu kuiondoa nguvu ya Dhambi ulimwenguni, alitufanya tufe! Sisi tumeifia Dhambi na Dhambi haina mamlaka tena juu yetu.

Hebu fikiria juu ya jambo hili. Sasa tuko katika nafasi mpya kabisa kuhusiana na Dhambi. Dhambi inapotujia na mpango wake wa uovu kutufanya tutende dhambi (katika hali ya wingi), tumeifia! Paulo alitwambia wazi na dhahiri kwamba "kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi" (Rum. 6:7). Hii ina maana kwamba hakika hatuna nguvu zetu wenyewe kuacha kufanya dhambi fulani zinazofanya tujikwae. Ushindi wetu mkuu zaidi uko katika kweli hii; Mungu ametupatia tiba kamili ndani ya Kristo. Njia pekee ya kuacha kutenda dhambi (katika hali ya wingi ni kuwa huru kutokana na nguvu za Dhambi (hali ya umoja), na hili hasa ndilo Kristo ametufanyia. Hatushindi Dhambi kwa nguvu zetu wenyewe. Dhambi itashinda kila mara. Hii ndiyo maana utu wetu wa kale (anthropos, kumbuka Sura ya 2) "ulisulubiwa pamoja naye ili ule mwili wa dhambi upate kuangamizwa, nasi

tusiendelee kuwa tena watumwa wa dhambi" (Rum. 6:6). Kweli ni kwamba hatimaye tumewekwa huru kupitia kifo cha Kristo, ili "vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima" (Rum. 6:4).

Maisha haya mapya yanabainishwa kwa kufahamu sisi ni nani kama mtu mpya aliye ndani ya Kristo Yesu. Sisi si wadhaifu na wasio na uwezo dhidi ya nguvu za Dhambi, bali sasa tuko hai pamoja na Kristo. Dhambi haitutawali tena. Tunashinda kwa kuendelea kujua sisi ni nani kulingana na yote ambayo Mungu ametufanyia. Tukiishi vinginevyo, tutashindwa vibaya na maisha yetu yatakuwa ya kuvunjika moyo na kukata tamaa.

Zingatio letu ni kwa uzima tulionao ndani ya Kristo. Yeye ni uzima wetu na kwa vile tumaini letu liko katika uzima Wake ulio ndani yetu hatuzingatii tena Dhambi (katika hali ya umoja) au dhambi (katika hali ya wingi).

> *Msamaha umeziondoa dhambi zetu na kufa kwetu pamoja na Kristo kumetuweka huru kutokana na nguvu za Dhambi.*

Mungu ametukirimia kwa ukamilifu kila kitu tunachohitaji. Kama vile Mungu alizisamehe dhambi mara moja wakati Yesu alikufa, katika kifo chake, Yesu "aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu" (Rum. 6:10). Hii ina maana kwamba Yeye na sisi tumeifia Dhambi kabisa. Sasa Yesu anayaishi maisha Yake kwa utukufu wa Mungu, na anafanya hivyo ndani yetu na kupitia kwetu sisi. Shukrani kwa Mungu kupitia Bwana yetu Yesu Kristo!

Kitu kimoja nisichotaka kufanya ni kushiriki kweli muhimu sana kisha nimwache mtu akijiuliza, "Hiyo ina maana gani kwa maisha yangu?" au "Inafanyika vipi kwangu?" Ni lazima tuweze kuileta kweli hii kwa sehemu halisi za maisha yetu

Hili halimaanishi kwamba kuitumia kweli hii katika maisha yako kutakuwa rahisi au hata kawaida wakati mwingine. Kweli ni kwamba, matumizi ya kweli katika maisha yako mara nyingi huwa na hali ya usumbufu. Hili hufanyika wakati umeona starehe kufanya kitu kinachopungua kweli ndani ya maisha yako kwa muda mrefu. Vivyo, kweli kamili huonekana kuwa uwongo unapoipata mara ya kwanza. Lakini ukitumia imani yako na kuamini kile Mungu anakuonyesha kuwa kweli, Yeye ni mwaminifu na ataikuza kweli hiyo ndani ya moyo wako na nia yako Kazi ya Roho ni kukuongoza na kukutia katika kweli yote (Yohana 16:13). Hatimaye utageuzwa na kweli hiyo na kweli hiyo itakuweka huru. Huu ni Ukristo halisi kabisa na ni wa kiroho na wa kweli kabisa.

Nilipogeuka kuwa Mkristo mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1986, nilikuwa na umri wa miaka ishirini na moja. Nilikuwa na sehemu nyingi maishani mwangu zilizokuwa mbaya. Kwa sababu ya mambo mengi niliyokuwa nimechagua nikiwa kijana aliyekomaa kati ya miaka kumi na mitano na ishirini na moja, nilikuwa na tabia nyingi za dhambi. Ilikuwa kawaida sana kwangu kujihusisha katika mambo hayo, na nilifanya hayo mambo bila kufikiria matokeo yake. Siku moja Roho Mtakatifu alianza kunisadikisha dhambi zangu, na hatimaye akanipa ufunuo wa Yesu na kuniambia kwamba nilihitaji kumwamini. Nilipopokea kweli na nikaungama dhambi zangu, Mungu alikuwa mwaminifu sana na mwenye haki akanisamehe kabisa (1 Yoh 1:9). Hata hivyo, kuna jambo moja muhimu ambalo sikulijua wakati huo. Sikujua kwamba nilikuwa nimekufa na Kristo na nilikuwa nimeifia nguvu ya Dhambi maishani mwangu. Hakuna aliyeniambia kwamba nilikuwa nimegeuka kuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo na nilikuwa hai kwa Mungu ndani ya Yesu Kristo (Rum. 6:10-11).

Baada ya tukio hilo la kuwa Mkristo, nilitambua kwamba bado nilikuwa na sehemu zenye mienendo ya dhambi maishani mwangu. Mimi kama muumini, bila shaka nilijua kwamba tabia hizo zilikuwa si sahihi, zilikuwa mbaya, na zisizohitajika. Kulikuwa na tatizo moja kubwa. Sikujua namna ya kujiondoa katika mikondo hiyo yenye dhambi. Kama wengi wenu, nilianza safari yangu ya kujaribu kujiondoa kwa mienendo yenye uharibifu. Nilijaribu vifaa kadhaa vya kuidhibiti dhambi. Nilijiunga na makundi

ya wanaume wengine ya kuwajibika. Wangeniuliza "maswali magumu" kila mara nami ningejaribu kuyajibu kwa njia ya kweli. Wakati mwingine ningesema ukweli na kukiri nilikuwa nimeshindwa, nao wangeniombea na kunihimiza nijitahidi zaidi. Wakati mwingine ningewadanganya tu na kusema nilikuwa naendelea vizuri lakini kweli ni kwamba nilikuwa ninashindwa vibaya sana katika sehemu nyingine za maisha yangu.

Hapa ndipo Wakristo wengi hujikuta. Wamezama ndani ya ardhi. Kwa vile hawajui kweli, wanaishi bila nguvu za kuishinda Dhambi ndani ya maisha yao. Wanajua kwamba wameokoa na wamesamehewa—ingawa wakati mwingine wao hukosa kuwa na hakika—lakini hawajafikia kiwango cha kufahamu kabisa wao ni nani katika Kristo kama kiumbe kipya, waliofia nguvu za Dhambi, na walio hai kwa Mungu ndani ya Kristo Yesu. Wamekwama. Watu wengine huishi vipindi vya muda mrefu mahali hapa, wakiwa wamevunjika moyo na wameshindwa, mpaka wanapopata kweli ninayofafanua katika sura hii.

Kwangu mimi, sikuweza kamwe "kupata ushindi" katika sehemu nyingine za maisha yangu. Nilivunjika moyo sana. Halafu Bwana akaanza kunifunulia kweli hii ya ajabu. Nikaanza kuona, ndani ya Maandiko na kupitia njia ya matukio mengi, kweli kwamba mtu wangu wa kale alikuwa amekufa na Kristo. Kwa ajili ya kifo hiki, nilikuwa nimewekwa huru kutokana na nguvu za Dhambi. Nilianza kugundua kwamba sikuhitaji kubadilsha mwenendo wangu, bali nilihitaji kubadilisha ufahamu wangu wa uhusiano wangu na nguvu za Dhambi. Niligundua kwamba Dhambi haikuwa tena na nguvu zozote juu ya maisha yangu za kunifanya nitende dhambi (katika hali ya wingi). Nilikuwa na uhalisi mpya maishani mwangu na nikaanza kuchagua uhakika huo. Nilianza kuigeuza nia yangu kwa kutumia kweli hii ya kuyabadilisha maisha (Rum. 12:2). Nikajifunza kumwamini Bwana aifanye kweli hii kuwa halisi ndani ya maisha yangu. Na nilipofanya hivyo Mungu alikuwa mwaminifu akanifikisha mahali ambapo nilianza kuipata kweli kama hakika ndani ya maisha yangu.

Kama matokeo ya kweli hii kudhihirika maishani mwangu, sikung'ang'ana tena na mikondo ya dhambi ya kale. Nilianza kupata nguvu za maisha ya Kristo ndani yangu zilizokuwa kuu zaidi kuliko nguvu za Dhambi. Nilianza kuelewa kwamba "sheria ya Roho wa uzima katika Kristo Yesu imeniweka huru mbali na sheria ya dhambi na mauti." (Rum. 8:2 NEN). Ufunuo wa kweli hii umeyabadilisha maisha yangu. Ulinipa ushindi ambao roho yangu ilitamani sana. Ulinifanya nifurahie zaidi kile ambacho Mungu alikuwa amenifanyia ndani ya Kristo. Pia ufunuo huo ulinisababisha kuona na kuamini kwamba watoto wote wa Mungu wanaweza kuenenda katika ushindi kutoka kwa nguvu za Dhambi. Sio kwa uwezo wao wenyewe kufanya mambo yaliyo sahihi, bali kwa uzima wa Yesu ulio ndani yao.

*Kupata Kweli*

**Kweli:** Nafsi yako ya kale ilisulubiwa na Kristo. Kupitia kifo chako ndani Yake, umewekwa huru kutokana na nguvu za Dhambi kwa kuwa yule aliyekufa yuko huru kutokana na Dhambi.

**Tamko la Imani:** Nimeifia Dhambi, lakini niko hai kwa Mungu ndani ya Kristo Yesu.

*Kuenenda Katika Kweli*

Chagua kila siku kuamini kwamba uko huru kutokana na nguvu za Dhambi maishani mwako na uko hai kwa Mungu ndani ya Kristo Yesu. Ikiwa unang'ang'ana na dhambi maishani mwako, usizingatie dhambi hizo. Badala yake, zingatia imani yako na utilie maanani kweli hii, umesamehewa kabisa na umefia nguvu za Dhambi maishani mwako leo. Amini kwamba maisha ya Yesu Kristo yaliyo ndani yako yatakuweka huru kutokana na nguvu za Dhambi. Endelea kutembea katika kweli hii kwa njia hii mpaka ugeuzwe na uishi ukiwa huru kutokana na Dhambi.

# 9

# MWILI

*"Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima."*

*~ Yohana 6:63*

*Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka.*

*~ Wagalatia 5:16-17*

Swali ninalosikia likiulizwa na watu wengi ni "Ikiwa kila kitu unachosema kuhusu kiumbe kipya ndani ya Kristo, msamaha, neema, na sisi kuwa huru kutokana na Dhambi ni kweli, mbona Wakristo bado wanatenda dhambi?" Hili ni swali zuri na linahitaji jibu zuri. Ikiwa kweli, Mungu amezisamehe dhambi zetu zote, mtu wetu wa kale amekufa na Kristo, na tumefufuliwa katika maisha mapya na Dhambi haina nguvu juu yetu, mbona bado tunatenda dhambi?

Jibu la swali hili litatupatia kweli nyingine muhimu sana ambayo ni ya lazima kwetu sisi kuishi katika ukamilifu wa maisha yetu ya uungu kama watoto wa Mungu. Kufahamu vizuri kile Biblia inamaanisha na "mwili" ni kiini cha jibu la swali hili.

Mwili umekuwa mada ya wasomi wa Biblia kwa karne nyingi. Bila kuingia sana katika asili yake, inaonekana dhana ya mwili ilikuweko katika fasihi ya kipindi kabla ya Ukristo, kwa hivyo Yesu na mitume walipolitumia neno hilo haikuwa dhana ya kigeni kabisa. Hata hivyo, inaonekana dhana ya "mwili" ilikuzwa zaidi katika wazo la Paulo. Anaipa maana zaidi na kuitumia kueleza sehemu muhimu sana ya maisha ya muumini. Lakini kabla ya kuiangalia, hebu tutoe maelezo ya asili yake ili tukuze ufahamu wa kimsingi wa maana ya "mwili."

Maana ya kwanza na ya kawaida sana ya "mwili" ni kitu chochote kinachohusu sehemu ya uzima yenye "ngozi na mfupa." Biblia inalitumia neno hilo hivi inapozungumzia nyama ya sadaka zilizotolewa

kwa Mungu na makuhani katika Agano la Kale (Lawi. 4:11). Vivyo hivyo, Yohana aliona malaika akiwa amesimama na kuwaita ndege wa angani waje “mpate kula nyama ya wafalme, na nyama ya majemadari, na nyama ya watu hodari, na nyama ya farasi na ya watu wawapandao, na nyama ya watu wote, waungwana kwa watumwa, wadogo kwa wakubwa?” (Ufu. 19:18).

Neno “Mwili” linaweza pia kurejelea wanadamu wote. Luka anatwambia, “Na wote wenye mwili watauona wokovu wa Mungu” (Luka 3:6), na Yesu alipokuwa akimwomba Baba, alitambua kwamba alikuwa amepewa “mamlaka juu ya wote wenye mwili” (Yoh 17:2). Maana hizi mbili ni wazi na rahisi kuelewa. Kuna sehemu nyingine ya maana ya “mwili” isiyo dhahiri na iliyo ngumu zaidi kuelewa. Ni matumizi ya neno hili ndiyo yanatumika kwetu sisi waumini.

Yesu alitumia neno “mwili” kwa namna kadhaa tofauti. Alizungumzia uhusiano wa ndoa kati ya mume na mume akasema, “. . . na hao wawili watakuwa mwili mmoja?” (Mat. 19:5). Hili bila shaka lilirejelea muungano wa kimwili kati ya mume na mke unaotimizwa kwa uhusiano wa kimapenzi. Hata hivyo, pia lilizungumzia muungano wa kina zaidi ambao mume na mke hufikia kiwango cha kina zaidi cha mapenzi kwa mwingiliano wa uhusiano na kujitolea mhanga katika muktadha wa ndoa yao. Mtu anaweza kuyaona mambo haya akiwa karibu na watu wawili waliokaa ndani ya ndoa kwa miaka mingi. Ni kama kwamba kila mara “huwa wanafanana” vile wanavyofikiria na kujieleza. Huu ni muungano wa kina ambao Mungu ananuia mume na mke wafurahie katika muktadha wa uhusiano wa ndoa.

Yesu pia alitumia “mwili” kurejelea maisha Yake mwenyewe aliposema kwamba mwili wake ni mkate anaoutoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu (Yohana 6:51). Alitwambia, “Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake” (Yoh 6:56). Kuna namna nyingine ambayo Yesu alitumia “mwili” na hii ndiyo muhimu zaidi kwetu sisi kuielewa.

Yesu alipowauliza wanafunzi wake wamwambie watu walikuwa wanasema Yeye ni nani, Petro akajibu akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai” (Mat. 16:16). Yesu alikubali jibu la Petro kwa moyo wake wote na akatangaza kwamba Petro alikuwa mbarikiwa kwa kuwa “mwili na damu” havikuwa vimemfunulia kweli hiyo (Mat. 16:17). Alikuwa amepokea ufunuo kuhusu Yesu kutoka kwa Mungu na huo ufunuo ulitoka kwa asili iliyokuwa nje ya uwezo wake wa kawaida kupitia fikira. Yohana alitumia dhana ya “mwili” kwa njia hiyo hiyo alipotwambia kwamba wana wa Mungu wamezaliwa “si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu” (Yohana 1:13).

Yesu alisema pia, “Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima.” (Yohana 6:63). Alikuwa anatwambia ni Roho pekee anayeweza kumpa mtu uzima na uwezo wetu wa kimwili na ufahamu havina manufaa katika uchunguzi wetu wa kutaka kujua Mungu ni nani.. Kutokana na vifungu hivi tunaona kwamba “mwili” ni kitu kinachohusiana moja kwa moja na uwezo wetu wa kimwili ambao ni tofauti kabisa na nguvu na uwezo wa Mungu.

Paulo aliendelea pale Yesu aliachia na akaikuza dhana hii ya “mwili” kwa upana. Paulo alitumia neno “mwili” (neno la Kigiriki sarx) zaidi ya mara 90 katika barua zake. Bila shaka hiyo ilikuwa dhana muhimu sana kwake. Alilitumia neno hilo vile Yesu na Yohana walivyolitumia, lakini kwa njia pana zaidi kufafanua hali ya asili ya jamii ya wanadamu. Hii hali haiwahusu wasioamini pekee. Aliwaambia waumini wa Korintho kwamba hangenena nao kama watu wa kiroho, “ bali kama watu wa mwilini, kama watoto wachanga katika Kristo” (l Kor. 3:1 NEN) na ambao bado ni watu wa “mwilini” (1 Kor. 3:3). Kutokana na kauli hizi tunaona kwamba inawezekana mtu kuwa muumini na bado awe na mambo ya kimwili.

Tunaweza kutumia matumizi mbalimbali ya Paulo ya neno hilo kuunda ufafanuzi wa “mwili” unaoweza kutumiwa, lakini hakuna anayeweza kusema kwa hakika kabisa ni nini maana ya neno hili. Huu ni ufafanuzi wa mtu mmoja wa “mwili” ninaoamini unazipa umuhimu, tofauti ndogo za neno hili

lililo muhimu.

> Mwili ni hali ambayo kwayo mwanadamu hufanya mambo akitumia uwezo wake mwenyewe, akifanya mambo apendavyo. Mwili ni asili ya ubinafsi tunayoitegemea kutimiza mahitaji yetu. Wengine huueleza mwili kuwa kama kisanduku cha vifaa ambacho kila mtu hujaribu kukitumia kushughulikia maisha au kutatua matatizo. Wengine hueleza mwili kuwa mikondo ya mazoea, namna ambayo mwanadamu hujaribu kuyastahimili maisha kwa nguvu zake mwenyewe (Jack Cole, kutoka kwa mafunzo ambayo hayajachapishwa yenye kichwa "Mwili").

Kinyume na wengine, siamini kwamba "mwili" unarejelea asili yetu yenye dhambi au mtu wa kale. "Mwili" hauwezi kuwa unarejelea asili yenye dhambi au mtu wa kale kwa sababu tayari tumeona wazi (kumbuka Sura ya 2 na 8) kwamba Mungu ameifisha kabisa asili yetu yenye dhambi msalabani kwa hivyo sisi sasa ni kiumbe kipya ambacho kimeumbwa katika "haki na utakatifu wa kweli" (Efe. 4:24). Kwa vile hii ni kweli, lazima "mwili" uwe ni sehemu yetu nyingine inayoweza kuweko na kuwa hai ndani ya maisha yetu baada ya mtu kuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo.

Ni katika sehemu mbili tu ndio waandishi wa Agano Jipya wanarejelea maisha yetu ya awali kabla ya kumpokea Kristo kwamba yako ndani ya mwili (Rum. 7:5; Efe. 2:3). Marejeleo yote mengine ya "mwili" yametajwa katika muktadha wa waumini. Hii inatwambia kwamba "mwili" ni kitu kilicho halisi kabisa katika maisha ya Kikristo na tunatakiwa kuelewa vizuri.

Tukitumia ufafanuzi niliotoa hapo juu, ni kweli kwamba "mwili" ni hali tunayoweza kuchagua kuenenda ndani wakati wowote katika safari yetu ya Kikristo. Hii inamaanisha kwamba, tunapochagua wenyewe au kwa ajili ya mikondo ya mazoea, tunaweza kutenda mambo kulingana na mwili. Tunapofanya hivyo, tunachagua kujitegemea na kujitosheleza. Tunaacha kuyategemea maisha ya Kristo yaliyo ndani yetu na tunatembea kwa nguvu zetu wenyewe na kutumia uwezo wetu wenyewe kuzishughulikia hali za maisha. Tunakataa kuenenda katika Roho, na tunaenenda kulingana na mwili. Paulo alieleza katika Warumi 8. Akasema,

> Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu (Rum. 8:5-8).

Jambo la kwanza kufahamu kuhusu kifungu hiki ni kwamba kinatokea katikati ya sura nzima inayozungumzia maisha ya muumini. Warumi 8 inaanza hivi, "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu" (Rum. 8:1). Sehemu iliyosalia ya sura hii inaelezea juu ya maisha ya watu walio ndani ya Kristo. Tutakuwa tunapotosha watu tukisema kwamba vifungu vya 5-8 vinamtofautisha asiyeamini na muumini. Badala yake, ni bora kusema kwamba vifungu hivi vinatofautisha hali ya muumini inayoweza kuweko wakati wowote ule. Paulo anasema kwamba kuna uwezekano wa muumini "*kuyafikiri mambo ya mwili*" au kuyafikiri "*mambo ya roho*.". Hili ndilo tatizo na pia changamoto kwa muumi wakati wowote ule. Lakini Paulo anaeleza wazi kwamba "Basi, kama ni hivyo, ndugu, tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili" (Rum. 8:12).

Kuna kifungu kingine cha Maandiko kinachoeleza zaidi dhana hii.Katika Wagalatia 5 Paulo alisema,

> Kwa hiyo nasema, enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa maana mwili hutamani yale yaliyo kinyume na Roho, naye Roho hutamani yale yaliyo

> kinyume na mwili. Roho na mwili hupingana na kwa sababu hiyo hamwezi kufanya mnayotaka (Gal. 5:16-17 NEN).

Vifungu hivi vinatwambia kwamba kuna vita halisi katika maisha ya muumini kati ya Roho na mwili. Vitu hivi vinatamani, vikishindana. Jambo la kusikitisha ni kwamba, kwa ajili ya kuuelewa vibaya "mwili," Wakristo wengi hushindwa katika vita hivi na kujihusisha katika aina nyingine ya mapambano yasiyo na mwongozo. Badala ya kuzingatia maisha ndani ya Roho kama njia kuu zaidi ya kuvishinda vita vilivyo ndani yao, wanafanya kila aina ya mambo ya kushangaza. Wanaomba wakambolewe kutoka kwa sehemu nyingine za maisha yao au wanafanya vita vya kiroho, wakidhani kwamba shetani ndiye anasababisha wawe na matatizo. Hii ni kweli katika hali nyingine. Hata hivyo, nimegundua kwamba hicho si chanzo cha tatizo kwa waumini wengi. Tatizo ni mwili. Na suluhisho la mwili ni Roho pekee!

Tukienenda katika Roho, hatutatimiza tamaa za mwili. Hii ina maana kwamba kuna tamaa ndani yetu zinazotoka kwetu wenyewe. Ni hali zetu za asili zinazosalia maadamu tuko ndani ya uhai huu. Hii ndiyo maana Paulo akasema, ". . . na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu" (Gal. 2:20). Alielewa kwamba huku akiendelea kuishi katika hali ya asili, bado alihitajika kuchagua kumtegemea Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yake kumwongoza, kumwelekeza, na kuihuisha nafsi yake. Tukikosa kufanya hivyo, tamaa za mwili hutuchochea kutenda mambo bila kumtegemea Bwana.

Tunaona kutoka kwa kifungu hiki kilicho katika Wagalatia 5 kwamba matendo ya mwili ni dhahiri na yanaonekana wazi. Nayo ni:

> . . . uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo (Gal. 5:19-21).

Hii ni orodha isiyopendeza kabisa. Hata hivyo, inawezekana wewe kuwa na tabia za aina hii usipoenenda katika Roho. Paulo alisema kwamba " hata hamwezi kufanya mnayotaka" (Gal. 5:17). Kuna uwezekano wa wewe kutenda dhambi kwa sababu ya tamaa za mwili zinazoshindana na Roho aliye maishani mwako. Hata hivyo, habari njema ya kweli hii ni kwamba ikiwa utachagua Roho aliye maishani mwako basi hutazitimiza tamaa za mwili kwa vyovyote vile.

Paulo alimaliza kifungu hiki kilicho muhimu kwa kutwambia "Wote walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili na shauku zake pamoja na tamaa zake" (Gal. 5:24). Utaratibu huu wa kuusulubisha mwili hufanyika unapoenenda katika Roho. Hii ndiyo maana alimaliza mazungumzo hayo kwa kusema:

> Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho. Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana (Gal. 5:25-26).

Je, unaona mwenendo unaochagua kuwa nao katika utaratibu huu wote? Unajifunza kuyategemea kabisa maisha ya Roho aliye ndani yako kwa kunyenyekea kabisa na kumtegemea. Hakuna nafasi ya majivuno na kiburi katika utaratibu huu kwa sababu sote tunaweza kuathiriwa na tamaa ya mwili kufanya upendavyo mwili ndani ya maisha yetu.

Habari njema zaidi ya zote ni kwamba sisi ni wenye haki ndani ya Kristo Yesu na hatuna tena mwelekeo wa asili wa kufuata mwili. Ndani yetu tuna tamaa ya kuwa wenye haki kwa sababu hiyo ndiyo hali ya asili kwa Yesu. Iwapo tutashindwa na mwili, tujue kwamba hatujashutumiwa kuishi kwa kuelekezwa nao. Tumshukuru Mungu tu kwa msamaha wake tulionao. Tuzingatie imani yetu kwa Roho aliye ndani yetu na tutambue kwamba Mungu ametupa kila kitu tunachohitaji ndani ya Kristo Yesu!

Kuna sifa nyingine ya mwili tunayopaswa kujadili iwapo tutaelewa kikamilifu kweli hii iliyo muhimu. Paulo alisema, sisi ni wale "tumwabuduo Mungu kwa Roho, na kuona fahari juu ya Kristo Yesu, wala hatuutumainii mwili." (Flp. 3:3). Aliendelea kusema kwamba alikuwa na kila sababu ya kuutumaini mwili wake.

> ...Nilitahiriwa siku ya nane, mimi ni Mwisraeli wa kabila la Benyamini, Mwebrania wa Waebrania. Kwa habari ya sheria, ni Farisayo, kwa habari ya juhudi, nilikuwa nalitesa kanisa, kuhusu haki ipatikanayo kwa sheria, mimi nilikuwa sina hatia (Flp. 3:5-6 NEN).

Hii ni orodha ya kuvutia sana ya ukoo wa mtu na mafanikio. Paulo aligusia mambo yote. Alitaja urithi wa ukoo wake, utaifa, familia, mafanikio ya kidini, kujitolea kwake kumtumikia Mungu, na uchaji Mungu. Sidhani kuna mtu aliyekuwa anahusiana na watu na aliyekuwa na mafanikio kumliko Paulo. Lakini alisema kwamba hangeweka tumaini lake kwa vitu hivi. Paulo alitambua kwamba kwa ulimwengu wa kawaida hivyo vyote vilikuwa vitu vinavyofikiriwa kuwa muhimu na njia halisi ya kufaidi. Asili yake, mafunzo, na sifa vilikuwa vitu ambavyo vingemfanya akubalike, awe na cheo cha juu, na hadhi kubwa ya kumfungulia milango ya nafasi nzuri. Licha ya hayo yote, Paulo alisema "naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu" (Flp. 3:8).

Hii inafungua kweli kuu kuhusu mwili, inayokuelekeza kufahamu kwa kina kitambulisho chako ndani ya Bwana. Lazima uwe tayari kuyaacha mambo yote katika maisha yako unayoyaona kuwa nguvu na njia ya kufaidi. Kuwa na usalama usio sahihi au kutafuta kitambulisho chako katika vitu hivyo kunaweza kukuzuia kumjua Bwana kwa undani zaidi. Yesu anataka awe asili ya nguvu zako na hatashindana na nguvu za asili za mwili wako.

Hili linaweza kusikika kuwa neno gumu na ninakubali lina changamoto, lakini nakuhakikishia ni lenye kukupa uzima. Bwana anajua vile tunaweza kuweka tumaini letu katika vitu visivyoweza kutudumisha na kutukamilisha. Yeye atafanya kazi kung'oa vitu hivi ndani ya mioyo yetu. Tukikataa kuweka tumaini letu katika mwili, tutamfahamu Yesu zaidi. Hii ndiyo mojawapo ya ufunuo muhimu niliowahi kupata pasipo wokovu wangu. Kweli hii ina nguvu ya kukuweka huru kwa njia ya ajabu na kuu. (Nitajadili hili zaidi katika Sura ya 11 kuhusu Mateso.)

Ulimwengu unaotuzingira hutushawishi kushangilia nguvu zetu na kujitambuilsha na vitu vingine pasipo Yesu. Ni rahisi sana kuingia katika mtego huu wenye uharibifu. Lakini tukiona udanganyifu wa mwili wetu, tunaweza kuwekwa huru na tuupate uzima wetu pamoja na kitambulisho chetu kwa ukamilifu ndani ya Kristo.

Thawabu yako kuu zaidi katika maisha haya ni kumpata Kristo. Sio kupata sifa kuu, staha, na heshima ya watu. Unapoishi kumpa Mungu utukufu na sio kujitukuza, moyo wako utatamani kitu kimoja tu. Utatamani kumpata Kristo na kupatikana ndani Yake (Fil. 3:9). Huu ni utaratibu wa kuendelea katika maisha yote na utakaokuhitaji kila mara ufanye hivi "nifikie ile alama ya ushindi iliyowekwa ili nipate tuzo ya mwito mkuu wa Mungu ambao nimeitiwa huko juu mbinguni katika Kristo Yesu" (Flp. 3:14 NEN).

Mwili ni kitu halisi sana kwa waumini. Unatakiwa kujua vile unafanya kazi ndani ya maisha yako. Si kitu unachotakiwa kuwa na wasiwasi kukihusu au kukifikiria sana, bali ni kitu unachotakiwa kujua unaweza kuwa huru kutokana nacho kwa kuenenda katika Roho kupitia nguvu za uzima wa Kristo aliye ndani yako. Kama Paulo, wewe pia unaweza kutangaza kwa hakika, "Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu" (Rum. 7:24-25).

*Kupata Kweli*

**Kweli:** Mwili ni tukio la kawaida kwa kila mtu. Hautakiwi kuyaishi maisha yako kulingana na mwili, bali kwa Roho wa Kristo anayeishi ndani yako.

**Tamko la Imani:** Mimi sitawaliwi na mwili, kufanya mambo ya mwili, bali naishi kwa Roho ambaye kupitia kwake nausulubisha mwili kila siku. Yesu anaishi ndani yangu, kupitia kwangu, kama mimi.

*Kuenenda Katika Kweli*

Una uwezo wa kutambua kila siku unapotenda mambo kulingana na mwili na kisha uchague kuenenda katika Roho. Unaweza kuleta mielekeo hiyo ya asili, tamaa, na hamu msalabani na kuvifisha kwa kitendo cha imani na hiari. Utaratibu huu utakuwa rahisi zaidi unapotambua kwamba matendo ya mwili huleta tu uharibifu ndani ya maisha yako na ndani ya maisha ya watu wengine walio karibu nawe, na kazi ya Roho huleta uzima! Unapoenenda katika Roho hutazitimiza tamaa za mwili.

# 10

# ROHO

*Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili, bali na Roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu.*

*~ Warumi 8:9a*

*Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, "Aba", yaani, "Baba."*

*~ Wagalatia 4:6*

Baada ya zaidi ya miongo mitatu ya kuwa muumini, mojawapo ya mada zenye kuleta utata nilizoona miongoni mwa Wakristo ni mada ya Roho. Mara nyingi nimejiuliza; "Ni kwa nini mojawapo ya vipengele vikuu vya Ukristo kimezingirwa na utata mwingi unaoelekea kuwagawanya Wakristo?" Nafikiri jibu pekee lililo sahihi liko ndani ya kweli kwamba shetani anamchukia Mungu na anataka kumdhoofisha kwa njia yoyote ile. Roho ni Mungu kamili na ni kiungo cha uzima kati ya Mungu na mwanadamu. Kazi ya Roho na shughuli Yake hapa duniani na ndani ya maisha ya muumini ni ya msingi kwa mpango wa Mungu.

Sote tumeathiriwa kwa njia moja au nyingine na maoni pamoja na mafundisho kadhaa kuhusu Roho. Wengine wetu tunatoka katika asili zenye kushikilia ukale na zilizorekebishwa zaidi ambapo tulijifunza kwamba kazi ya Roho si sehemu hai sana katika matukio ya kila siku ya muumini. Wengine wetu tunaotoka katika asili za Kipentekoste au ya Karisma tulifunzwa kwamba Roho ni sehemu hai sana ya maisha ya muumini.

Nilikutana na Bwana na nikafunzwa mambo ya Kikristo katika kanisa la Baptisti na hatimaye nikapata shahada yangu ya uzamivu au PhD kutoka kwa seminari ya Baptisti. Nashukuru kwa mizizi yangu ya Baptisti. Nilijifunza kuyapenda Maandiko na kuwa na moyo wa kupenda kazi ya misioni na mataifa. Lakini nakumbuka vizuri sana katika nyakati hizo za kukua kiroho nilifunzwa kuwa mwangalifu sana hasa katika kuwa na uhusiano wa kirafiki na Roho Mtakatifu. Usinielewe vibaya, watu walioyaathiri

maisha yangu waliamini kwamba Roho alihusika katika wokovu wangu, lakini baada ya hapo mambo hayakuwa dhahiri sana, na hawakuyaona mambo sawa na marafiki wangu waliokuwa wa pentekoste na madhehebu yanayosisitiza sana vipawa vya Roho.

Nilijifunza upesi kwamba mabishano mengi yaliibuka wakati waumini walianza kuzungumza juu ya vipawa au kujidhihirisha kwa Roho pamoja na kubatizwa kwa Roho. Nitasema wazi, sitashughulikia mada hizi kinagaubaga. Siamini kwamba mada hizi zapaswa kuwa zingatio kuu katika kumfahamu Roho, lakini naamini tunahitaji kuelewa kazi ya Roho na uhusiano wetu naye katika maisha yetu ya kila siku.

Yesu alitoa maagizo yaliyo wazi zaidi kuhusu kazi na shughuli ya Roho kuliko mtu yeyote yule katika Maandiko. Mengi ya mafundisho yake kuhusu Roho yanapatikana katika injili ya Yohana. Katika Yohana 16 Yesu anawaambia wanafunzi wake kwamba ni bora yeye aende ili Msaidizi aweze kuja (Yohana 16:7). Aliahidi kumtuma Roho ambaye angekuwa hai ndani ya maisha ya waumini na vilevile ulimwenguni.

Yesu alitwambia Roho angefanya kazi gani ndani ya maisha ya muumini. Alisema,

> "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari. Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwapasheni habari" (Yohana 16:13-15).

Yesu alisema Roho angewaongoza "nyinyi" awatie kwenye kweli yote. "Nyinyi" inaelekezwa kwa wanafunzi, wanaomfuata Yesu na kumwamini. Roho atatuongoza atutie kwenye kweli yote. Roho humtukuza Yesu ndani ya maisha yetu na kutupa kila kipawa Chake.. Nashukuru kwamba Roho anafanya kazi ndani ya maisha yangu kunielekeza katika kweli yote na kunipa kila kipawa ambacho ni cha Yesu (1 Kor. 2:12). Je, unafurahia kujua kwamba Roho anafanya kazi hii ndani ya maisha yako sasa hivi?

Kweli kuu zaidi ambayo Roho anakueleza kwayo ni kwamba wewe ni mtoto wa Mungu. Mungu ametuma Roho moyoni mwako na Yeye anaendelea kushuhudia kwamba wewe ni mtoto wa Mungu mpaka hatimaye mwalia "Abba, yaani, Baba" (Rum. 8:15-17; Gal. 4:6-7). Yesu alipokuwa duniani, alikuwa salama kabisa kujua ukweli huu kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu. Roho anakupa hakikisho hilo hilo. Anakuelekeza kusadiki kikamilifu kwamba una Baba wa mbinguni na wewe ni mtoto Wake. Ikiwa wewe ni mtoto Wake, basi wewe pia ni mrithi wa Mungu na arithiye pamoja na Kristo (Rum. 8:17). Hii inamaanisha kwamba kila kitu ambacho ni cha Yesu ni chetu pia.

Roho anahusika vilivyo katika kusudi kuu la Mungu la kushiriki nawe maisha Yake. Roho ndiye atiaye uzima (John 6:63; 2 Cor. 3:6), na uzima anaokupa ni uzima wa Yesu. Roho wa Uzima ndani ya Kristo anafanya kazi maishani mwako kuendelea kukupa ushindi dhidi ya Dhambi na mauti (Rum. 8:2). Uwepo wa Roho wa Kristo ulio ndani yako ni thibitisho kwamba wewe ni wa Mungu (Rum. 8:9) na Roho aliye ndani yako "ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa" (Rum. 8:11). Unapoongozwa na Roho, unaonyesha kwamba wewe ni mtoto wa Mungu (Rum. 8:14). Roho hudhihirisha tunda Lake ambalo ni "upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi" ndani yako (Gal. 5:22). Hii ndiyo hulka ya Yesu ya kujidhihirisha kupitia kwa maisha yako.

Roho pia hukusaidia kwa kukuombea unapokuwa mdhaifu na hujui jinsi ya kuomba. Yeye anajua hasa jinsi ya kuomba kwa sababu anajua nia ya Mungu, naye huomba kulingana na mapenzi ya Mungu (Rum. 8:26-27).

Roho hukubatiza ili uingie katika mwili wa Kristo unapoamini mara ya kwanza (1 Kor. 12:13) kisha

anakupa vipawa kadri na mapenzi Yake kwa manufaa ya mwili wa Kristo (I Kor. 12:7; 1 1). Yeye ni muhuri na thibitisho la urithi utakaopata siku za usoni baada ya wewe kufa (2 Kor. 1:22; 5:5). Mwili wako ni hekalu halisi la Roho naye anadumu ndani yako (1 Kor. 6:19). Haya ni machache ya mambo ya ajabu ambayo Roho hufanya ndani ya maisha ya muumini.

Kuongezea kufanya kazi kwa nguvu sana ndani ya maisha ya waumini, Roho yuko hai pia ulimwenguni. Yesu alisema,

> "Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena; kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa" (Yoh 16:8-11).

Hivi ni vifungu vyenye dhana kuu kwa watu wengi ambao hufunza juu ya kazi ya Roho ndani ya maisha ya Mkristo. Lakini ningependa utambue neno kuu katika vifungu hivi. Neno hilo ni "ulimwengu." Yesu alisema kwamba baada ya Roho kuja atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.

Katika Biblia "ulimwengu" unarejelea vitu vya dunia ambavyo Mungu ameumba. Lakini, muhimu zaidi, neno hilo linarejelea hasa wasioamini. Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtuma Mwanawe (John 3:16) ili ulimwengu upate kuokolewa (Yohana 3:17), bali ulimwengu haukumtambua (John 1:10) mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini (2 Cor. 4:4), Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake (2 Cor. 5:19). Vifungu hivi vinaelekeza kwa ukweli huu; "ulimwengu" unarejelea wasioamini.

Yesu alikuwa anatwambia kwamba Roho atakuja ili aliteke hakika-ufahamu na utambuzi—kwa ulimwengu usioamini katika sehemu hizi tatu:

- Dhambi
- Haki
- Hukumu

Kuna makosa mawili ya kawaida ambayo mimi huwaona watu wakifanya kuhusu vifungu hivi. Kwanza, wao wanakosa kujua ukweli kwamba Roho anauhakikisha ulimwengu-wasioamini. Pili, wanaacha kusoma baada ya kifungu cha nane. . Nilitaja hapo mwanzoni katika Sura ya 1 kwenye ufafanuzi wangu wa Warumi 8:28-29 kwamba tunatakiwa kila mara kusoma sura nzima katika Maandiko. Tukiachia tu kwa kifungu cha nane, tunakosa kujua wazo zima ambalo Yesu alikuwa akisema. Katika Yohana 16:9-11, Yesu alifafanua alichomaanisha hasa aliposema Roho atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, haki, na hukumu.

- Dhambi ⟶ kwa kuwa haawamini.
- Haki ⟶ kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena.
- Hukumu ⟶ kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa.

Napenda vile Yesu alikuwa wazi kabisa. Hakuwacha nafasi ya watu kubahatisha. Kazi ya Roho ni kuhakikisha wasioamini katika sehemu tatu.

Kwanza, Roho amekuja kuwahakikisha wasioamini kwamba hawaamini. Anataka waone kwamba kutoamini kwao ndiko kunawatenga na Mungu. Yesu akajibu, " Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye" (Yoh 6:29), na "Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu" (Yoh 3:18). Kweli kabisa,

Mungu anautaka ulimwengu uokoke, na ili jambo hilo lifanyike wanatakiwa kumwamini Yesu. Kazi ya Roho ni kuhakikisha ulimwengu kuhusu kutoamini kwao ili wapate kumwamini Yeye.

Pili, Roho anauhakikisha ulimwengu kwa habari ya haki. Anafanya hivyo kwa kuwa Yesu hayuko ulimwenguni tena kama mwanadamu ili ulimwengu umwone. Yesu alikuwa mfano wa haki na alionyesha dhahiri ni nini maana ya kuwa na haki mbele za Mungu. Lakini kwa vile ameenda mbinguni, ni kazi ya Roho kuonyesha au kuhakikisha ulimwengu vile haki inafanana. Hili ni jambo la ajabu kulifikiria. Roho anawaonyesha wasiomini vile haki inafanana kwa sababu hawawezi kumwona Yesu. Hii inamaanisha kwamba Roho anaufunulia ulimwengu ni nini maana ya kuwa katika uhusiano sahihi na Mungu. (kumbuka Sura ya 5 kuhusu Haki). Roho hazunguki akiuonyesha ulimwengu vile una makosa mbele za Mungu. Anawaonyesha namna ya kuwa sahihi na Mungu!

Tatu, Roho anauonyesha ulimwengu kwamba mkuu wa ulimwengu huu, amekwisha kuhukumiwa. Mkuu wa ulimwengu huu ni shetani. Paulo alimwita "mfalme wa uwezo wa anga" (Efe. 2:2) na "mungu wa dunia hii" (2 Kor. 4:4). Kazi ya Roho ni kuudhihirishia ulimwengu kwamba shetani amekwishahukumiwa! Roho anaufunulia ulimwengu kabla hawajaamini kwamba Yesu amekwisha "kuzivua enzi na mamlaka," na "alizifanya kuwa kitu cha fedheha hadharani kwa kuziburura kwa ujasiri, akizishinda" katika msalaba wa Kristo (Kol. 2:15).

Wengi wenu huenda mmesikia mtu akisema kwamba kazi ya Roho maishani mwako ni kukuhakikisha kwa habari ya dhambi. Utakapomaliza kitabu hiki, utaona kwamba jambo hilo halina maana mara tu utakapoelewa kile ambacho Mungu amefanya kuhusu Dhambi (katika hali ya umoja) na dhambi (katika hali ya wingi) zako (kumbuka Sura ya 6, 7, na 8). Maandiko hayafunzi mahali popote kwamba Roho huwahakikisha waumini kwa habari za dhambi zao.

Yohana 16:8 ndicho kifungu pekee kwenye Biblia kinachozungumzia kuhakikisha kuhusu dhambi na hii ni dhambi ya kutoamini. Neno "hakikisha" katika lugha ya Kigiriki lina maana ya "kuonyesha" au "kufichua." Linaweza pia kuwa na maana ya "shutumu." Sababu ya kusema Roho haonyeshi au hafichui dhambi zetu au hatushutumu kuhusu dhambi ni kwa kuwa Mungu amezisamehe dhambi zetu zote na hizo si muhimu kwa Bwana.

Ukielewa kabisa wewe ni nani ndani ya Kristo, basi utajua kwamba hauhitaji Roho azifichue dhambi zako. Paulo alisema kwamba matendo ya mwili yenye dhambi ni "dhahiri" (Gal. 5:19), na unatakiwa "kuyafichua" mwenyewe (Efe. 5:11). Paulo alieleza kinaganaga vile utaratibu huu unafanya kazi ndani ya maisha yako. Alitaja matendo kadhaa yenye dhambi na uasherati "usitajwe kwenu kamwe" (Efe. 5:3). Kisha akasema,

> …kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni kama watoto wa nuru, kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli; mkihakiki ni nini impendezayo Bwana.(Efe. 5:8-10).

Kama muumini, kila mara unajifunza ni mambo gani yanampendeza Bwana na namna ya kuenenda katika Nuru. Unapofanya hivi, "yote yaliyokemewa hudhihirishwa na nuru maana kila kilichodhihirika ni nuru" (Efe. 5:13). Neno "dhihirisha" lililo hapa ni neno lilo hilo lililotumiwa katika vifungu vingine lenye maana ya "kuhakikisha" katika mikutadha tofauti (Yohana 16:8; 1 Kor. 14:24; Yuda 1:15). Bila shaka, "kuhakikisha" kokote ndani ya maisha yetu huja kama matokeo ya kawaida ya kuwa ndani ya Nuru, kwa kuwa Kristo ndiye "aliyeng'aa mioyoni mwetu" (2 Kor. 4:6) na hatuko tena ndani ya giza. . Sisi "tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.' (l Yoh 1:7).

Maisha ndani ya Roho yanaeleza wazi kabisa kuliko kweli yoyote ile, ni nini maana ya kuwa Mkristo.

Uliumbwa na Mungu ili uwe na ushirika na Yeye, na hili hufanyika kupitia kwa Roho Wake aliye ndani yako. Roho anakupa uzima, na uwepo wake ndani yako unathibitisha kwamba wewe ni mtoto wa Mungu na mrithi pamoja na Kristo. Akiwa na Baba na Mwana, Roho hutimiza hali ya Mungu kushiriki uzima Wake nawe.

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Roho wa Kristo, Roho Mtakatifu, anaishi ndani yako kukufanya ujue na kukupa kila kitu ambacho ni cha Yesu.

**Tamko la Imani:** Yule Roho aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu anaishi ndani ya mwili wangu naye anatenda kazi kwa njia nyingi, ikijumlisha kushuhudia kwamba mimi ni mtoto wa Mungu, kuniongoza katika kweli yote, na kuniwezesha kuishi maisha yasiyo na dhambi, na akidhihirisha tunda Lake ndani yangu na kupitia maisha yangu.

### *WKuenenda Katika Kweli*

Haijalishi umekuwa na mtazamo upi kuhusu Roho Mtakatifu hapo awali, anza leo kuamini kwamba anaishi ndani ya mwili wako, na kwamba Yeye ni Roho wa Yesu Kristo. Amekuja kuishi ndani yako ili adhihirishe uzima wa Yesu. Omba Bwana ayafunue macho yako ili ujue kweli yake na akusaidie kuishi ndani ya Roho kila siku.

# 11

# MATESO

*Mateso peke yake si kitu. Bali mateso yakishirikishwa na shauku ya Kristo ni kipawa cha ajabu, kipawa bora zaidi, na ishara ya upendo.*

*~ Mama Teresa*

*Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake.*

*~ Wafilipi 1:29*

Hakuna anayetaka kusikia kwamba mateso ni sehemu muhimu sana ya kuwa Mkristo. Ningetaka kukosa kuiweka sura hii ndani ya kitabu hiki. Lakini, la kusikitisha, ingawa hatutaki kusikia jambo hili, Mungu ana mengi ya kusema kuhusu mateso. Kwa hivyo, itatufaa zaidi kuitazama mada hii yenye changamoto lakini iliyo muhimu. Tukielewa ukweli kuhusu mateso, tunaweza kuyakubali kama sehemu muhimu na yenye faida ya kuishi katika kusudi kuu la Mungu.

Maisha ni magumu lakini hatuna starehe ya kuchagua ni matukio yapi yatatupata. Ingekuwa bora kama tungechagua matukio mazuri pekee na kuyaacha mabaya. Lakini Yesu alitwambia tujipe moyo kwa kuwa ulimwenguni tutakuwa na dhiki-mambo magumu–lakini ameushinda ulimwengu (Yohana 16:33). Hii ni ahadi nzuri sana na yenye kutia moyo, lakini inachukulia kwamba mambo yatakuwa magumu, na hakuna yeyote kati yetu anayependa mambo magumu.

Habari njema ni kwamba Mungu ni mwaminifu katika hali yote tunayopitia naye hutumia kila kitu kinachofanyika maishani mwetu. Kumbuka tulivyoona hapo mwanzo katika Sura ya 1 kwamba katika mambo yote Mungu hutenda kazi katika kuwapatia mema. "Mambo yote" yanajumlisha mazuri na mabaya. Anayatumia yote kutufanya tufuate mfano wa Kristo.

Agano Jipya limejaa vifungu vinavyorejelea mateso. Waandishi hao wanatumia Angalau maneno matano tofauti yanayotokea mara 120 kueleza mateso kwa njia moja au nyingine. Mojawapo ya

mateso yanayorejelewa ni matukio ya miili ya waumini kudhuriwa kwa sababu ya imani yao katika Kristo. Mojawapo ya maelezo haya yako katika Matendo wakati mitume walichapwa kwa fimbo kwa kuihubiri injili, nao walijaa furaha kwa sababu walihesabiwa kustahili kupata aibu kwa ajili ya jina la Yesu. (Matendo 5:41). Walikuwa wanafanya kile ambacho Yesu aliwaambia wafanye aliposema,

> "Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu" (Mat. 5:11-12).

Mitume waliyaona mateso kuwa sehemu ya kawaida ya maisha ya Kikristo. Petro alitwambia, "Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake" (1 Pet. 2:21).

Wakati Sauli (Paulo) aliitwa na Yesu aliyefufuka akiwa njiani kuelekea Dameski, alitumwa kwa Anania. Bwana akanena na Anania kuhusu Sauli akasema,

> "Nenda tu; kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli. Maana nitamwonyesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya Jina langu" (Matendo 9:15-16).

Mungu alikuwa na mwito maalum kwa Paulo naye alitumiwa na Mungu kueneza injili mahali kwingi kuliko alivyofanya mtu yeyote katika miaka 2000 iliyopita. Mbali na kulitangaza jina la Yesu, Mungu alisema pia vile Paulo angeteseka. Sote tungependa kusikia Mungu akinena vile atatutumia kwa hali kuu zaidi. Lakini nashangaa, tutafanyaje ikiwa Mungu ataongeza, mbali na kutumiwa naye kufanya mambo makuu, "lazima tuteseke?"

Paulo aligundua vizuri sana kwamba kile Mungu alikuwa amenena kumhusu kingetimia. Sikiza maelezo marefu aliyotoa Paulo kuhusu mateso yake:

> Je, wao ni watumishi wa Kristo? (Nanena kiwazimu.) Mimi ni zaidi yao. Nimefanya kazi kwa bidii kuwaliko wao, nimefungwa gerezani mara kwa mara, nimechapwa mijeledi sana, na nimekabiliwa na mauti mara nyingi. Mara tano nimechapwa na Wayahudi viboko arobaini kasoro kimoja. Mara tatu nilichapwa kwa fimbo, mara moja nilipigwa kwa mawe, mara tatu nimevunjikiwa na meli, nimekaa kilindini usiku kucha na mchana kutwa, katika safari za mara kwa mara. Nimekabiliwa na hatari za kwenye mito, hatari za wanyang'anyi, hatari kutoka kwa watu wangu mwenyewe, hatari kutoka kwa watu wa Mataifa; hatari mijini, hatari nyikani, hatari baharini; na hatari kutoka kwa ndugu wa uongo. Nimekuwa katika kazi ngumu na taabu, katika kukesha mara nyingi; ninajua kukaa njaa na kuona kiu; nimefunga kula chakula mara nyingi; nimehisi baridi na kuwa uchi. Zaidi ya hayo yote, nakabiliwa na mzigo wa wajibu wangu kwa makanisa yote (2 Kor. 11:23-28).

Huduma yote ya Paulo ilikuwa na mateso mengi, lakini alidumisha mtazamo wa kushangaza sana katika hali hizo zote. Alisema, "Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu" (Rum. 8:18). (Tutaangalia kifungu hiki kinagaubaga baadaye katika sura hii.)

Wengi wetu hatutawahi kamwe kustahimili kuteswa mwili kwa sababu ya imani yetu. Hata hivyo, idadi isiyohesabika ya Wakristo wameteseka kwa ajili ya imani yao kwa zaidi ya miaka 2000 iliyopita, na wakati huu ndugu na dada zetu wengi walio ndani ya Kristo wanateseka kwa ajili ya jina lake. Hatupaswi kupuuza kwamba jambo hili linaweza kututendekea maishani mwetu. Petro aliyetwambia tuufuate mfano tulioonyeshwa na Kristo alitwambia pia, "Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba

ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho" (1 Pet. 4:12). Petro alikuwa anawatia moyo waumini waliokuwa wanapitia nyakati ngumu za mateso, wasione kuwa ni ajabu kana kwamba "kitu kigeni" kilikuwa kinawapata. Ingawa huenda tusipitie mateso ya mwili, bado tutapitia mambo magumu katika maisha haya. Kuna majaribu mengi na shida, na yote hayo ni sehemu ya mateso tunayoyapitia sisi.

Kuongezea kwa mateso ya kimwili, kudhihirika kwa kawaida zaidi kwa mateso katika Agano Jipya ni la dhiki na kuumizwa. Hii inaweza kujitokeza kwa njia za kila aina, na hakuna yeyote asiyeweza kudhurika. Aina hii ya mateso huja sanasana kwa ajili ya dhambi iliyoingia ulimwenguni. Wakati mwingine, uovu wa ulimwengu huyagusa maisha yetu binafsi na kutupa changamoto nzito. Kinaweza kuwa kitu cha kawaida kama uhusiano wa kulazimisha, au chaweza kuwa kitu cha kuvuruga kama msiba usiotarajiwa, unaoathiri maisha yetu au maisha ya wapendwa wetu. Matukio haya huleta "uzito" wa kweli ndani ya maisha yetu ulio na uchungu na wakati mwingine usioweza kuvumilika. Paulo alituhimiza kwamba katika nyakati hizi "ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini" (Rum. 5:3-4). Mara nyingi sisi huzungumza kuhusu uponyaji na ushindi na kusema machache sana kuhusu huzuni na udhaifu. Hizi ni sehemu za kawaida za maisha na kweli ni kwamba hizo hutimiza kitu fulani kinachoweza tu kutendeka tunapoyapitia mateso.

Kuongeza kwa mateso ya mwili na kulemewa maishani, pia tutapitia majaribu na majaribio ili imani yetu iweze kutakaswa kwa utukufu wa Mungu. Naamini kwamba matukio haya ni sehemu ya mateso pia, na tunaweza kuyakubali kama vyombo vya mgeuzo katika utaratibu wetu wa kukomaa. Tunajua kwamba tutapitia "majaribu mbalimbali" (Yak. 1:2) na pia "mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali" (l Pete. 1:6) kwa ajili ya kujaribiwa kwa imani yenu.

Imani yetu ni kitu cha thamani sana na siku moja, baada ya hiyo kujaribiwa na kutakaswa, kitakuwa ndicho kitu cha kuleta "sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo." (1 Pet. 1:7). Ni wazo la ajabu kwamba hatimaye tutakapomwona Bwana uso kwa uso, kitu kimoja kitakachompa utukufu zaidi ya vitu vingine vyote ni imani yetu. Mungu anayatumia majaribu yetu yote kuitakasa imani yetu na kuifanya kuwa safi kama dhahabu.

Tukiikubali kazi ya mateso ndani ya maisha yetu, tunaweza hata kuamua kupoteza vitu vingi kwa ajili ya Kristo. (Nilijadili jambo hili katika Sura ya 9 kuhusu Mwili.) Najua inaweza kuwa vigumu kulisikia hili, lakini huu ni ufunguo wa kufungua uhusiano wa upendo mkuu na Yesu. Tunatakiwa kufikia mahali ambapo tuko tayari kuyahesabu mambo yote mema katika maisha yetu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo (Flp. 3:7-8). Hakuna chochote tulichonacho maishani mwetu kinaweza kufananishwa na "uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu" na "ili nipate Kristo" (Phil. 3:8). Hili linawezekana tu tunapokusudia kuviacha vitu vinavyotupa kitambulisho, nguvu, na liwazo.

Nakumbuka wakati mmoja baada tu ya kumaliza masomo katika chuo cha seminari mwaka wa 1997 na shahada yangu ya uzamivu au PhD. Nilikuwa nasoma Biblia yangu siku moja na nikakisoma kifungu hiki katika Luka 16:15 (NEN): "Ninyi mnajionyesha kuwa wenye haki mbele za wanadamu, lakini Mungu anaijua mioyo yenu. Kwa maana vile vitu ambavyo wanadamu wanavithamini sana, kwa Mungu ni machukizo." Nilikuwa nimekaa miaka kumi katika chuo kikuu na nikapata shahada ya juu zaidi inayoweza kupatikana katika masomo. Nilikuwa najisikia vizuri sana na nilikuwa na hakika mafanikio yangu yalistahili heshima mbele ya watu wengine. Halafu nikakisoma kifungu hiki. Nilisikia Bwana akisema kwamba vitu ambavyo wanadamu wanavithamini sana ni machukizo kwa Mungu. Hii haimaanishi kwamba Mungu anachukia masomo. Yeye ndiye aliniambia nisome na nimalize shahada yangu. Alikuwa anajaribu kunionyesha kweli muhimu zaidi. Niliona kwamba mwanadamu ni mwepesi kuhisi ndani ya mwili wake kwamba anataka kuvithamini sana vitu. Lakini Mungu havioni vitu jinsi

mwanadamu anavyoviona. Kweli hii ilinisumbua sana na nikamuuliza Bwana vile inawezekana mimi kuvihesabu kama hasara vitu visivyoshikika maishani mwangu.

Bwana alinisaidia kuona kwamba singeweza kuondoa shahada yangu ya uzamivu au PhD maishani mwangu na kuondoa mambo yote niliyojifunza. Singeweza kufanya hivyo kama vile Paulo hangeacha kuwa Mwebrania, au kuacha kuwa wa kabila la Benyamini, n.k. Hata hivyo, niligundua kwamba ningeamua kuvihesabu vitu hivyo kuwa hasara kwa ajili ya Kristo Yesu. Ningeweza kuvihesabu kuwa hasara vitu kama: sifa, elimu, utaifa, na mafanikio mengine kama alivofanya Paulo. Hili halihusu kuviondoa vitu hivyo katika maisha yetu. Bali linahusu kuviachilia na kutoruhusu vitu hivyo vizame mioyoni mwetu. Wakati niliona vile moyo wangu ulivishikilia vitu hivyo ili niweze kupata kitambulisho na sifa kutoka kwa wanadamu, nilielewa maana ya kuvihesabu vitu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo.

Ni Yesu pekee ndiye anataka kusimama katika nafasi ya thamani ndani ya moyo wako. Hakuna chochote ulichopata maishani kinaweza kufananishwa na kumjua Kristo na kumruhusu kuwa na nafasi yake inayostahili ndani ya maisha yako. Naweza kukuhakikishia kwamba ukiwa tayari kuviachilia vitu vinavyoshindana na Yesu moyoni mwako na kuviona kuwa hasara, kuna mateso ya kweli yatakayofanyika. Lakini hilo linastahili ili kumpata Kristo!

Kwa kuwa mateso ni sehemu muhimu sana ya maisha ya Kikristo, inafaa kujua jinsi tunapaswa kuyachukulia na kile yanatimiza. Mambo haya mawili huambatana, na waandishi wa Biblia wanaeleza wazi kabisa.


Soma vifungu hivi na usikilize moyo wa watu waliopata kuelewa vizuri kazi ambayo mateso yalifanya ndani ya maisha yao.

- Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake (Kol. 1:24).
- Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi (Rum. 5:3-5).
- Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi (Yak 1:2-3).
- Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali (1 Pet. 1:6).

Kitu kinachounganisha vifungu hivi vyote ni mtazamo wetu kuhusu mateso. Tunapaswa kufurahi tunapopata mateso! Tunafurahi kwa sababu tunajua kwamba mateso tunayoyapata yanahusiana moja kwa moja na matukio ambayo Yesu alipitia, nasi pia tumeitwa kwa kusudi hili kwa vile Yesu alituachia mfano wa kufuata katika hatua zake (1 Pet. 2:21).

Sisi pia tuna hakikisho kwamba dhiki tunayopitia inatimiza jambo fulani lenye thamani kuu ndani ya maisha yetu. Paulo aliliita jambo hilo "utukufu ule utakaofunuliwa" (Rum. 8:18). Alisema, "Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana;" (2 Kor. 4:17). Hili linatupa tumaini kwamba dhiki yetu si bure.

Kuna mambo kadhaa muhimu ya kutambua katika vifungu hivi. Kwanza, dhiki tunayoipitia ni "ya muda mfupi" na "nyepesi," lakini utukufu ni "wa milele" na "wa maana." Hii ina maana kwamba dhiki yoyote tunayoipitia huchukua tu muda mfupi ikifananishwa na milele. Pia ni "nyepesi" ikilinganishwa na "wingi" wa utukufu. Mchoro huu unatupa macho ya kuona kweli hii.




Pili, dhiki hiyo "inatufanyia" utukufu. Hii ina maana kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya dhiki na utukufu. Utukufu unaweza tu kupatikana iwapo kuna dhiki. Dhiki hii inatimiza jambo fulani ndani ya maisha yetu na ni dhiki tu ndiyo inaweza kufanya hivyo.

Mateso pia yana kusudi la kutukamilisha na kutufanya tuwe watu waliokomaa. Yesu "alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata" (Ebr. 5:8), na

> . . . kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso (Ebr. 2:10).

Yesu alipitia mateso ili aweze kujifunza kutii na awe mkamilifu. Huenda hili likawa gumu sana kuelewa. Haimaanishi kwamba Yesu hakuwa mkamilifu na kwamba alikuwa na dhambi au dosari ya uadilifu. Ina maana kwamba kulikuwa na kuridhika na kutaka kukamilisha yote ambayo Mungu alitaka kutimiza ndani ya maisha ya Yesu. Na hili lingewezekana tu kupitia mateso yake na Yeye kujifunza kumtii Baba ingawa lilikuwa jambo gumu.

Neno "kukamilisha" katika kifungu hiki lina maana ya "kumaliza" au "kutimiza." Kuna mambo mengi yaliyohitaji kukamilishwa ndani ya maisha ya Yesu, na haingewezekana pasipo mateso. Njia hii ilifikia kilele ndani ya maisha Yake alipomwambia Baba, "... walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke" (Lk. 22:42).

Vivyo hivyo, kuna mambo mengi ndani ya maisha yako yanayotakiwa kukamilishwa, na hayo yatafanyika tu kupitia mateso. Mungu atatumia mambo magumu unayopitia kukufunza kutii na kukufikisha mahali pa ukamilifu. Huu ni utaratibu wa wewe kujua "ushirika wa mateso yake" (Flp. 3:10) na "nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo," (Kol. 1:24). Ukiiona kweli hii na kuikubali kwa imani, utakua katika uwezo wako wa kustahimili dhiki, ukijua kwamba inakufanyia jambo fulani ndani ya maisha yako lenye thamani kabisa. Mtazamo huu ni ishara ya ukomavu wa kiroho na alama ya mwana anayetii.

Mateso hukuunganisha na maisha ya Yesu kwa njia ya upendo mwingi zaidi. Labda hii ndiyo kweli muhimu zaidi kuhusu mateso. Unapopitia mateso, unayagusa maisha ya Yesu kwa sababu Yeye yuko nawe katika mateso yako. Paulo alimaanisha hivyo aliposema maneno haya "ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake" (Flp. 3:10). Neno "ushirika" lina maana ya kushiriki kwa undani. Unapopitia mateso, Yesu yuko nawe katika

mateso yako. Anachagua kushiriki nawe binafsi katika maisha yako. Kadri unavyoelewa zaidi ukweli huu wenye fumbo, ndivyo utakavyoelewa zaidi thamani ya mateso. Kuna ushirika wa kina zaidi kati yako na Yesu unaoweza kufanyika tu unapopitia mateso. Hii ndiyo maana mateso ni kweli ya kukupa uzima na ni muhimu sana.

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Mateso ni sehemu ya kuwa Mkristo na Mungu huyatumia ndani ya maisha yako kwa njia zinazoweza kukufunza kumtegemea zaidi, na yatakufanyia utukufu wa milele unaozidi mateso unayopitia sasa.

**Tamko la Imani:** Sitayapinga au kuyadharau mateso yanayofanyika ndani ya maisha yangu na nitaamini kwamba nina fursa ya kushiriki katika mateso ya Yesu na kupata faida itakayopatikana baada ya kupitia mateso.

### *Kuenenda Katika Kweli*

Anza kuona kwamba mateso ni sehemu muhimu ya maisha yako kama mtoto wa Mungu. Kubali kwamba, ingawa mateso si kitu cha kufurahisha, unataka kupata ushirika na Yesu kupitia mateso yoyote yatakayofanyika ndani ya maisha yako. Amini kweli hii kwamba mateso unayoyapitia yanakufanyia kitu fulani ndani ya maisha yako usichoweza kuhisi au kuona wakati huu. Jipe moyo, kujua kwamba Yesu yuko nawe kila mara katika mateso unayopitia kwa sababu mateso uyapitiayo ni sehemu ya mateso Yake. Jua kwamba Mungu atakuhifadhi katika mateso yoyote utakayopitia na atakupitisha ndani ili uwe na ushirika wa kina zaidi naye.

# 12

# PUMZIKO

*Kwa hiyo basi, imebaki raha ya Sabato kwa ajili ya watu wa Mungu; kwa kuwa kila mmoja aingiaye katika raha ya Mungu pia hupumzika kutoka kazi zake mwenyewe, kama vile Mungu alivyopumzika kutoka kazi zake.*

*~ Waebrania 4:9-10*

*"Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi."*

*~ Matthew 11:28-30*

Je, umewahi kuhisi "umechoka" katika safari yako ya Kikristo? Kuna sababu nyingi za sisi kuchoka katika eneo la kidunia, lakini tunaweza pia kuchoka katika maisha yetu ya Kikristo. Watu wengi huhisi kana kwamba kuwa Mkristo ni jambo gumu na wao hung'ang'ana kupata hali njema na amani. Nina hakika hilo ni kwa sababu hawajawekwa huru kupitia kweli muhimu sana ninayoshiriki katika kitabu hiki. Nimeishi muda mrefu wa kutosha kuniwezesha kujua kwamba ustawi wetu hautokani na hali zetu. Ustawi unaweza tu kupatikana kwa kujua kwa kina sisi ni nani kama watoto wa Mungu na kutembea katika ukweli wa yote aliyotufanyia kupitia Yesu Kristo. Hii ndiyo maana Yesu alitwambia tuje kwake ili tupate pumziko. Wacha tuimalize safari yetu pamoja kwa kuona ni kwa nini pumziko ni kweli muhimu sana.

Mungu anajua kwamba tunahitaji pumziko na pia anajua ni kwa nini. Tumeona mara tena na tena kwamba uamuzi ambao mwanamume na mwanamke wa kwanza walifanya wa kutomtii Mungu ulikuwa na athari kubwa kwa jamii nzima ya wanadamu. Matendo yao yalibadilsha vile waliishi, na kutokana na hayo jinsi kila mtu ameishi tangu wakati huo. Kabla ya uasi wao, walifurahia uhusiano kamili na Mungu naye aliwakirimia kila kitu walichohitaji. Baada ya uasi wao, walipoteza uhusiano

wao na Mungu na wakaachwa wajitafute riziki, sio tu kimwili, bali pia kihisia na kiakili. Uhusiano kati yao na Mungu ulivunjika na waliachwaa peke yao kujua namna ya kuishi. Je, waweza kufikiria ukubwa wa tukio hilo?

Tunapotafuta kuelewa maana ya kweli ya pumziko, hebu tuzingatie tena tofauti nyingine kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Tukio lingine la Mungu kuwapa wanadamu pumziko tena lilifanyika alipowapa wana wa Israeli Sabato kama sehemu ya Agano la Kale. Fikira ya Sabato kuwa siku fulani ya wiki ilikuwa imekita mizizi ndani ya ufahamu wa Waebrania na haikuwezekana kwa Wayahudi wakati wa Yesu kufikiria vinginevyo. Mtazamo wa pumziko kuwa siku maaluma umeathiri sana ufahamu wetu pia na kutupa mtazamo finyu kuhusu Sabato. Sabato ina maana pana zaidi kuliko kuitenga siku moja pekee katika wiki tunapoacha kufanya kazi na kujitolea kumwabudu Bwana. Siku kama hii ina manufaa na huenda ikawa pendekezo zuri lililo halisi, lakini halitugusi sana katika nafsi yetu ya ndani tunapohitaji pumziko. Kabla ya kueleza umuhimu wa pumziko tunalopata ndani ya Yesu, ningependa kusema kwamba mbali na Yesu kuwa mwenye kutimiza Sabato—Yeye anatimiza kila kitu cha Agano la Kale.

Tumeona ndani ya kitabu hiki chote kwamba makusudi yote ya Mungu yanapatikana ndani ya Yesu Kristo na kupitia kwa Yesu Kristo. Sabato, kama sehemu nyingine zote za Agano la Kale, ilikuwa tu kivuli cha jambo fulani ambalo lingepata kudhihirika kamili ndani ya nafsi ya Yesu. Hili ndilo Paulo alimaanisha aliposema,

> Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo (Kol. 2:16-17).

We see this throughout the history of the Jewish people. ForTunaliona jambo hili katika historia yote ya Wayahudi. Kwa mfano, Musa alikuwa kiongozi mkuu zaidi miongoni mwa Waebrania. Alinena na Mungu ana kwa ana na akazipokea sheria ambazo Mungu aliwapa Waisraeli jangwani. Hata hivyo, Musa aliwaambia Waebrania, "Bwana Mungu wenu atawainulia nabii kama mimi kutoka miongoni mwa ndugu zenu wenyewe. Msikilizeni yeye" (Kum. 18:15 NEN). Kisha mtume Petro akatwambia katika Matendo 3 kwamba nabii huyo alikuwa Yesu na kwamba "kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake." (Matendo 3:23). Musa alijua vizuri sana kwamba huduma yake kwa Waebrania ilikuwa tu kivuli cha yale ambayo yangedhihirika ndani ya huduma ya Yesu (angalia pia Ebr. 3:1-6).

Damu ya kondoo wa Pasaka wa Agano la Kale ni mfano mwingine wa kuonyesha dalili. Ilikuwa matayarisho ya kuwasaidia Wayahudi kumtambua Yesu kama kondoo wa dhabihu. Mungu aliwaagiza wana wa Israeli wapake damu ya kondoo juu ya milango ya nyumba wakati wa usiku wa Pasaka ya kwanza kule Misri. Baada ya kukombolewa kutoka Misri walisherehekea mlo wa Pasaka kama kumbukumbu ya kile walichofanyiwa na Mungu, nayo ikawa desturi ya vizazi hadi vizazi chini ya Agano la Kale. Lakini haikutakiwa kuwa desturi ya kudumu. Kunyunyizia damu ya wanyama ulikuwa tu mfano wa dhabihu kuu na ya mwisho ambayo ingefanyika msalabani. Yesu alikuwa "Mwana-kondoo wa Mungu" (Yoh. 1:29, 36) na "wetu wa Pasaka" (1 Kor. 5:7) aliyefanyika kuwa dhabihu kamili na ya mwisho. "Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele (Ebr. 9:12).

Ukuhani wa Agano la Kale ulikuwa tu mfano wa ukuhani bora zaidi na kamili uliopatikana kupitia maisha ya Yesu. Hakutoka katika kabila la Lawi, lakini alitoka katika kabila la Yuda. Kabila hili halikuwa la makuhani. Licha ya hilo, tunajua kwamba "bali kwa nguvu za uzima usio na ukomo;" (Ebr. 7:16) Yesu alitangazwa "Wewe u kuhani milele Kwa mfano wa Melkizedeki" (Ebr. 7:17).

Yesu alisema kwamba mwili Wake ungechukua nafasi ya hekalu aliposema, “Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha” (Yoh. 2:19). Hekalu liliwakilisha kiini cha maisha ya Wayahudi—kidini, kidesturi, na kijamii. Kauli ya Yesu kusema kwamba mwili Wake ni hekalu ilikuwa ya maana zaidi kuliko kauli zote ambazo aliwahi kuwaambia Wayahudi.

Hii yote ni mifano ya timizo lililofanyika ndani ya Yesu. Pia kuna mifano mingine mingi ambayo Yesu tayari alikuwa kiini hata wakati wa Agano la Kale. Kwa mfano, Mungu aliwalisha wana wa Israeli mana iliyotoka mbinguni kila asubuhi kwa miaka arobaini wakiwa jangwani. Baadaye Yesu aliwaambia Mafarisayo, “Mimi ni chakula kilichoshuka kutoka mbinguni” (Yoh. 6:41). Yesu aliitumia kweli hii kimsingi aliposema, “Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake” (Yoh. 6:55-56).

Yesu hakuwa tu timizo bali pia kiini cha yote yaliyofanyika katika Agano la Kale. Bila kupata ufunuo wako mwenyewe kuhusu umuhimu wa Yesu katika mambo haya yote, hatuwezi kuelewa na kuishi katika ukweli kamili wa kile Mungu ametuwekea kama watoto Wake. Ukijaribu kuyafafanua mambo nje ya maisha ya Yesu Kristo utakosa kuelewa kiini cha kweli—Yesu!

Sabato ni mfano bora wa kweli ya Agano la Kale iliyopata kutizwa ndani ya Yesu Kristo. Historia ya wana wa Israeli inatuonyesha kwamba ingawa walishika vilivyo kanuni ya siku iliyoitwa Sabato, hawakuingia katika pumziko ya Bwana. Mwandishi wa Zaburi alitwambia kwamba kwa ajili ya uasi uliokuwa mioyoni mwao na kutoamini kwao, Mungu aliapa katika hasira yake, “...Hawataingia mahali pangu pa pumziko” (Zab. 95:11 BHN). Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alithibitisha kweli hii ambayo mwandishi wa Zaburi alizungumzia mamia ya miaka hapo awali (Ebr. 4:1-12). Hili linatuonyesha kwamba pumziko la kweli halihusu tu kutofanya kazi siku fulani, linahusu hali ya mioyo yetu. Kuhusu pumziko, Yesu alijali sana juu ya kweli kuu kuliko siku maalum. Vile Yesu alivyo haki, uzima na kusudi letu-Ndivyo alivyo Sabato yetu!

Yesu alisema,

> “Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi” (Mat. 11:28-30).

Yesu aliposema kwamba anataka kuzipa nafsi zetu pumziko anatuonyesha kitu ambacho ni kiini. Hili ni tatizo ambalo limemkumba mwanadamu tangu alipotenda dhambi ya asili ndani ya bustani ya Edeni. Tatizo hilo ni kuwa kuishi maisha kwa kutegemea nguvu na juhudi zetu wenyewe huweka mzigo mzito ndani ya nafsi zetu. Yesu aliahidi kwamba tukienda kwake nafsi zetu zitapata pumziko. Pumziko tunalohitaji si pumziko la mwili wetu. Bali, tunatarajia kupata pumziko linalotufanya tupate amani na kuridhika ndani ya nia na hisia zetu.

Kuna sababu mbili za nafsi zetu kuhitaji pumziko. Kwanza ni kwa sababu kabla ya kwenda kwa Yesu hatuna hakikisho la kuwa na uhusiano mwema na Mungu. Tumeshaona wazi kwamba Mungu amefanya kila kitu kinachohitajika ili tupokee kipawa cha uzima ndani ya Kristo, kinachotimiza hitaji letu la kuwa wenye haki mbele za Mungu. Hili huleta amani na pumziko ndani ya nafsi zetu (Rum. 5:1-2).

Sababu ya pili ya kuhitaji pumziko ndani ya nafsi zetu ni kwamba kuishi maisha bila Mungu hutuchosha! Hatukuumbwa kuishi maisha ya kujitegemea wenyewe na kutumia juhudi zetu wenyewe. Hii ni kweli ngumu sana kwa watu wengi, hasa katika ulimwengu wa sasa unaopigia debe nguvu, uhuru, na kujitegemea. Lakini kuishi hivi husababisha kuhangaika, kuishiwa nguvu, na uchovu ndani

ya nafsi zetu. Hii ndiyo maana Yesu alikuja kutuokoa na kutufunza njia mpya ya kuishi. Mungu anataka kutupatia uzima Wake. Tumwamini aishi ndani yetu na kupitia kwetu sisi. Nira yake ni rahisi na mzigo wake ni mwepesi. Aliahidi tukienda kwake, atazipumzisha nafsi zetu. Yesu alifahamu kwamba nafsi zetu ndizo zilihitaji pumziko, sio miili yetu pekee.

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anayajumlisha haya yote katika Waebrania 4. Aliwahimiza wasomaji wa kitabu hicho "asije akashindwa" kupata pumziko hilo (Ebr. 4:1 BHN) na kwamba "tujitahidi" kuingia katika pumziko hilo (Ebr. 4:11 BHN). Hii inamaanisha tunapaswa kutamani na kujitahidi kuingia katika pumziko. Aliwatumia wana wa Israeli kama mfano tusiopaswa kufuata. Sababu ya wao kukosa kuingia katika pumziko la Mungu ni kwamba walikosa kuiunganisha imani yao na neno la Mungu (Ebr. 4:2 BHN). Hiki ni kipengele muhimu tunachotakiwa kukiona. Lazima tuwe tayari kuonyesha imani yetu—kuamini na kutumaini—kile ambacho Mungu anatwambia ili tuweze kuingia katika pumziko Lake. Ikiwa hatuna imani, tutakosa pumziko.

Mwandishi wa Waebrania anaunganisha pumziko na hadithi ya uumbaji ambapo Mungu alipumzika siku ya saba. Hili ni wazo la kufurahisha. Siku ya mwisho ya kufanya kazi kwake, siku ya sita, Mungu alimuumba mwanamume na mwanamke. Uumbaji wa mwanamume mwanamke ulikuwa kilele cha yote ambayo Mungu aliumba katika kipindi hicho cha siku sita za kazi. Kisha Biblia inatwambia "siku hiyo ya saba Mungu akapumzika baada ya kazi yake yote aliyofanya" (Mwa. 2:2; Ebr. 4:4 BHN). Siku iliyofuata baada ya Mungu kumuumba mwanadamu, alipumzika. Hii ina maana kwamba siku ya kwanza ya maisha ya mwanadamu na ilikuwa siku ya kupumzika na Mungu!

Mungu alikuja ili akurejeshe katika pumziko na vilevile kumtegemea. Una nafasi ya kuingia katika pumziko lililo ndani yake. Amani kuu huja unapoamini kweli ya yote ambayo Mungu amekufanyia ndani ya Kristo. Yeye ni pumziko lako, na unapodumu ndani Yake uko salama katika uhusiano wako na Mungu. Unaweza kumtegemea, ukijua kwamba amekukirimia yote unayohitaji kuishi maisha ndani Yake kwa ukamilifu zaidi (2 Petro 1:3). Jua na pia uamini kwamba kukubaliwa na Mungu kunategemea yote ambayo Kristo amekufanyia. Hapa ndipo mwaliko wa Yesu unakuwa halisi katika maisha yako. Anataka umwendee Yeye kila siku na uingie katika pumziko Lake.

### *Kupata Kweli*

**Kweli:** Yesu ni mahali pako pa pumziko la kudumu. Yeye ni Sabato!

**Tamko la Imani:** Nimeacha kutambua tu wakati fulani au siku fulani ya kupumzika kwa sababu wazo hilo ni kivuli tu cha kile ambacho Mungu ameniahidi ndani ya Kristo. Kiini chote ni cha Yesu nami naingia ndani Yake na kupata pumziko kamili la nafsi yangu.

### *Kuenenda Katika Kweli*

Ianze kila siku kwa kujifungamanisha na kweli hii ya ajabu. Tambua kwamba Yesu ni pumziko lako, hata unapokuwa na shughuli nyingi. Amekualika uje kwake na uchukue nira Yake. Tambua Kwamba nira nyingine unazobeba ni nzito na ni mizigo. Zinakufanya uhisi uchovu ndani ya nafsi yako. Nira ya Yesu ni rahisi na nyepesi. Unavaa nira Yake, hupaswi kutenda mambo ili akuidhinishe na kukukubali. Unapojua kwa kina Yeye ni nani na yote aliyokutendea, unaweza kuishi ukiwa huru kabisa ndani Yake, na ataipatia nafsi yako pumziko!

# HITIMISHO

Ningependa kufunga kwa kuunganisha kila kweli muhimu sana niliyoelezea kwa kuwapa "kitabu changu cha kumbukumbu za kila siku" kuonyesha vile mimi huiweka kweli hii ndani ya uhusiano wangu na Mungu kila siku. Hii ni njia yangu mwenyewe ya vile ninavyothibitisha kweli hii maishani mwangu baada ya miaka mingi ya kutembea na Bwana. Kweli hii imeunda imani yangu na kuniathiri kwa kiwango cha kina iwezekanavyo.

Natumaini na naomba kwamba unaposoma hitimisho hili utaona vile Bwana anataka kweli hii ikuweke huru kwa kiwango cha kina kikuu. Huenda hata ukataka kuitumia kama kifaa katika ibada yako binafsi, kusoma na kukiri kweli hiyo juu ya maisha yako mwenyewe; au huenda ukataka kuiandika tena na kuifanya ikufae zaidi unapohisi kweli hii ikikuweka huru.

*Ninavyoishi Maisha Yangu Kulingana na Kweli Muhimu Sana*

Nina imani kuu na ya kudumu na pia nasadiki kwamba Mungu ana kusudi kuu linalowahusu watu wote. Atatimiza kusudi hilo kupitia Mwanawe, Yesu Kristo. Mungu aliamua kabla ya kukiumba kitu chochote kwamba kusudi hili lingekuwa njia atakayoifuata katika nyakati zote na milele. Alipomuumba mwanamume na mwanamke, aliwaumba akiwa na nia ya kuwa na ushirika wenye upendo kwa kushiriki nao maisha yake. Mwanadamu alipotangaza hali ya kutomtegemea Mungu kwa kuasi katika bustani ya Edeni, Mungu alianza mfululizo wa matukio yaliyodhihirika katika historia yote ili kuturudisha mahali pa kuwa na ushirika kamili na kuungana naye. Hili lilitimizwa kwa kumtuma Mwanawe Yesu Kristo duniani kuishi na mwanadamu na kutuonyesha mfano wa maana ya kuishi maisha ya kumtegemea Mungu kwa ukamilifu ili kupata kila kitu.

Nimeitwa na Mungu kulingana na **kusudi** Lake la milele katika Kristo Yesu. Kusudi hili ndilo huamua yote afanyayo Mungu ndani ya maisha yangu kila siku. Anataka niwe kama Mwanawe Yesu Kristo kabisa. Anatumia kila kitu ninachopitia maishani mwangu kunifanya nifuate mfano wa Yesu. Ninavyoishi maisha yangu, naishi nikijua kwamba hiki ndicho Mungu anaendelea kufanya.

**Mtazamo** wangu umebadilika kabisa kwa vile nimekuja kuelewa, kwa kufunuliwa na Roho aliye ndani ya maisha yangu, kwamba nikiwa ndani ya Kristo mimi ni kiumbe kipya. Nina asili mpya kabisa. Mimi ni sehemu ya mtu mpya aliye ndani ya Kristo, na mtu huyu ni mwenye haki na mtakatifu. Haki yangu mwenyewe ni halisi na kweli. Si kitu cha kiteolojia au cha uwezo. Mungu ananijua tu nikiwa ndani ya Kristo. Kwa kuwa niko ndani ya Kristo, Kristo ananifanya mwenye haki, mtakatifu, na asiyekuwa na lawama. Mungu hatafuti makosa ndani yangu. Jambo hili linaniletea usalama mkuu na furaha ndani ya maisha yangu. Kwa kuwa mimi ni mtu wa kiroho sasa, nina uwezo wa kuyaona mambo vile ayaonavyo Mungu. Kuyaishi maisha nikiwa na mtazamo wa Mungu kunabadilisha ninavyopitia kila sehemu ya maisha yangu.

Nafahamu kwamba nimepewa **neema** ya Mungu kupitia uzima wa Yesu. Neema Yake huniwezesha kushiriki katika maisha ya Mungu na kuishi maisha yangu ndani Yake. Siyaishi maisha yangu kwa

nguvu na juhudi zangu mwenyewe, bali kwa neema tu, ambayo ni uwepo wa Mungu ndani yangu.

Naamini kwa **imani** na kutumaini kabisa kwamba Kristo anaishi ndani ya mwili wangu kwa uwepo wa Roho Wake aliyenipa. Naamini Kristo ni kiini cha maisha yangu nami naamua kila siku kwamba ataishi ndani yangu, kupitia kwangu, kama mimi, ninapomwamini afanye hivyo. Anaweza kabisa kuishi maisha Yake ndani yangu nikiwa chombo Chake. Kadri ninavyoamini zaidi kweli hii na kujinyenyekeza kwake, Yeye anayageuza maisha yangu kuwa katika mfano Wake.

Najua kwamba kwa ajili iya imani yangu kwa Mungu, amenifanya kuwa mwenye haki kabisa. Hii ina maana kwamba nina haki mbele za Mungu na hakuna ninachotakiwa kufanya kukubaliwa naye au kutimiza matakwa Yake. Nimekuwa **haki** ya Mungu ndani ya Kristo Yesu. Mungu amependezwa nami, na ninaweza kuishi nikiwa na hakika kabisa kwamba nimekubaliwa na napendwa kila wakati.

Roho mtakatifu aliponifunulia kwamba nilikuwa mwenye dhambi na nilihitaji kuungama dhambi zangu mbele za Mungu na kukubali kipawa cha bure cha Mungu kupitia kwa Kristo Yesu kwa imani, niliamua kuamini na kuweka imani yangu ndani Yake. Nilipofanya hivyo, nilipokea **msamaha** wa Mungu wa dhambi zangu zote—za kale, za sasa, na za siku za usoni. Najua kwa hakika kwamba tangu wakati huo dhambi zangu zote zimesamehewa. Huwa sijiulizi iwapo Mungu atanisamehe. Ikiwa nitafanya kitu chochote cha dhambi, ameshanisamehe, na ninachotakiwa tu kufanya ni kuishi kwa kufahamu msamaha Wake uliopatikana kupitia damu ya Yesu iliyomwagika. Siishi nikijiona kuwa mwenye dhambi kwa sababu najua kwamba damu ya Yesu imeisafisha dhamiri yangu.

Sihitaji kuzihesabu dhambi zangu tena kwa sababu zimesamehewa na Mungu ameamua kutozikumbuka tena. Mimi kama mtoto wa Mungu, sihitaji **kuungama** ili nipate msamaha wa Mungu. Situmaini kwamba Mungu atazisamehe dhambi zangu, wala sihitaji kuishi nikiwa na hofu kwamba nisipoungama dhambi zangu kwake hatanisamehe. Najua kwamba alinisamehe kabisa Yesu alipokufa msalabani, na kwamba nilipata msamaha huo binafsi nilipomwamini mara ya kwanza. Hakuna uhusiano wa sababu na athari kati ya kuungama na kusamehewa katika maisha yangu kwa sababu hiyo ingemaanisha kwamba damu ya Yesu haikumtosha Mungu hivyo basi kuungama kwangu kungehitajika. Hili lingekanusha imani na kudhoofisha kiini cha injili.

Naamini kwamba mimi mwenyewe nimepitia kusulubiwa, kifo, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu. Hili lilifanyika kwa sababu nilikuwa ndani ya Kristo alipoyapitia mambo haya. Chochote alichopitia, nilikipitia. Ingawa hili ni fumbo, si kwa ajili hii. Kwa vile nilikufa na Kristo, niliifia dhambi kabisa. **Dhambi** haina nguvu juu ya maisha yangu tenda. Nimeifia Dhambi, na sasa niko hai kwa Mungu kupitia Kriso Yesu. Shughuli ya maisha ya Yesu inayofanya kazi ndani yangu imeniweka huru kutokana na kanuni ya Dhambi na mauti iliyokuwa ikitenda kazi ndani ya maisha yangu. Hii inamaanisha kwamba niko huru kutokana na Dhambi!

Kwa siku zangu zilizosalia hapa duniani nitapitia hali ya kuishi ndani ya mwili wa kawaida. Katika hali hii ya kawaida, **Mwili** bado uko ndani yangu. Hii ni sehemu ya maisha yangu iliyo na uwezo wa kufanya mambo nisiyotaka kufanya. Lakini Mungu amenipa Roho Wake na vilevile wingi wa neema Yake na maadamu ninachagua kuenenda katika Roho, sitatimiza tamaa za mwili wangu. Nikitambua sehemu yoyote ya maisha yangu inayotoka kwa mwili, naweza, kwa imani, kuipelekea sehemu hiyo msalabani na kuisulubisha isiwe tena na nafasi ndani ya maisha yangu.

Najua kwamba **Roho** wa Kristo, ambaye ni Roho wa Mungu, anaishi ndani yangu. Roho wake anaendelea kunishuhudia kwamba mimi ni mtoto Wake. Roho Wake hunifundisha yote ninayohitaji kujua kuhusu Mungu na ananiongoza kwa kweli yote iliyo ndani ya Kristo Yesu. Roho, aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu, huupa mwili wangu uzima ili udhihirishe uzima wa Kristo kupitia kwangu kila siku.

Natambua kwamba katika maisha haya nitapitia **Mateso**. Naamini kwamba Yesu yuko nami kila wakati. Yuko nami, na pia anatenda kazi na kuyafanya mateso ninayopitia yawe na thamani kuu. Huenda nisiione thamani hiyo sasa au hata katika maisha haya, lakini naamini kabisa kuna utukufu wa milele ambao mateso niyapitiayo yatanifanyia. Ninamjua Kristo zaidi kupitia mambo yote niyapitiayo. Pia nachagua kuyaona mambo yote yaliyo ndani ya maisha yangu kuwa hasara ili niweze kumpata Kristo. Ninaamua kutoweka kitambulisho change ndani ya nguvu zangu na mafanikio yangu na ninatamani tu kumjua Yesu zaidi.

Kweli hii yote inaelekeza kwa kila kitu ambacho Mungu amenifanyia katika Kristo ili niwache kung'ang'ana na niweze kupata **Pumziko** Lake na amani Yake. Wakati ninajua na kuamini kweli ndani ya nafsi yangu, Yesu ataniongoza kuingia katika pumziko lake. Pumziko hili hunifanya kuwa na amani na mimi mwenyewe, na Mungu, na wengine walio karibu nami. Ni jambo kuu kujua kwamba Mungu anapendezwa sana nami na kwamba mimi ni mtoto Wake mpendwa.

Najua kwamba Mungu amefaulu kabisa kufanya kila kitu kilichohitajika ili kutimiza shauku lake la kunirejesha kwa ushirika kamili na Yeye na pia kuunganishwa naye kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo.

Kweli muhimu sana inayabainisha maisha yangu nami naishi kila siku na ufahamu huu usiobadilika. Kama yule aliyekubali kweli hii, naishi kama Mkristo. Naomba kila siku. Nasoma Maandiko. Nawaelezea wengine kuhusu imani yangu, Bwana anaponipa nafasi. Mimi hutoa. Namwamini Mungu. Nashiriki na waumini wengine. Natumia karama za kiroho na mengine mengi. Yote haya ni madhihirisho ya kawaida ya maisha ya Kristo yaliyo ndani yangu lakini hayaamui kitambulisho changu. Nikiyafanya zaidi, au nisipoyafanya, hayawezi kubadilisha kweli ya ambacho Mungu amenifanyia kupitia kwa Kristo Yesu.

Nimejua kweli na kweli imeniweka huru!

# OMBI LA BARAKA

Ombi la baraka hutamka baraka juu ya watu. Mara nyingi hufanywa mwisho wa ibada ya kanisa. Waandishi wa Agano Jipya pia waliandika ombi la baraka mwisho wa barua zao kwa makanisa.

Tukio lililokuwa na maana sana la ombi la baraka lilifanyika nilipokuwa katika chuo cha seminari. Mmoja wa wahadhiri wangu, Dkt. E. Earle Ellis, mara nyingi alitamka ombi la baraka alipomaliza mhadhara wake. Dkt. Ellis alikuwa mtu wa pekee na wa ajabu. Hakuoa maisha yake yote na alikuwa amejitolea kabisa kwa masomo yake. Kama mwanateolojia bora zaidi wa kimataifa, alichangia pakubwa katika masomo yanayohusu mafundisho ya Paulo na vilevile kuandika ufafanuzi wa vitabu mbalimbali vya Agano Jipya. Aliishi ndani ya ulimwengu wake mwenyewe wa mtindo wa nyuma sana wa kuvaa suruali ndefu za polyesta, mashati ya kola pana, na tai nyembamba ya ngozi.

Mimi na Stefani tulipata fursa ya kukuza uhusiano wetu na Dkt. Ellis na tulimkaribisha nyumbani kwetu mara kadhaa. Katika ushirika wetu naye, Dkt. Ellis angezungumza nasi kuhusu uhakika aliopata alipokuwa na ushirika wake binafsi na Bwana Yesu. Maisha yake ya kusoma, na kuzama zaidi ndani ya Maandiko, yalidhihirika katika ufahamu mkuu wa Mungu na yalinitia moyo nikiwa mwanafunzi aliyekuwa na hamu kuu ya kumjua Mungu.

Mwisho wa mihadhara yake, Dkt. Ellis angefunga kitabu chake na kutwambia tusimame. Akiwa amenyosha mikono yake miembamba na mirefu kuelekea tulikokuwa, viganja vya mikono yake vikiwa wazi, angenena maneno mazuri sana ya baraka juu ya maisha yetu kutoka moyoni mwake na kutoka kwa Maandiko. Macho yake yakiwa yamejaa machozi, angemaliza ombi lake la baraka na kuondoka darasani mara moja kurudi katika maisha yake yenye fumbo ya mwanateolojia aliyeishi peke yake. Dkt. Ellis aliyaathiri maisha yangu vilivyo na akapanda mbegu za ufahamu ambazo zimekua na kukomaa katika miaka thelathini iliyopita.

Kwa heshima ya Dkt. Ellis, ambaye sasa yuko katika uwepo wa Yesu, nafanya ombi la baraka juu ya maisha yako.

Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, akufanye wewe kuwa mkamilifu katika kila tendo jema, upate kuyafanya mapenzi yake, naye afanye ndani yako lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo. Akuimarishe kabisa na uwe thabiti katika ufahamu sawasawa na mfano wa Mwanawe, na akuwezesha kuenenda katika uhalisi wa kweli yote iliyo ndani Yake, na akuhifadhi uwe mwaminifu hadi mwisho. Bwana akubariki na akulinde, Bwana akuangazie nuru ya uso wake na kukufadhili. Bwana akugeuzie uso wake na kukupa amani. Utukufu ni wake milele na milele. Amina (Ebr. 13:20-21; Col. 3:10; 2 Pet. 1:8; Hes. 6:24-26).